

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 9 Februari, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Mwaka ya Upimaji wa Utekelezaji wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kwa Mwaka 2016/2017 *(Annual Performance Evaluation Report on Public Procurement Regulatory Authority for Financial Year 2016/2017)*.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 108

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapelaka fedha za kutosha kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga ambao umeanzishwa kwa nguvu za wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kupitia fedha za ruzuku kutoka Serikalini imekamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), nyumba moja ya mtumishi pamoja na jengo la kutolea huduma za ushauri nasaha ambalo liko katika hatua ya upauaji. Jumla ya shilingi milioni 365 zilitumika kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao:-

Ruzuku kutoka Serikali Kuu shilingi milioni 267; mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya shilingi milioni 86; nguvu

za wananchi shilingi milioni saba na mchango wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 110 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo ambapo kati ya hizo shilingi milioni 40 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na shilingi milioni 70 ni ruzuku kutoka Serikali kuu. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zitatengwa shilingi milioni 110 kwa ajili ya kendeleza ujenzi wa hospitali hiyo ambapo shilingi milioni 50 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na shilingi milioni 60 ni ruzuku kutoka Serikali Kuu. Serikali itaendeleza ujenzi wa hospitali hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha ili wananchi waweze kupata huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azza Hillal, swali la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikuliza swali hili toka nilivyoingia ndani ya ukumbi huu mwaka 2010. Ujenzi wa hospitali hii umeanza toka mwaka 2007 mpaka hivi tunavyoongea fedha inayoonekana hapo ndiyo ambayo imeshafika katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, lakini wakati nauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, nipongeze Serikali kwa hatua kubwa ambayo wameamua kuchukua katika uboreshaji wa vituo vya afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Tinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, je, Serikali inawaahidi nini wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kuhusu ukamilishwaji wa ujenzi huu kwa kuwa umekuwa ni wa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, Serikali imeweka mpango gani madhubuti ili kuhakikisha kwamba pindi ujenzi huu wa vituo vya afya unapokuwa umekamilika unaweza kupata wataalam wa kutosha katika majengo yetu ya upasuaji na huduma zingine zinazostahili? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika na mimi tangu nimemfahamu Mheshimiwa Azza amekuwa akipigania ujenzi wa hospitali, lakini kama hiyo haitoshi ni pamoja na kupigania Vituo vya Afya na Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Naomba kwa pekee nimpongeze kwa jitihada zake hizo na ndizo ambazo zimezaa upatikanaji wa vituo vya afya viwili, kwa maana ya Kituo cha Afya Tinde na Kituo cha Afya Samuye ambacho kimoja ni shilingi milioni 400 na kingine milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija upande wa maswali yake, anataka ahadi ya ukamilishaji wa hospitali hizo. Kama ambavyo nimekuwa nikijibu hapa, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa hospitali 64 katika Wilaya ambazo hazina Hospitali za Wilaya na hasa kwa wananchi wa wilaya yake ambao wameshaonesha moyo kwanza kwa kutenga eneo lakini pia ujenzi umeshaanza na ndio maana *OPD* imeweza kukamilika. Kwa kadri bajeti itakavyoruhusu hakika naomba nimuhakikishie tutatupia jicho letu kuhakikisha kwamba hospitali hiyo inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ametaka kujua juu ya suala zima la hospitali inapokamilika na wataalam wawepo. Naomba nimuhakikishie, ni azma ya Serikali, si suala la kujenga majengo tu, tunataka tujenge majengo ambayo yatumike. Kwa hiyo, pale ambapo ujenzi unakamilika na wataalam watakuwa wamepatikana ili waweze kutoa huduma kwa wananchi waliokusudiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata, swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Vijiji vya Kasu, Milundikwa, Katani, Kisula pamoja na Malongwe, Kata ya Kandanse wameamua kujenga Kituo chao cha Afya Kasu na wadau mbalimbali wameonesha kuwachangia ikiwepo Mfuko wa Jimbo. Je, Serikali ipo tayari kuwaunga mkono juu ya juhudi zao hizo za kupata Kituo cha Afya? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ninafahamu Mheshimiwa Mipata na mwenzake Mheshimiwa Keissy katika Wilaya yao kule wamefanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha ajenda ya afya na ndiyo maana nilipofika pale nimeona jiografia ya Wilaya ya Nkasi ina changamoto kubwa sana. Hii ndiyo maana katika kipaumbele chetu, kwa kuunga mkono wananchi wa Kasu, tumehakikisha kwamba katika kipindi cha hivi karibuni tutawezesha Kituo cha Afya cha Kasu na Wampembe kuhakikisha kwamba vile vituo vya afya viwili vya maeneo hayo viweze kupata huduma ya upasuaji kwa lengo kubwa kwamba *population* iliyopo kule na wengine kutoka nchi jirani muweze kuhakikisha mnawa-*manage* vizuri katika sekta ya afya.

Kwa hiyo, hilo tumeliangalia na tunalipa kipaumbele. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Heche, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tarime tumejitahidi na Mheshimiwa Kandege alikuwepo, tumejenga hospitali kubwa pale ya Wilaya ambayo iko Nyamwaga, tumejenga vituo vya afya karibia vine, kuanzia Nyandugu, Mriba na Sirari ambako ni kituo ambacho Waziri Mkuu alisema kiwe cha mfano nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa shida yetu ni watumishi, ni lini mnatuletea watumishi hasa kwenye Hospitali ya Nyamwaga ambayo tumeshanunua na vifaa ili ile hospitali ianze kuhudumia wananchi wa Tarime ambao wamefanya kazi kubwa pale kujenga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maneno kwamba wakifanya vizuri upande wa Upinzani hatuwapongezi, lakini kwa dhati kabisa naomba nipongeze kazi nzuri ambayo imefanywa na wananchi wa Tarime akiwepo na Mbunge Mheshimiwa Heche kwa sababu tumeenda tukatizama kwa macho na kuona ni kusadiki, mmefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Heche atakubaliana na mimi kwamba katika ziara aliyofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliahidi kwamba taratibu zikamilike mara moja ili Hospitali ya Nyamwaga ianze kufanya kazi na tena ni matarajio yetu kwamba muda sio mrefu itakuwa ni miongoni mwa Hospitali za Wilaya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kakonko ni kati ya wilaya mpya na mpaka sasa Wilaya hiyo haina Hospitali ya Wilaya. Eneo hilo la Kakonko limepakana na Mkoa wa Kagera na wananchi wengi wanakuja kutibiwa katika Kituo cha Afya cha Kakonko kwa kuwa hawana hospitali jirani yao. Serikali iliahidi kupeleka shilingi milioni 500, mpaka sasa shilingi milioni 500 hizo hazijapelekwa katika Wilaya ya Kakonko. Nilitaka kujua, je, ni lini Serikali itapeleka milioni 500 ili wananchi wa Kakonko waweze kupata huduma ya matibabu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kakonko ni sehemu yenye changamoto kubwa na Mheshimiwa Mbunge nakumbuka hata tulivyokuwa kule kipindi kile tumeona idadi kubwa ya watu kutoka Burundi wakitibiwa pale katika kituo kile cha afya.

Ni kweli tumetenga shilingi milioni 500 na nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zile zilikuwa zinaenda awamu kwa awamu. Ni imani yangu kwamba sasa hivi kwa muda huu ninapozungumza katika ile *batch* ya mwisho zitakuwa zimefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ondoa hofu ndani ya kipindi hiki nina amini, lakini nita-*cross check* leo hii kwa nini hazijafika kwa sababu tumeshazitengea zile fedha ziende Kakonko kwa ajili ya uboreshaji wa kituo kile cha afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela na Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla King, Mbunge wa Makete sasa aulize swali lake.

Na. 109

**Kusuasua kwa Miradi ya Maji Jimbo la Makete**

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING** aliuliza:-

Mwaka 2013 Serikali ilianza kutekeleza mradi wa maji wa Kata za Kinyika na Matamba katika Wilaya ya Makete lakini mradi huo haukufanikiwa kutokana na Serikali kutoa maelekezo ya kulaza mabomba ya inchi 2.5 na 4 badala ya inchi 8 kwenye mradi wa kilometa 18; mradi wa maji wa Tarafa za Magoma na Bulongwa ulijengwa muda mrefu wakati idadi ya watu ikiwa ndogo lakini sasa idadi ya watu na matumizi vimeongezeka.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Tarafa ya Matamba?

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Tarafa ya Bulongwa ili Kata za Bulongwa, Kipagalo na Luwumbu ziweze kupata maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Norman Sigalla King, Mbunge wa Makete lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Kata ya Matamba na Kinyika unaosambaza huduma za maji kwenye vijiji tisa ulianza kujengwa mwaka 2007 na ulikamilika mwaka 2014. Kabla ya ujenzi kuanza usanifu wa mradi huo ulilazimika kubadilishwa ili kutumia bomba la inchi 4, 2 na 1.5 badala ya bomba la inchi 8 kulingana na fedha zilizokuwepo kwani gharama za mradi kwa usanifu wa awali zilikuwa kubwa zaidi. Kutokana na ongezeko la watu kutoka 12,019 mwaka 2007 hadi 17,686 kwa sasa mradi huo haukidhi mahitaji. Ili kukidhi mahitaji Serikali inakamilisha usanifu wa



mradi utakaotoa maji Mto Misi ambapo ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mradi wa maji Bulongwa na Magoma unaohudumia vijiji 14 uliojengwa mwaka 1984 haukukidhi mahitaji ya sasa na miundombinu yake ni chakavu. Serikali imeanza ukarabati wa mradi ambapo hadi sasa bomba jipya kwa umbali wa kilometa nne limelazwa na linahudumia Vijiji vya Unyangogo, Iniho na Mwakauta. Mchakato wa kumpata mkandarasi atakayetekeleza awamu ya pili ya ukarabati huo unaendelea ili kukarabati bomba kwa umbali wa kilometa mbili. Ukarabati wa mradi mzima unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 30, 2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla swali la nyongeza.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na pia natambua kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikifanya kazi nzuri kwenye suala maji. Nina maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni kweli kabisa kwamba tangu mradi huu uanze, wananchi wa Matamba, Nakinyika, Itundu na Mlondwe hawajawahi pata maji hayo. Nini kauli ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inakamilisha mradi huo?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Tarafa hii ya Matamba pia linafanana sana kwenye Kata za Tandala, Mang'oto pamoja na Ukwama; nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba pia Kata hizi tatu zinapata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Norman Sigalla, nimefanya ziara kule na hilo tatizo nililikuta,

kwamba mradi umetekelezwa lakini wananchi hawapati maji, lakini pia wananchi wameongezeka na tukakubaliana. Tumetengeneza mpango ambao utakuwa na gharama ya zaidi ya bilioni nne, na tutatekeleza miradi katika eneo lake katika hiki kipindi cha miaka miwili iliyobaki kwenda mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Norman Sigalla, amesimamia Halmashauri, andiko wameleta, tunakamilisha kulifanyia kazi ili utekelezaji uendelee. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Norman Sigalla pamoja na wananchi wa Matamba na Kinyika kwamba Serikali ya CCM itahakikisha ikifika 2020 wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza mradi mkubwa sana wa maji wa kutoka Ziwa Victoria kwenda Tabora na mradi huo kuna kipindi vifaa vya ujenzi vilikuwa vina mikwamo kwamo. Swali langu ni dogo tu, je, mradi huo umefikia kwenye hatua gani ya utekelezaji na wananchi wa Tabora wategemee kupata maji hayo lini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji unaendelea vizuri sana, tulikuwa na matatizo machache ya kuhusu masuala ya msamaha wa kodi lakini tumeshayamaliza, na Mheshimiwa Mbunge wewe mwenyewe ni shahidi; wakandarasi wote watatu wameshaanza kazi, mabomba wanaendelea kuleta na sasa hivi kama unaenda barabara ya kwenda Dar es Salaam

utakutana na malori yanabeba mabomba kupeleka Tabora; kwa hiyo mradi unaendelea vizuri. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Theonest Lwehikila, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo changamoto kubwa sana ya barabara kutokana na mitandao ya maji na hasa katika kata mbalimbali za Jimbo la Segerea ikiwemo Kata ya Vingunguti; je, ni kutokana na ubovu wa mabomba ndiyo maana tunazidi kuona maji yanazidi kutiririka hovy katika maeneo haya?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, changamoto hiyo ipo. Kama tunavyokumbuka, wakati nilipotembelea barabara ya Kwa Mnyamani kutoka hapa Buguruni barabara ya Kwa Mnyamani kwenda Vingunguti, barabara ile muda mwingi sana maji yamejaa barabarani' Tatizo kubwa ni kwamba yale mabomba yanapasuka kwa hiyo yanajaa barabarani na barabara inaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana nilitoa agizo pale kwamba Manispaa yetu ya Ilala, *TARURA* pamoja na *DAWASCO* waweze kukaa pamoja kuangalia ile miundombinu yote ambayo iko barabarani iwekwe vizuri. Bahati nzuri zoezi hilo limekamilika, hivi sasa linaendelea vizuri, niwashukuru sana *DAWASCO*, pia niwashukuru Manispaa ya Ilala kwa kazi kubwa waliyofanya, na hivi sasa hata ile barabara tunaiboresha, sasa itakuwa kwa kiwango cha lami yote kuanzia hapa Buguruni tunapoingilia mpaka unafika Vingunguti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limefanyika shirikishi, kwamba maeneo hayo sasa yawe yanapitika vizuri, vilevile na mitandao ile ya maji ambayo inachanganyana

sana wataalam nimewaagiza waiweke vizuri kuhakikisha kwamba tunalinda barabara zetu hizi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shukuru Kawambwa swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani za wananchi wa Bagamoyo kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa namna ambavyo amesimamia ujenzi wa tenki kubwa la maji Bagamoyo, swali langu ni kuwa, je, lini mradi wa usambazaji wa mabomba ya maji katika Mji wa Bagamoyo pamoja na kata zote za Bagamoyo utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Mkoa wa Dar es Salaam tunakaribia kuikamilisha. Baada ya kupata vyanzo vya maji tunayo maji ya kutosha, tuliweka makadirio ya dola milioni 100 kwa ajili ya usambazaji. Awamu ya kwanza tulipata dola milioni 32 na miradi hii inaendelea, ndiyo ambayo imejenga hilo tenki analolisema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi tumepata tena dola milioni 45 na mwezi huu tunatangaza *tender* ili tuweze kupata mkandarasi ili ahakikishe kwamba sasa tunaweka mabomba ya kusambaza maji katika maeneo yote likiwemo eneo la *EPZ* kule Bagamoyo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake kwamba huduma ya maji katika eneo lake tunakamilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Zungu, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa namna inavyofanya maendeleo nchini, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa namna yeye na timu yake wanavyohangaikia maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Waziri akisema juu ya barabara za lami na mabomba kuanzia Buguruni kwenda Vingunguti, sikumsikia akisema kwenye eneo ambalo kodi ndiko zinakokusanywa, kuanzia Buguruni kurudi mjini. Je, maeneo haya ya Buguruni kurudi mjini barabara za lami na maji vipi Mheshimiwa Waziri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli jambo la maji na barabara ni mtambuka lote kwa pamoja nafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Zungu kwanza kuhusu suala la hiyo mitandao ya barabara na maji tumetoa maelekezo, lakini hata hivyo tukija katika upande wa barabara, Mheshimiwa Zungu ofisi yetu itafanya kila liwezekanalo kuhakikisha kwamba Jimbo lile la Ilala kupitia Mradi wa *DMDP* jimbo lako litaweza kuwa linang'ara zaidi kwa sababu hili ni jukumu la ofisi yetu, na kwa vile unapigana sana kwa wananchi wako, jambo hili tunalibeba na tunalisimamia kwa nguvu zote kwa kipindi hiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali namba 110, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe sasa aulize swali lake.

Na. 110

## Ahadi ya Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Karagwe

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wa Karagwe wamekuwa wakiahidiwa kujengewa Hospitali ya Wilaya na taratibu zote zimekuwa zikifuatwa kupitia Vikao vya Baraza la Madiwani na *RCC* lakini maombi haya hutupiliwa mbali na TAMISEMI.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa hospitali hii ambayo pia ipo kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetenga eneo la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na kupitishwa kwenye vikao vya kisheria ili kutekeleza shughuli ya ujenzi. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 imetengwa shilingi milioni 70 kutoka kwenye fedha za mapato ya ndani na shilingi milioni 60 kutoka kwenye ruzuku ya miradi ya maendeleo (*CDG*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imeweka kipaumbele na kutenga shilingi milioni mia moja ili kuendelea na ujenzi wa hospitali hiyo endapo Bunge litaridhia maombi hayo. Chanzo cha fedha hizo ni mapato ya ndani shilingi milioni 50 na shilingi milioni 50 zitatokana na ruzuku ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, na pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Selemani Jafo na Dada Jenista Mhagama. Baada ya kufika Karagwe na kukuta wilaya ambayo ina watu takribani 360,000 ina Kituo cha Afya kimoja cha Serikali waliweka nguvu na Serikali sasa imetusaidia tumekamilisha hicho Kituo cha Afya cha Kayanga, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa vile Wilaya ya Karagwe ina Kituo cha Afya kimoja cha Serikali, na hivi sasa naishukuru TAMISEMI tunaenda kukamilisha Kituo cha Afya cha Nyakayanja, mnaonaje wakati mchakato wa kujenga Hospitali ya Wilaya unaendelea mtupe angalau vituo vya afya viwili ili ku-*balance* jioografia ya Karagwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa TAMISEMI na Wizara ya Afya wanafanya kazi nzuri, mnaonaje mkae na *development partners* kwa sababu Kamati ya Huduma za Jamii inaonesha kwamba kuna Wilaya 67 katika nchi yetu ambazo bado hazina Hospitali za Wilaya. Sasa kwa sababu Serikali inafanya kazi nzuri ya kutoa huduma mnaonaje mkae na *development partners* ili mtengeneze *proposal* ambayo itatusaidia kukamilisha ujenzi wa Hospitali 67 za Wilaya? Nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, maibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza ndugu yangu, Mheshimiwa Bashungwa kwa jinsi ambavyo anapigana katika jimbo lake kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapata huduma ya afya iliyo bora. Katika maelezo yake anaongelea kwamba kuna kituo cha afya kimoja, ni kiu yake kwamba vituo vya afya vingengezeka walau viwili tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya afya vinajengwa katika maeneo yote na kwa kufuata uwiano sawia. Kwa hiyo, katika awamu inayokuja naomba nimhakikishie kwamba walau tutahakikisha kwamba kituo kingine cha afya kinapelekwa kule haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili anauliza uwezekano wa Serikali kushirikiana na *development partners* katika kuhakikisha kwamba tunaenda kumaliza tatizo la ujenzi wa Hospitali za Wilaya. Ni nia ya Serikali na milango iko wazi kwa yeyote yule ambaye ana nia njema ya kusaidia Serikali katika ujenzi wa Hospitali za Wilaya, tunamkaribisha, ilimradi katika yale masharti ambayo yatakuwa si ya kudhalilisha nchi yetu, sisi kama Serikali tuko tayari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mchemba, swali la nyongeza.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Tabora Wilaya mbili hazina Hospitali za Wilaya, Sikonge na Tabora Manispaa na viwanja tayari vipo, je, Serikali inasema nini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, ambaye wakati tumefanya ziara kwenda Kilolo yeye ndio alikuwa Mwenyekiti wa Kamati na akashuhudia kazi njema ambayo inafanywa na Serikali, Hospitali ya Wilaya ya Kilolo itakuwa miongoni mwa hospitali za kutilia mfano. *(Makofi)*



Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika swali lake anasema Serikali inasema nini kuhusiana na Wilaya mbili za Sikonge na Tabora Mjini ambazo hazina Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya mwanzo, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo hakuna hospitali za wilaya zinajengwa ili kupunguza mlundikano wa wagonjwa kwenda katika Hospitali za Rufaa ili wale ambao wanaweza kutibiwa katika Hospitali za Wilaya waweze kutibiwa. Naomba niombe Halmashauri, ni vizuri na wao wakaonesha kwamba ni hitaji la wananchi kwa hiyo na wao katika vyanzo vyao vya mapato waanze pia ujenzi ili na Serikali Kuu tuweze kushirikiana nao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Tunduma na Wilaya yetu ya Momba kulikuwa na majengo ambayo yalikuwa yanatumika na Kampuni ya CC iliyokuwa inajenga barabara ya kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga. Majengo hayo yaliteuliwa kwamba yangeweza kutumika kama Hospitali ya Wilaya, lakini sasa hivi inaonesha kuna mabadiliko. Waziri anawaambia nini wananchi wa Mji wa Tunduma kuhusiana na majengo yale kwa sababu aliwahakikishia kwamba itakuwa Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Namuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nitaenda kufanya *follow up* kujua kwamba ni Waziri gani alitoa *commitment* hiyo.

Jambo la pili, nafahamu wazi kwamba kuna maeneo mengi sana majengo yaliyokuwa yakitumika na wenzetu wa Wizara ya Ujenzi, hasa yale makampuni, majengo yale mengi sana yameombwa kwa ajili ya ama vituo vya afya au maendelezo ya Hospitali za Wilaya. Ninafahamu wazi kwamba Tunduma kuna changamoto kubwa kwa sababu idadi ya watu pale ni kubwa na ndiyo maana tunaanza ule ujenzi wa kituo cha afya, japokuwa umekuwa ukisuasua lakini tutasimamia kwa karibu ili uweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo hilo ndugu yangu Mheshimiwa Mwakajoka naomba niseme kwamba tunalichukua kwenda kulifanyia tathmini kuona nini kimekwamisha, kwa sababu hatimaye tunataka wananchi wa Tunduma wapate huduma vyema kabisa. Kwa hiyo tutalifanyia kazi Serikali kwa ujumla wake wote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 111

### **Kuunganisha Mfumo wa EPICOR, LGMD na LAWSON**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, ni lini Mfumo wa *EPICOR, LGMD* na ule wa *LAWSON* iliyopo kwenye halmashauri itaanza kuwasiliana na si kuwa *stand alone system* kama ilivyo sasa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hii; ule wa Usimamizi wa Fedha za Umma (*Intergrated Financial Management Systems – IFMS*) au *EPICOR*, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*Human Capital*

*Management Information System*) au *Lawson* na Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Utoaji Huduma (*Local Government Monitoring Database*) ilinunuliwa kwa nyakati tofauti kutegemeana na teknolojia iliyokuwepo wakati huo na kwa madhumuni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na teknolojia zake, ni kweli mifumo hiyo ilikuwa halingiliani au kubadilishana taarifa (*automatic data exchange*). Hali hii imesababisha kuwepo kwa changamoto ya kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na usimamizi. Gharama hizi ni pamoja na mafunzo kwa watumiaji, leseni za mifumo, ununuzi wa mitambo na vifaa pamoja na gharama nyingine za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa mifumo hii inaunganishwa ili kuleta ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji kwa kuwa sasa teknolojia imekuwa na pia uwezo wa Serikali kiutaalam umeongezeka hususan baada ya kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao (*eGA*) na Idara/Vitengo vya TEHAMA katika Ofisi za Serikali kuanzia miaka ya 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa mifumo hii inawasiliana hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(a) Kuandaa miongozo ya viwango (*technical specifications*) kwa kuzingatiwa wakati wa kusanifu, kujenga na kuimarisha au kuhuisha mifumo kwa lengo la kufanya maandalizi ya kuunganisha na kuimarisha.

(b) Kutengeneza mfumo maalum wa ubadilishanaji taarifa kutoka mifumo mbalimbali.

(c) Kuweka miundombinu ya TEHAMA ambapo mtandao mkuu wa mawasiliano Serikalini ambapo taasisi, tumeziorodhesha 72 za Serikali, Wizara 26, Wakala wa Serikali 29, Idara zinazojitemea 17 zilizopo Dar es Salaam, Dodoma

na Pwani. Aidha, Serikali imeunganisha katika mtandao huu taasisi za Serikali zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 77, Sekretarieti za Mikoa 20, Halmashauri za Majiji, Miji, Wilaya 38 na Hospitali za Mikoa 19 kwa lengo la kuwezesha kuunganisha mifumo inayotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kulingana na mpango kazi ullopo kazi iliyobaki ya kuunganisha mifumo mbalimbali ndani ya Serikali, ikiwemo mifumo hii mikuu inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa hatua inayochukua katika kusimika mifumo mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kurahisisha uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pamoja na pongezi hizo, nampongeza vilevile Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, changamoto kubwa katika utumiaji wa mifumo hii ni upatikanaji wa wataalam wa TEHAMA katika Mamlaka za Serikali zetu za Mitaa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri wataalam wa kutosha wa TEHAMA hasa katika halmashauri mpya ambazo zimeanza hivi karibuni kama Nanyamba na Halmashauri ya Mji wa Newala?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba kwenye Mfumo wa *EPICOR* kuna changamoto nyingine ambayo inapatikana hususan wakati wa kutayarisha *final account* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kiasi kwamba wataalam hulazimika kutafuta taarifa nyingine nje ya mfumo. Je, Serikali ina mpango gani wa ku--*repair* changamoto hii ili tunapoandaa hesabu za mwisho kwa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa wataalam wategemee taarifa za kwenye *system* tu na si kuchukua nyingine kutoka nje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, Mwalimu Mstaafu, Mkurugenzi Mstaafu, *RASM* Mstaafu, mdogo wangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuwaajiri wataalam wa TEHAMA, Wizara ya Utumishi na Utawala Bora tutakuwa tayari kuajiri watumishi hao kulingana na mahitaji. Katika zile nafasi 52,000 ambazo zilipitishwa na Bunge ambazo karibuni tutaanza kuajiri, zipo baadhi ya Halmashauri ambazo zimeweka maombi ya kuajiri wataalam hao. Sasa kila Halmashauri inawahitaji hawa kulingana na mahitaji yake yanahitilafiana.

Naomba nishauri, kwa hiyo, kama mdogo wangu Mheshimiwa Chikota, kule Nanyamba uliweka katika maombi, basi itakapofika kuajiri tutaajiri na kama hawakuwekwa tunashauri Nanyamba na Halmashauri nyingine zote katika bajeti inayokuja kutuwekea maombi hayo mkishirikiana na Wizara mama ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali la pili la Mheshimiwa Chikota linahusu mfumo wa *EPICOR* ambao unasimamiwa na Wizara ya Fedha. Kwa sababu Kwa muuliza swali anapaswa kupata majibu sahihi ninaomba nimuombe Waziri mwenzangu wa Fedha ajibu suala la *EPICOR* kwa sababu linasimamiwa na Wizara yake, kwa ruhusa yako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Chikota kwa kweli kwa kujali umuhimu wa mifumo hii kuingiliana na kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo anaisema ambayo sasa wataalam wanajikuta wakitegemea taarifa kutoka nje badala ya ndani ya mifumo kimsingi inatokana na madiliko ya teknolojia ambayo tunaenda nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chikota atakumbuka kwamba tulinza na platnum wakati ule, tukajikuta kwamba mifumo hii na ina hitilafu tukaamia kwenye *EPICOR 7.0*; lakini nayo kulikuwa na *modules* ambazo ni *friendly* kwa mtumiaji, lakini ikawa na changamoto nyingine tukahama tena tukaenda 7.35 tukaenda 9.05 na sasa tumefika *EPICOR 10.20*. Kwa hiyo, kwa kweli changamoto anayoisema ni ya kiteknolojia zaidi. Tunatarajia kwamba huu mfumo wa *EPICOR 10.2* sasa *to zero* itajalibu kushughulikia hizi changamoto ambao zinajitokeza katika utumiaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kumekuwa na utaratibu wa kutengeneza mifumo yetu nyeti nje ya nchi jambo ambalo linaweza kuhatarisha usiri na usalama wa taarifa zetu.

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kutumia wataalam wetu wa ndani ili kuepuka matatizo ambayo yanaweza kujitokeza? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumushi na Utawala Bora majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeunda Wakala wa Serikali Mtandao. Serikali Mtandao iko pale kwa kusimamia mifumo yote inaayoanzishwa ndani ya Serikali na kwamba mifumo yote iliyopo sasa imeanzishwa kwa kuhusishwa Serikali Mtandao. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Kamati ya Bunge inayohusika na masuala ya Utawala na

Serikali za Mitaa imependekeza na mimi nawaunga mkono kwamba Wakala wa Serikali Mtandao ibadilishwe iwe mamlaka ili iweze kusimamia mitandao yote na mifumo yote inayoanzishwa ndani ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Khalifa Mohamedi Issa Mbunge wa Mtambwe sasa aulize swali lake.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba sasa swali langu lipate majibu ya Serikali.

Na. 112

**Sababu za Kataalam Kuthibitisha Kuwa Wanawake Ndio Waathirika Wakubwa wa UKIMWI**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Kwa takwimu zilizopo inakisiwa kuwa watu wote wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania ni zaidi ya milioni moja na laki tano na inaaminika kuwa na wanawake ndio waathirika wakubwa zaidi ikilinganishwa na wanaume.

Je, ni sababu gani za kataalam ambazo zimesababisha Wanawake kuwa ni waathirika zaidi kuliko Wanaume?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa Mbunge wa Mtambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kitaam zinazosababisha wanawake kuathirika zaidi na maambuzi

ya VVU na UKIMWI zipo kama nne na naomba nizitoe kama yafuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kwanza ni ya kimaumbile na kibaiolojia. Mwanamke yuko katika hatari zaidi ya kuambukizwa VVU ukilinganishwa na wananume kwa kuwa maumbile ya mwanamke ni rahisi kupata michubuko wakati wa tendo la ndoa na hivyo kurahisha virusi vya UKIMWI kupenya. Aidha, maumbile ya mwanamke hupokea mbegu za kiume kutoka kwa wanaume wakati wa tendo la ndoa. Iwapo mwanamke atafanya mapenzi na mwanaume mwenye VVU, mwanamke huyo anaweza kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili kwamba kuna tabia na mazingira hatarishi ambayo husababisha hatari zaidi kwa wanawake kuambukiwa VVU, ikiwa ni pamoja na kufanya biashara ya ngono na kuanza mapenzi katika umri mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya tatu ni mfumo dume uliokuwepo katika jamii yetu unaowapa fursa wanaume ya kuamua kufanya ngono na wanawake wengi, kutotumia kondomu, kuoja wasichana wenye umri mdogo na na hata kufanya ukatili wa kijinsia. Mfumo huu unasababisha baadhi ya wanawake kuambukizwa VVU na hata kushindwa kueleza hali zao za maambukizi kwa wenza wao kwa kuhofia kuachika, kutengwa au kufukuzwa kutoka kwenye familia. Kwa kawaida mfumo dume huambatana na wanyanyapaa na ubaguzi ambao pia ni kikwazo kikubwa kwa wanawake kuwa wazi kuhusu hali zao za maambukizi ya VVU na hasa na hasa kutengwa na familia yao au jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sababu ya mwisho ni kwamba wanawake wengi hujitokeza kupima kuliko wananume. Nitoe rai kwa wanaume kujitokeza kupima, tusitumie wenza wetu kama kipimo cha maambukizi yetu sisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa swali la nyongeza.



**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini pia nishukuru kwa majibu ya kitaalam ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo pamoja na majibu hayo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sababu za kimaumbile pamoja na mabo mengine kama alivyotaja katika jawabu lake la msingi Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba bado kuna mila potofu za ukeketaji wa wasichana kwa kutumia zana za kienyeji, zana moja kwa watu wengi. Lakini pia kuna mila potofu ya kurithi wajane, kuna mila ambazo mjane anarithiwa baada ya mume kufa bila ya kupima au kujulikana amekufa kwa sababu zipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, bado Virusi vya UKIMWI au UKIMWI katika nchi yetu ni tatizo na maambuzi kila siku yanazidi kuliko kupungua, na ziko njia nyingi ambazo zinasababisha maambukizi kama vile ngono na Serikali inajua kuna vishawishi vingi na kuna biashara ya ngono hasa katika maeneo ya mjini.

Je, Serikali ina mpango gani hasa hasa maalum ambao watautumia katika kuzuia biashara hizi za madangulo, biashara hizi zinafanyika na hatuwezi kuwalaumu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshauliza maswali yako, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba kumekuwa na mila potofu za ukeketaji na kurithi wajane ambazo kwa njia moja au nyingine nazo zinachangia kwa kiasi katika maambukizi dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI. Serikali tunaendelea kuchukua jitihada za kuelimisha jamii kuhusiana na madhara haya ya masuala ya ukeketaji na ya kurithi wajane. Moja ya shughuli ambayo na mimi nitaifanya baada ya Bunge hili kukamilika ni kwenda katika Wilaya ya Kilindi katika Mkoa wa Tanga

kwenda kushiriki pamoja na jamii wale wakeketaji ambao walikuwa wanafanya shughuli hizi za kuiacha shughuli hiyo na sasa kuanza sasa kuhakikisha kwamba taratibu za kawaida zinaweza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali inaendelea kuchukua juhudi ya kutoa elimu lakini vilevile kuamasisha jamii kuachana na mila potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili lilikuwa ni kuhusiana na suala la biashara ya ngono. Serikali inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwenye jamii kuhusiana na biashara hii ya ngono na kuchukua taratibu za kisheria pale tunapobaini kwamba kuna madangulo katika maeneo husika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea, Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 113

### **Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto**

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

Vifo vya mama katika Mkoa wa Mwanza pamoja na mambo mengine huchangiwa na kukosa huduma za upasuaji, damu salama na upungufu wa watumishi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo vya mama na mtoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vifo vinavyotokana na uzazi bado ni changamoto nchini. Tafiti zilizofanyika mwaka 2015/2016 zinaonesha kwamba kuna idadi ya vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Mkoa wa Mwanza ulikuwa na vifo 305 kwa kila vizazi hai 100,000. Katika kukabiliana na tatizo hili Wizara yangu imeandaa mpango mkakati wa kuboresha huduma ya afya kwa wanawake wajawazito wa mwaka 2016 mpaka 2020 na mpango maalum wa kutekeleza afua muhimu zenye matokeo makubwa ambao umezinduliwa mwezi Novemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo muhimu yaliyomo katika mpango mkakati huu ni pamoja na kuimarisha huduma kwa wanawake wajawazito ikiwemo huduma ya dharura wakati wa ujuzito wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua. Sanjari na hiyo tumeimarisha mifumo ya afya ikiwemo kuwa ajili watumishi wenye ujuzi vifaa tiba pamoja na dawa ili kuhakikisha kwamba huduma inayotolewa ina ubora unaokidhi viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepata ufadhili wa *World Bank* na Canada kwa ajili ya kujenga na kuboresha miundombinu katika vituo vya afya ili kuwezesha kutoa huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kumtoa mama mtoto tumboni. Katika Mkoa wa Mwanza vituo vya Kome (Buchosa), Karume (Ilemela), Kahangara (Magu), Malya (Kwimba), Kagunga (Sengerema) na Bwisya (Ukerewe) vimepata jumla ya bilioni 2.6 kwa ajili ya ukarabati wa au kujenga vyumba vya upasuaji, wodi ya wazazi, chumba cha kijifungulia, maabara ya damu na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kibali cha ajira cha watumishi wa afya takribani 3152 kilichotolewa mwezi Disemba, 2017 Mkoa wa Mwanza umepokea jumla ya watumishi 78. Aidha Wizara imeupatia Mkoa wa Mwanza magari ya wagojwa manane kwa ajili ya huduma za rufaa za wajawazito kwenye vituo vya afya, vilevile tunaendelea kuhamasisha akina mama wajawazito kujifunguliwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma swali la nyongeza.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali; kwa kuwa fedha za *basket fund* pamoja na mambo mengine kutumika pia kupunguza vifo vya mama na mtoto. Hata hivyo fedha hizi zimekuwa zikienda taratibu na pia zina chelewa sana kufika. Kwa mfano *the first quarter* kwenda kuanzia Julai - Septemba zinaenda Desemba tena mwishoni kabisa na baadhi ya vituo kutokupata kwa mfano Kituo cha Ihelele kilichopo Misungwi pamoja na Hospitali ya Bukumbi hazija pata kabisa fedha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kifedha tofauti na mfuko wa *Basket Fund* ambao unatolewa na wafadhili kuhakikisha kwamba vifo vya mama na mtoto vina pungua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunashukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya alifika Mkoa wa Mwanza na akatembelea katika Kituo cha Karume na kuangalia kazi iliyofanyika katika Kituo cha Karume kwa pesa ambazo zimetolewa na Serikali, lakini pia Mheshimiwa Waziri alihaidi kukipatia fedha kituo cha afya kilichopo Buzuruga fedha kwa ajili ya kutengeneza *theater* ambapo kwa sasa kituo kile hakitoi huduma za upasuaji na kituo ambacho kinategemewa sana.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo ili kuendelea kupunguza vifo vya mama na mtoto katika Mkoa wa Mwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Kiteto Koshuma kwa kupigana kiume na kike katika kuimarisha afya ya uzazi na mtoto ikiwemo wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza kwamba fedha za *Basket Fund* zina chelewa nini mkakati wa Serikali katika kutafuta fedha za ndani. Kwanza kuhusu fedha za *Basket Fund* tumefanya mashauriano na wadau ambao wanachangia mfuko wa afya wa pamoja. Moja ya makubaliano ambayo tumeyafanya na Waziri wa Fedha akiwemo ni kwamba fedha hizi sasa watajitahidi kuzitoa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika bajeti yetu ya mwaka 2017/2018 tumetenga rasilimali fedha za ndani kwa ajili ya kuimarisha huduma za uzazi ikiwemo kuhakikisha uzazi salama. Kwa mfano katika huduma za uzazi wa mpango kwa mara ya kwanza tumetenga bilioni 14 na zimetoka, fedha za ndani kwa ajili ya huduma za uzazi. Lakini tumetenga fedha pia kwa ajili ya kujenga maabara za damu katika mikoa mitano na tumetenga fedha pia kwa ajilia ya kujenga vyumba vya upasuaji katika vituo vya afya. Kwa hiyo sambamba na fedha za *Basket Fund* lakini pia tunazo hela za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu Kituo cha Afya cha Buzuruga, ni kweli tumepata fedha za *Basket Fund* bilioni 15.5 na tunategemea pia kupata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya ili kuviwezesha kutoa huduma za uzazi za dharura.

Nitumie fursa hii kuelekeza tena fedha hizi sio za kujenga mabwalo ya kulia chakula, si fedha za kujenga ukuta sifedha za kujenga mambo ambayo hayahusiani moja kwa moja na huduma za afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua vituo vya afya vina changamoto nyingi lakini hebu tujikite katika kumuokoa mama mjamzito na mtoto mchanga baadae tutakuja kujenga wodi za kufunga vidonda lakini kwetu sasa hivi hicho sio kipaumbele, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal Haonga, swali la nyongeza.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ambayo pia inatumika kama Hospitali ya Mkoa wa Songwe akina mama ambao hujifungua pale ni wastani wa akina mama 18 hadi 20 kwa siku, lakini kwa bahati mbaya sana hospitali ile haina wodi ya wazazi.

Je, ni lini Serikali itajenga wodi ya wazazi katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi ambayo hutumia kama Hospitali ya Mkoa kwa sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la ndugu yangu, *comrade* wangu hapa kuhusu swali la Hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna changamoto kubwa ya wodi ya wazazi na jukumu la Serikali yetu ni kuhakikisha kwamba hizi Hospitali za Wilaya zote tunahakikisha tunaziimarisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunachukua hoja hiyo halafu kwenda kufanya *analysis* kupitia wataalam wetu kwenda pale kuangalia mapungufu yaliyokuwepo ili tuboreshe hospitali ile na hatimaye wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma nzuri. Kwa hiyo, nalichukua hili kwa ajili ya kuhakikisha tunalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Aida Khenan.

Na. 114

**Polisi Kuwapiga, Kuwatesa Watuhumiwa**

**MHE. AIDA J. KHENAN (k.n.y MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA)** aliuliza

(a) Je, kuna sheria yoyote ya nchi inayomruhusu askari polisi kumkatamata mtuhumiwa, kumpiga na kumtesa kabla hajajua kosa lake na kabla ya kufikishwa katika Kituo cha Polisi?

(b) Je, Serikali inachukua hatua zipi za kuhakikisha kuwa askari wanaofanya vitendo kama hivyo wanawajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi?

(c) Je, mpaka sasa ni askari wangapi wameshachukuliwa hatua za kisheria kutokana na makosa ya kujichukulia hatua mkononi?

**NAIABU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum lenye shemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 kifungu cha 11 kinaeleza namna ya ukamataji. Aidha, kifungu hiki mahsusi cha ukamataji hakimruhusu askari kumpiga na kumtesa raia wakati wowote anapokuwa kizuizini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utendaji wa Jeshi la Polisi (*PGO*) askari yoyote anapobainika kufanya vitendo vya kupiga au kutesa raia huchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa kazi na au hata kufikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Januari mpaka Desemba, 2017 jumla ya askari 105 waliotenda makosa mbalimbali walichukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu, anasema ni askari 105 ambao wamechukuliwa hatua za kinidhamu. Katika matukio ambayo yametokea ambayo hayana shaka, ni matukio ya wazi, ni matukio ambayo yametokea kwa Mheshimiwa Nape Nnauye ya kutolea bastola hadharani lakini pia Mdude Nyangali ambaye amepigwa mpaka sasa hawezi kutembea vizuri, Husna Amri ni kiongozi wetu wa CHADEMA ambaye amefanyiwa hicho kitendo mpaka sasa hivi tuko hospitali. Je, katika hao askari ambao wamechukuliwa hatua za kinidhamu ni miongoni mwa hao 105?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna askari ambao umekiri kwamba wamechukuliwa hatua za kinidhamu na hawa watu wanaoteswa wengine hawawezi tena kuendelea na shughuli zozote, wanapata fidia gani kulingana na madhara ambayo wamekuwa wameyapata? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake ameuliza kwa kutoa mifano michache ya baadhi ya watu ambao walipata majeraha mbalimbali, lakini naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi kidogo wa majibu ya swali hili, nadhani itasaidia kuweza kutoa uelewa mpana wa utaratibu wa jinsi ambavyo



polisi wanafanya shughuli zao wanapokabiliana na changamoto ya uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimezungumza katika jibu langu la msingi kwamba ukamataji nchini unasimamiwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu namba 11 ambacho kinaeleza kwamba polisi anapaswa atumie njia ya kumshika muhusika (*physical contact*) pale tu ikiwa yule mtuhumiwa amegoma. Katika hali ya kawaida ni kwamba polisi wanapohitaji kumkamata mtuhumiwa inamueleza na watuhumiwa ambao wanafuata sheria bila shuruti huwa polisi hawana haja ya kuwashika au kuwakamata kwa kutumia mikono yao. Hii inadhihirishwa na hata Waheshimiwa Wabunge huwa ni mashahidi mara nyingi, wakiwemo viongozi ambao wamekuwa wakituhumiwa kwa mambo mbalimbali wanapelekewa taarifa kwa njia ya simu au hata kwa barua waweze kujisalimisha wenyewe polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya pili ni ambayo sheria hii inaainisha ni kwamba endapo mtu huyo atakuwa amebisha, basi polisi wataweza kutumia njia yoyote ambayo ni stahiki kuweza kumkamata mtuhumiwa, kwa kiingereza wanasema; *“may use all means necessary to effect the arrest.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi ndivyo ilivyoandikwa katika Sheria yenyewe ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Hata hivyo, hata hii nayo imefafanuliwa katika PGO namba 274 ambayo inaeleza utaratibu wenyewe hata wa kukamata ukoje na unazingatia mambo mengi. Kwa mfano, unaweza ukaangalia aina ya tishio kwamba je, madhumuni ya mtu huyu ni yapi na mazingira ambayo yanahusisha mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine mengi ambayo yanaangaliwa miongoni mwayo wanaangalia vilevile, kwa mfano; wanaangalia *resistance* ilivyo. Wakati mwingine inawezekana mtu akawa amesimama tu au ameshikilia kitu au wakati mwingine ameshikilia silaha, kwa hiyo vile vile maamuzi ya kumkamata

yanategemea aina ya mtuhumiwa mwenyewe mazingira yake aliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia inategemea aina ya silaha ambazo polisi anazo, inategemea vilevile utafiti ambao polisi wanafanya kabla, mbinu gani watumie. Wanaweza wakahitaji kupata taarifa za kiintelijensia kabla ya kumkamata muhusika. Niliona nitoe ufafanuzi huo ili nieleweke vizuri. Hata matumizi ya nguvu kwa wale ambao ni majambazi au wanaotumia silaha nao kuna utaratibu wake kwa mujibu wa *PGO* namba 7 na 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kujibu *specifically* suala la watu ambao wanawataja itategemea na mambo yote ambayo nimeeleza, kwamba je, mazingira ambayo mtuhumiwa alikuwepo yalikuwa ni yapi? Sasa kusema sasa hivi kwamba mtu fulani alikuwa amechukuliwa hatua gani kwa maelezo ya hapo moja kwa moja, nadhani cha msingi ni kwamba tunashughulika na kesi kwa kesi kulingana na aina ya mtuhumiwa jinsi ambavyo ametenda lile kosa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa Mbunge wa Lupa sasa aulize swali lake.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuleta salamu za shukurani kwako wewe binafsi kwa wananchi wa Chunya Mjini pale ambapo shule ya msingi Chunya Mjini iliezuliwa na madarasa matatu, ofisi za walimu, vijana wako wa *Tulia Trust* walifika pale wakaleta mabati 100 ya *gauge 28* na kwa misaada hiyo madarasa yamejengwa na sasa hivi wananfunzi wako darasani, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba swali langu namba 115 lipate majibu.

Na. 115

## **Ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Kisasa-Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Wananchi wa Wilaya ya Chunya wameanza kujenga uwanja wa michezo wa kisasa wa Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi huu ili ukamilike haraka?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mbunge wa Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Maendeleo ya Michezo ya mwaka 1995 kifungu cha 5.1.8(b) (vi) inaelekeza wajibu wa mamlaka ya Serikali za Mitaa kushirikiana na wananchi katika kujenga, kulinda na kutunza miundombinu ya michezo ikiwemo viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa uwanja wa michezo wa Chunya unatekelezwa kwa kuzingatia sera ya michezo ikisimamiwa na Serikali kupitia Halmashauri ya Chunya kwa ushirikiano wa karibu na wananchi pamoja na wadau. Mradi huo unaotarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni nane umetumia kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 100 zilizotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya katika mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Seriakli kupitia Halmashauri ya Chunya imetenga kiasi cha shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuendelea na hatua mbalimbali za mradi wa ujenzi wa uwanja huo wa michezo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Victor Mwambalaswa swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina mswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, katika uwanja huo mimi kama Mbunge nilitoa hela yangu mwenyewe shilingi milioni kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimuona mtu anatoa hela yake mfukoni kupeleka kwenye *project* ya wananchi kwa zama hizi ujue kilio hicho ni kikubwa sana. Chunya ni Wilaya ambayo ni kongwe sana, sasa hivi ina miaka 76. Viongozi wengi wa nchi hii akiwemo Profesa Mark Mwandosya amesoma Chunya na viongozi wa kidunia akiwemo aliyekuwa Rais wa makaburu wa mwisho Pieter Botha alizaliwa Chunya na kusoma Chunya. Kwa hiyo, Chunya ni Wilaya ambayo inatakiwa iangaliwe kwa huruma sana. Serikali inasemaje kuhusu kututafutia Chunya wafanyabiashara wakubwa wanaoweza kutusaidia kujenga uwanja huo ili waweze kutangaza biashara zao? La kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje kuhusu kuja Chunya aje auone uwanja huo ili awe na uelewa mkubwa na mpana kuhusu uwanja huo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa mzee wangu Mheshimiwa Mwambalaswa kwa jitihada zake kubwa ambazo amekuwa akizifanya katika kuboresha miundombinu ya michezo katika jimbo lake. Niseme wazi kabisa kwamba Wizara yangu pia inayo taarifa kwamba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na wananchi wa

Wilaya ya Chunya na Jimbo la Lupa wamechangia kiasi cha shilingi milioni 224, ambazo kati ya hizo milioni kumi ametoa Mbunge wa Jimbo la Lupa Mheshimiwa Mwambalasma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pia nichukue nafasi hii kuweza kuomba Wabunge wote kuiga mfano huu mzuri ambao Mheshimiwa Mbunge ameuonesha, lakini vilevile kuiga Halmashauri zote nchini zichukue mfano huu mzuri ambao umeonyeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya katika kuwashirikisha wadau katika kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu ya michezo.

Kuhusu swali lake la kwanza ambalo ameuliza kuomba wadau, kwamba Wizara imsaidie kuweza kutafuta wadau. Mimi niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge Wizara yangu iko tayari kabisa kushirikiana pamoja na wewe, lakini vilevile na Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na Jimbo la Lupa kuhakikisha kwamba tunahamasisha wadau mbalimbali waweze kujitokeza katika kuchangia ujenzi huo wa uwanja wa michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi lake la pili, niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge mimi nikutoe wasiwasi, na ni mwezi wa 12 tu nilikuwa katika Wilaya ya Mbeya Vijijini. Kwa hiyo, niseme kwamba tutakapotoka hapa naomba tukutane tukae, tujadili, tuongelee ratiba kwamba ni lini ili na mimi niweze kuja kujione uwanja huo wa Lupa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wengine mmesimama na si wanamichezo sasa sijaelewa mnataka kuuliza nini! Mheshimiwa Maryam Msabaha swali la nyongeza. *(Kicheko)*

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vijana wetu wanaanza vipaji wakiwa mashuleni, je, Serikali ina mpango gani kuipa sekta ya

michezo hasa mashuleni ili angalau vijana hao tuwakuze katika vipaji vya michezo ili tuweze kufikia kama nchi ya Brazil?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, numshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri ambalo ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Wizara kupitia Serikali tuna mpango mzuri sana wa kuhakikisha kwamba vijana wetu waliopo shuleni wanashiriki katika michezo. Sasa hivi ninavyoongea tayari Wizara kwa kushirikiana na Serikali tumesharejesha ile michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA katika mashule yetu. Haya ni mashindano ambayo kwa kiasi kikubwa sana yanasaidia kuibua vipaji vya vijana. Tumeshuhudia kwamba michezo hiyo inakwenda vizuri na wanafunzi wengi wamekuwa wakishiriki na vipaji vingi vya vijana vimeendelea kujitokeza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikutoe hofu kwamba Wizara tuna mikakati mizuri na tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba tunaendelea kuinua vipaji vya vijana wetu ambao wapo mashuleni, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri wa Michezo atakapokuwa anakwenda Chunya akumbuke hata zile milioni 250 ambazo Mheshimiwa Mwambalasma amesema na sisi wananchi wa Songwe tulichangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikua namuomba tu apite pale Wilaya Mpya ya Songwe, pale Mkwajuni na mimi najenga uwanja pale ili na mimi aje anaagalie na kunisaidia juhudi ambazo nazifanya pale Mkwajuni, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani ombi umelikubali. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Naibu Waziri atapita Songwe, kwa hiyo Mheshimiwa Mulugo usitie shaka.

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 116

### **Mpango wa Kuwawezesha Wanawake Kujua Haki Zao**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Wanawake wengi bado hawaelewi haki zao hasa kuhusu haki za kumiliki ardhi.

Je, kuna mkakati gani wa Serikali wa kuwawezesha wanawake waweze kujua haki zao za kumiliki ardhi?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi imekuwa ikitoa elimu kwa umma kuhusu haki ya wanawake kumiliki ardhi. Elimu hiyo imekuwa ikitolea kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipindi vya redio na luninga, mikutano ya hadhara, warsha, semina, maonesho mbalimbali kama vile Siku ya Sheria, Wiki ya Utumishi wa Umma, Siku ya Mtoto wa Afrika, Maadhimisho Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, Wiki ya Msadaa wa Kisheria pamoja na maonyesho mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa ikichapisha machapisho yenye kuelimisha umma kuhusu masuala ya

umiliki wa ardhi. Aidha, Tume hiyo imetoa elimu katika Kata 72 katika Wilaya 18 za Tanzania Bara na Shehia nane za Wilaya nne za Tanzania Zanzibar. Wilaya za Tanzania Bara ni Biharamulo, Ngara, Mpanda, Babati, Simanjiro, Mbarali, Mbeya, Mvomero, Ulanga, Ludewa, Makete, Nkasi, Namtumbo, Tunduru, Kahama, Kishapu, Kilindi na Tanga; na Wilaya za Tanzania Zanzibar ni Unguja Kusini, Unguja Kaskazini-A, Mkoani na Michweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuendelea kuelimisha umma katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar hasa kwa wanawake ili wananchi wote waweze kufurahia haki zao za msingi ikiwemo haki ya kumiliki ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, licha ya elimu kutolewa lakini bado kuna matatizo kuhusu haki ya ardhi. Sasa Serikali inaonaje kutoa kipindi maalum, narudia, kipindi maalum kwa muda muafaka kwenye luninga au kwenye redio kusudi elimu hii iwafikie hasa wanawake kwa wakati muafaka na kwa muda muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa sehemu kubwa ya ardhi inatumiwa sana na wanawake; kama asilimia 70 wanawake wanatumia hii ardhi hasa kwa uzalishaji mali hasa kwa kilimo. Hata hivyo wanawake hawa hawana maamuzi kuhusu ardhi hii. Je, Serikali inatoa kauli gani hasa ya kueneza elimu hii na kutokana na kwamba kwenye makabila mengine bado kuna mfumo dume ambao hauwapi ridhaa wanawake kumiliki ardhi? ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.



**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Dkt. Christine Gabriel Ishengoma kwa sababu alifanya utafiti mmoja ambao ulikuwa ni utafiti mzuri sana kuhusu mfumo wa kumiliki ardhi kwa watu wanaotoka katika makabila ambayo ni *matrilineal* au *matriarchal*. Yaani wale *ursine local matriarchal* wa makabila ya Pwani kama Wazaramo, Wakwere, Wakutu, Waluguru, Wanguu, Wakaguru lakini pia wale *matrilineal* ambao ni Wamwera, Wayao, Wamakua, Wamakonde na kuonesha ni jinsi gani katika maeneo hayo mfumo ule ambao sasa sijui ni mfumo jike, lakini umiliki wa ardhi unatoa maeneo ambayo yangesaidia watu wa mfumo dume kujifunza; na labda ndiyo maana katika historia ya Bunge letu wanawake wengi mwanzoni walioshinda Ubunge wa Majimbo walitoka maeneo hayo ya Wamwera, Wayao, Wamakua na Wamakonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakubaliana naye kwamba kuna umuhimu wa kuwa na kipindi maalum cha mambo ya ardhi katika luninga na redio kwa wakati muafaka ili wanawake wengi wakisikie. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kumuahidi kwamba nitaongea na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili kuandaa vipindi hivi kwa wakati muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake la pili, niseme tu kwamba tuendeleo kuelimishana kuhusu umuhimu wa wanawake kumiliki ardhi hasa katika maeneo ya mfumo dume. Vilevile pia niwaombe Mahakimu na Majaji wengi waelewe umuhimu na utofauti wa umiliki wa ardhi katika maeneo ya Tanzania ya Pwani na Kusini yenye mfumo jike katika kumiliki ardhi kwa sababu hukumu zao zimekuwa hazielewi kwanini katika maeneo hayo wanawake wana sauti ya maamuzi. Na kwa maana hiyo basi tuendeleo kuimarisha jambo hili ili mwisho wa siku jinsia zote mbili ziwe na haki sawa katika umiliki wa ardhi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake.

Na. 117

**Kuongeza Usambazaji Maji Katika Vijiji 100**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Mwaka 2014/2015 Serikali iliahidi kuongeza usambazaji maji katika vijiji 100 vilivyoko umbali wa kilometa 12 kutoka bomba kuu la Ziwa Victoria hadi Kahama na Shinyanga na Serikali ilishatenga shilingi bilioni nne ili kutekeleza mradi huo.

(a) Je, vijiji vingapi vimeshapatiwa maji kati ya hivyo 100 hadi sasa?

(b) Je, Serikali itafikisha lini maji ya Ziwa Victoria katika Vijiji vya Mwakazuka, Mwaningi, Kabondo, Ntundu, Busangi, Buchambaga, Nyamigege, Gula, Izuga, Buluma, Matinje na Bubungu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatekeleza mradi wa maji wa vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga. Utekelezaji wa mradi huo unafanywa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika awamu ya kwanza jumla ya vijiji 40 vilivyopo katika Halmshauri za Msalala, Misungwi, Kwimba na Shinyanga vimetambuliwa na ujenzi wa miradi ya maji ambapo katika vijiji 33 umekamilika na baadhi ya vijiji vingine vinaendelea na ujenzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyotajwa juu ni miongoni mwa vijiji 100 vilivyotambuliwa. Tayari halmashauri ya Msalala imekamilisha usanifu wa kina kwenye vijiji vya Ntundu, Busangi, Nyamigege, Gula, Ntobo, Masabi na Chela.

Aidha, vijiji vya Mwakazuka, Kabondo na Izuga zabuni zake zimeshatangazwa na *KASHWASA* na tayari mkandarasi amepatikana. Vijiji vya Mwaningi, Buchambaga, Buluma, Matinje na Bubungu vipo katika hatua za awali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika vijiji vinavyoendelea na vilivyobaki kulingana na bajeti ilivyotengwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige swali la nyongeza.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi naomba nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na naomba tu niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, vijiji hivi 100 kimsingi ni ahadi iliyotolewa na Serikali mwaka 2014 hapa Bungeni na ilitegemewa kufika mwaka 2015 vingekuwa vimepata huduma ya maji, lakini mpaka sasa hivi kama ambavyo jibu limeeleza kwamba fedha hazijapatikana.

Nilitaka nipate tu uhakikisho wa Mheshimiwa Waziri, kwamba kwa mwaka huu wa fedha tunaouanza 2018/2019 je, Serikali inaweza ikamaliza hii ahadi ya muda mrefu ili vijiji hivyo vipate maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi sasa Serikali inatekeleza miradi miwili mikubwa ya maji. Mmoja ni wa maji kutoka Kahama kwenda Isaka na mradi mwingine ni wa kutoka Mangu kwenda Ilogi. Miradi hii yote inatekelezwa kwa awamu ya kwanza kwa maana ya kupeleka bomba kuu peke yake bila usambazaji kwenye vijiji vilivyo jirani. Ahadi imekuwa kwamba awamu ya pili ambayo itaanza 2018/2019 itahusisisha usambazaji wa maji kwenye vijiji vilivyo jirani.

Je, Waziri anaweza akanihakikishia kwamba utekelezaji wa hii awamu ya pili ambayo itahusisisha

usambazaji wa maji kwenye vijiji vilivyo jirani katika miradi hiyomiwili utatekelezwa pia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji na umwagiliaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba awali ya kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anazofanya katika jimbo lake na kuwatetea wananchi wake wa Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kabisa ahadi ni deni na hii ni ahadi ya Serikali. Nataka nimuhakikishie kwamba katika vile vijiji 100 sisi kama Wizara ya maji tulikuwa tukitoa fedha na tutaendelea kutoa katika kuhakikisha vijiji vinapatiwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu katika vijiji ambavyo vipo katika awamu ya pili, tunatambua siku zote safari yoyote ni hatua. Tumeshanza hatua ya kwanza katika kuhakikisha kwamba tunaliweka bomba kuu, na tutahakikisha kwamba baada ya kukamilika utandazaji wa bomba hili kuu vijiji vilivyokuwa jirani ya kilometa 12 vyote vitapatiwa maji; ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji kabla sijataja wa kuuliza swali waangalie Wabunge waliosimama hapo, kila mmoja ana hoja. Mheshimiwa Abdallah Mtolea swali la nyongeza.

**MHE ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji liliko Msalala linafanana na tatizo la mji liliko katika Halmashauri ya Temeke ambayo kwa kiasi haina mfumo wa maji ya bomba. Hata hivyo bomba kubwa la maji kutoka Mto Ruvu linalopeleka maji katika Kambi ya Jeshi ya Navy linapita Temeke.

Sasa ni lini Serikali itatoa matoleo kutoka kwenye bomba lile ili wananchi wa Kata za Mtoni, Azimio, Tandika, Makangarawe pamoja na Buza nao waweze kupata maji kutoka kwenye bomba hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji na umwagiliaji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jukumu la kuwapatia wananchi maji ni jukumu letu sisi Wizara ya Maji na kwa kuwa sisi ni Wizara ya Maji na si Wizara ya ukame tupo tayari kuhakikisha wananchi wake wanapata maji. Mheshimiwa Mbunge nataka nikuhakikishie Jumatatu mimi naanza ziara katika mkoa wa Dar es Salaam, na katika maeneo nitakayotembelea nitafika Temeke tuangalie namna bora ya kuweza kuwapatia wananchi wako maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani swali la nyongeza.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Waziri wa maji kwanza niwapongeze kwa kazi nzuri mradi wa maji wa Mombo - Mlembule ulikuwa wa Serikali imetenga shilingi milioni 900 lakini cha kushangaza sasa hivi mradi huo umekuwa wa shilingi bilioni nne. Nini tamko la Serikali kuhusiana na mradi wa shilingi milioni 900 mpaka ukafika shilingi bilioni nne? Hizo shilingi bilioni nne ni kwa ajili ya mradi gani mwingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulikuwa na mradi wa shilingi milioni

900, lakini usanifu wake haukuhusisha vijiji vya Mji wa Mombo pamoja na maeneo yanakotoka maji Vuga. Kwa hiyo tukafanya *review*, hiyo *review* sasa imekamilika lakini sina taarifa kwamba hiyo *review* imefikia shilingi bilioni nne.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba baada ya Bunge hili leo mimi na wewe twende pamoja, nitakusanya wataalam wangu ili tuweze kuangalia mradi huo uweze kutekelezwa haraka. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela sasa aulize swali lake.

Na. 118

### **Madini Tanaokotwa Jimboni Kwela**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Katika ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa katika Jimbo la Kwela, kwenye ukingo wa Milima ya Lyamba lyamfipa inayoambaa katika Kata za Mfinga, Mwadui, Kalumbaleza, Nankanga, Kapeta hadi Kaoze, baadhi ya wananchi wamekuwa wakiokota madini mbalimbali bila kutambua ni madini ya aina gani.

(a) Je, Serikali imeshafanya utafiti wowote katika maeneo hayo?

(b) Kama jibu ni hapana, je, ni lini utafiti utafanyika ili kujua eneo hilo lina madini gani?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTTO M. BITEKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia miaka ya 1950 Serikali imekuwa ikifanya utafiti mbalimbali wa awali wa madini kwenye maeneo ya Ukanda wa Bonde wa Ziwa Rukwa yakiwemo maeneo ya Jimbo la Kwela kwenye mwambao wa milima ya Lyamba Iyamfipa. Utafiti wa awali ulibaini uwepo wa madini mbalimbali yakiwemo madini ya vito kama vile *Garnet, Kyanite, Zircon* na *Sapphire* na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za uwepo wa madini katika Ukanda wa Bonde wa Ziwa Rukwa zinapatikana kwenye ofisi zetu za Wakala wa Jiolojia Tanzania. Hata hivyo nachukua nafasi hii kuwashauri sana ndugu zetu wote wakiwemo wa Jimbo la Kwela kutumia Ofisi zetu za Madini za Kanda ya Magharibi iliyoko Mpanda na taarifa zilizopo kwenye ofisi ya Wakala wa Jiolojia iliyoko Dodoma, ambapo wako wataalam watawasaidia kuyachambua madini hayo pamoja na kuwashauri namna ya kufaidika na rasilimali hiyo ya madini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kushika nafasi hiyo mpya na kwa kweli ameanza kuifanya vizuri Mwenyezi Mungu aendelee kumuongoza aendelee kuifanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza sisi sote tunafahamu wazi kwamba maeneo yaliyo na madini yanatoa fursa kwa vijana wengi kujiajiri kwa machimbo madogo madogo kwa kujipatia kipato na vilevile Serikali kukusanya kodi. Tunafahamu kwamba Serikali ilishafanya utafiti katika maeneo mengi, lakini utafiti huo uko ndani ya vitabu mpaka uende maktaba jambo ambalo sio rahisi wananchi wa kawaida vijijini kutambua wapi kuna madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa nini Serikali isiainishe maeneo yote yenye madini kwa uwazi ili wananchi waweze kuyatambua na kufanya kazi ya uchimbaji mdogo mdogo?

La pili umesema kwamba wananchi wanaweza kutumia ofisi za kanda za Magharibi zilizopo Mpanda na Dodoma, jambo ambalo ni vigumu kwa wananchi wa kawaida hasa wa vijijini kuzitumia ofisi hizo kutokana na umbali uliopo. Kwa nini Serikali isiweke *branch* katika mikoa yote ili kurahisisha wananchi kuzishilikia ofisi hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTTO M. BITEKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ijulikane tu kwamba matumizi ya ofisi zetu za Wakala wa Jiolojia ni matumizi ambayo yanawahusu Watanzania wote. Ni bahati mbaya tu kwamba wageni wanaotoka nje kuja kutafuta madini hapa nchini wao wanazitumia zaidi ofisi hizi kuliko sisi Watanzania.

Naomba nitoe wito sasa kwa Watanzania wote tuzitumie Ofisi zetu hizi za Wakala wa Jiolojia ili ziweze kutusaidia katika sekta hii ya madini.

Lakini la pili kwa nini Serikali sasa isiweke *branch* kwa kila Wilaya na kila maeneo. Naomba nimuombe Mheshimiwa Malocha, na kwasababu amekuwa mdau mkubwa sana wa kufuatilia jambo hili kwaajili ya wananchi wake; sisi ni watumishi wa wananchi, sisi hatukai ofisisni Mheshimiwa Malocha ukiwahitaji wataalamu wetu wa Jiolojia kuja kwenye eneo lako wakati wowote watakuja, na hata kama utamuhitaji Waziri mwenyewe atakuja kwasababu sisi ni watumishi wa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.



Na. 119

### **Elimu ya Matumizi ya Nyavu kwa Wavuvi**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Kwenye bahari na maziwa yetu kuna samaki wa aina mbalimbali kama vile dagaa, furu, uduvi au dagaa mchele na wengine ambao ni wadogo sana.

(a) Je, ni nyavu zenye ukubwa wa *size* gani zinahitajika kwa ajili ya uvuvi wa aina hizo ndogo ndogo za samaki?

(b) Je, Serikali inafanya utaratibu gani wa kuwapatia wavuvi wa nyavu ndogo ndogo za samaki nyavu zinazohitajika kwa uvuvi huo?

(c) Je, elimu ya kutosha kwa nyavu husika imefanyika kwa kiwango gani hasa kwa wavuvi wanozunguka Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kila samaki hunaswa kwa kutumia wavu wa aina yake bila kuathiri samaki wengine. Kwa mfano kulingana na kanuni za uvuvi nyavu za kuvulia dagaa baharini zinapaswa kuwa na macho au matundu yenye ukubwa wa milimita 10 na kwa upande wa dagaa wanaovuliwa ziwani ukubwa wa macho au matundu ya milimita nane. Aidha, dagaa huvuliwa nyakati za usiku kwa kutumia mwanga wa taa za karabai.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuwawezesha wavuvi kupata dhana za uvuvi kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na

kuwaondelea kodi katika dhana na malighafi za uvuvi zikiwemo nyuzi za kushonea nyavu vifungashio na injini za kupachika. Aidha, Serikali inaendelea kuwahimiza wavuvi kujiunga katika vikundi na kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi, vyama vya akiba na mikopo (*SACCOS*) na *VICOBA* ili waweze kukopesheka na kuweza kununua dhana na vyombo bora vya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia programu ya utoajiwa ruzuku kwa wavuvi Serikali katika awamu ya kwanza ilinunua *engine* 73 ambapo hadi sasa *engine* 49 zimelipiwa na kuchukuliwa vikiwemo vikundi 13 kutoka ukanda wa Ziwa Victoria. Vile vile Serikali imeweka mazingira ya kupata mikopo kwa ajili ya kununua dhana bora za uvuvi kwa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwatumia Maafisa wa Idara ya Uvuvi na *BMUs* imekuwa ikitoa elimu ya kutosha kuhusiana na matumizi endelevu ya nyavu za uvuvi kwa wavuvi wanaozunguka Ziwa Victoria na katika maeneo mengine nchini. Aidha, viongozi wa mikoa na Wilaya wamekuwa wakiongelea suala hili katika hotuba zao wanapofanya ziara za kuwatembelea wavuvi katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Biti Sokombi swali la nyiongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuleta majibu ambayo hayaridhishi.

Kwanza ni uongo, kokolo la milimita 10 linavua dagaa na wale sangara wadogo ina maana kwamba unapowavua unaenda kuwatupa? Naomba muwe mnakaa mnaleta majibu ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakwenda kwenye maswali yangu ya kimsingi. Ziwa Victoria kuna samaki ambao *nature* yao ni wadogo, kwa mfano furu, gogogo pamoja

nembe. Wizara inatenganisha vipi uvuvi huu wa samaki wa aina ya gogogo na sangara? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ziwa Victoria linatumika na nchi tatu ambayo ni Kenya, Uganda na Tanzania yenyewe; na ndani ya ziwa hakuna ukuta ambao utatenganisha samaki kutoka Tanzania kwenda Uganda au kwenda Kenya, je, Serikali inafahamu kwamba wavuvi wa Tanzania wanapata shida kulinganisha kuliko wavuvi wa Kenya na Uganda? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa mifugo na uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza nataka nimthibitishie kwamba nyavu za kuvua dagaa za milimita nane zipo kwa mujibu wa Sheria Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 kanuni namba 58 (1) (a)ukienda kusoma utakuta pale *size* ya milimita nane kwa ajili ya dagaa wa maji baridi na milimita 10 *section* hiyo hiyo 58 (1)(b) utakwenda kukuta kwa ajili ya milimita 10 zile za baharini, kwa hivyo si uongo ni mambo ya ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa upande wa sangara wadogo anaowazungumzia, ni kweli nyavu hizi za milimita nane zitakapokwenda katika ziwa hazitachagua, tunafahamu hilo jambo. Kwa vyovyote vile sangara wadogowadogo ama sato watavuliwa na hiyo kwa kitaalamu tunaita *bycatch* kwa maana ya kwamba wale ambao hatukuwatarajia kanuni zetu na sheria zetu ziko wazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mvuvi wa dagaa kama atakwenda kuvua kilo 100 atayoipata kwa ajili ya dagaa kwa vyovyote vile anaweza pia kwenda kupata kiasi cha kuanzia kilo moja hadi kilo 10 ya samaki ambao hawakutarajiwa na hivyo tunafahamu jambo la namna hiyo wala sio jambo geni kwamba samaki anaweza akaenda akanaswa katika mtego ambao si wa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la lake la pili sasa Mheshimiwa Sokombi ni kuhusuiana na jambo la kuwatesa wavuvi wetu wa Tanzania na wavuvi wa nchi jirani, kwa maana Ziwa Victoria hili ni mali ya nchi tatu sisi Waganda na Wakenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba tayari nchi ambazo tuna-*share* nao Ziwa Victoria wametuletea maombi, na mijadala inaendelea ya kuweza kushirikiana katika ulinzi shirikishi wa Ziwa letu Victoria na *module* ambayo wao inawavutia sana ni *module* hii ambayo sisi Watanzania tunaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli samaki kama sangara ni samaki wanaosafiri umbali mrefu, lakini nataka nikuhakikishie bado fursa kubwa ya uvuvi katika Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania ambao ndio tunamiliki sehemu kubwa ipo kubwa na wavuvi wamekuwa wakinufaika na sisi wenyewe kama nchi tumekuwa tukinufaika.

Naomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla wake wajue kwamba Ziwa Victoria hili ni mali yetu, ni mgodi wetu, tuulinde kwa ajili ya kizazi chetu cha leo na kizazi kijacho. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 120

### **Hitaji la Umeme Katika Baadhi ya Kata – Morogoro Kusini Mashariki**

**MHE. OMARY T. MGUMBA** aliuliza:-

Kata sita za Tegetelo, Kibuko, Tomondo, Tununguo, Seregete, Matuli na Mkulazi katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki hazijafikiwa na miundombinu ya umeme mpaka sasa.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika kata hizo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kufikisha umeme katika vijiji vyote visivyo na umeme nchini ikiwemo vijiji vya Wilaya ya Morogoro ifikapo mwezi Juni, 2019. Kupitia mzunguko wa kwanza wa awamu ya tatu ya miradi ya kusambaza umeme vijijini katika Wilaya ya Morogoro vijiji 14 vitapatiwa umeme ifikapo mwezi Aprili, 2019. Vijiji hivyo ni pamoja na Tununguo, Kibwege, Lung'ala, Kidugalo, Kinonko, Vihengele, Konde, Vigolegole, Singisa, Rudewa, Bonye, Mtego wa Simba, Muungano na Mangala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za kupeleka umeme katika vijiji hivyo, zinajumuisha ujenzi wa kilometa 16.5 za njia za umeme msongo wa kilovolti 33 na kilometa 16 za njia za umeme msongo kilovolti 0.4, kufunga *transformer* nane na kuunganisha wateja 258. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.3. Kazi hii itatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya *State Grid Electrical and Technical Works*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vitakavyobaki katika mzunguko wa kwanza wa *REA* Awamu ya Tatu vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa *REA* Awamu ya Tatu ambapo mradi unategemewa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba swali la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki tulipata vijiji 17 kati ya vijiji 64 katika miradi ya umeme ya REA Awamu ya Kwanza na REA Awamu ya Pili, na kwa kuwa katika awamu zote hizo utekelezaji wake wa miradi hiyo kuna taasisi za umma kama vile shule, zahanati, vituo vya afya na nyumba za ibada na vijiji na vitongoji vingi kwa mfano, Kijiji cha Tomondwe, Mfumbwe, vitongoji vya Misala vilirukwa.

Je, Serikali huu mradi wa *densification* utafika lini Morogoro hususan katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki ili vijiji na vitongoji hivi vilivyorukwa vipatiwe umeme? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na majibu hayo nataka niweke kumbukumbu sawa. Swali kama hili nililuliza katika Bunge lililopita katika swali la nyongeza na swali la msingi Bunge lingine lililopita. Serikali ilinipa majibu katika jimbo langu wamenipa vijiji 20 na si 14; mpaka sasa hivi huyo mkandarasi ameshafika na amefanya *survey* ya vijiji vyote 20. Hata hivyo kwa kuwa amefanya vijiji saba amepata mkataba wa kufanya *survey* pamoja na kujenga miundombinu ya umeme. Lakini vijiji 13 ameambiwa tu afanye *survey* ukizingatia ndani ya vijiji hivyo ndiko kunakojengwa kiwanda kikubwa cha sukari ambacho kitaanza ujenzi mwaka huu pamoja na Bwawa la Kidunda.

Je, Serikali imejipanga vipi ili kumalizia na ujenzi katika vijiji hivi 13 na vijiji vile vingine vya Tomondo na sehemu zingine? (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza Mheshimiwa Mgumba amejielekeza kwenye utekelezaji wa miradi ya REA Awamu ya Kwanza na REA Awamu ya Pili ambako yako maeneo mbalimbali yalirukwa.

Napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo ambayo yalirukwa katika awamu ya kwanza na ya

pili Serikali yetu imekuja na mpango wa *densification*, kwa maana ya ujazilizi katika maeneo ambayo taasisi za umma, vijiji na kaya mbalimbali. Kwa kuwa *densification* imetekelezwa katika mikoa nane ya awali kama ambavyo tumepata kusema ndani ya Bunge lako Tukufu, awamu inayofuata sasa Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini imeajiri mshauri elekezi ambaye ni *Multiconsult ASA* kutoka Norway pamoja na NORPLAN ya Tanzania kwa ajili ya kufanya *verification* ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia kupitia Wakala wa Umeme Vijijini imeomba ufadhili kutoka Norway, Sweden na Ufaransa kwa ajili ya *densification* ya awamu ya pili. Nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba maeneo mbalimbali na mikoa mbalimbali yataanza kufikiwa na *densification* ya awamu ya pili ikiwemo Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Mgumba amejielekeza kwenye maeneo yale ambayo kama ambavyo amerejea jibu letu Bungeni la Mkutano wa Tisa kwamba katika vijiji vyake 20, vijiji saba vimefanyiwa *survey* na hivyo 13. Kama tunavyotambua jimbo hilo miradi mikubwa ya kimkakati inatekelezwa ikiwemo ujenzi wa Kiwanda cha Sukari pia na ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge nia yetu sisi kama Wizara ya Nishati ni kuwezesha sekta zingine. Kwa hiyo ni wazi kabisa kwamba vile vijiji 13 ambavyo vipo katika maeneo ambayo miradi mikubwa inapita tumemuelekeza mkandarasi ambaye ni *State Grid* maeneo yote ambayo amefanya upembuzi yakinifu amalizie kuendelea na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mgumba kwamba maeneo yote ambayo ameyataja, hivyo vijiji 20 lakini pia kwa kutambua umuhimu wa maeneo hayo pia tumemuongezea vijiji nane vikiwemo vijiji viwili katika Kata ya Mkulazi ambako mradi mkubwa wa ujenzi wa kiwanda cha sukari unafanyika na Bwawa la Kidunda. Pamoja na kwamba maagizo ya Serikali pia yameelekeza kwamba maeneo ambayo kuna miundombinu

mikubwa ya umeme iliyopita katika kata yake mojawapo ambayo ameitaja Tomondo pia tumempa vijiji vinne kwa sababu iko karibu na Kata ya Kiloka na Mikese ambako kuna miundombinu ya umeme. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara inafanya kazi pamoja naye. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Joseph Monko swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii, na niwashukuru sana wana-CCM na Chama changu cha Mapinduzi na hasa wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini kwa kuniwezesha kuwa mwakilishi wao hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yaliyozungumwa katika Jimbo la Morogoro Kusini yanafanana sana na Jimbo la Singida Kaskazini. Jimbo la Singida Kaskazini wakati unaongelea usambazaji wa umeme *REA* Awamu ya Tatu tulipata Mradi wa *REA* Awamu ya Pili katika vijiji vya Mrama, Makhandi, Mitula, Merya, Mipilo, Magojoha, Msange, Madasenga, Njia Panda, Mohamo, Mwamba na Mgori. Hata hivyo, mwaka 2016 mwishoni mkandarasi huyo alifilisika wa SPENCON na kazi hiyo ilisimama tangu mwaka 2016 na hadi sasa mradi huo haujaendelea mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri atuambie Serikali inatueleza ni lini mkandarasi mwingine atapatikana kwa sababu mkandarasi huyu aliyekuwepo tunaambiwa hawezi kuomba tena kazi hiyo ya kuendeleza shughuli hiyo ya *REA* Awamu ya Pili, atapatikana mkandarasi mwingine na kumalizia shughuli hiyo ili wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini waendeleo nao kunufaika na nishati ya umeme? Ahsante sana. *(Makofi)*



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu swali hili la nyongeza la Mheshimiwa Monko. Na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Monko kwa kuaminiwa na wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumepata kusema ndani ya Bunge, na tumeweza kuwapa pole wananchi wa Mikoa ya Singida na Kilimanjaro baada ya kutokea matatizo ambayo hayakutarajiwa ya mkandarasi SPENCON ambaye kwa kweli alifanya kazi kama asilima 65 na akashindwa kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyopata kusema pia, Serikali kwa kuliona hilo ikachukua hatua stahiki kupitia Wakala wa Umeme Vijijini na kuanza harakati za kutafuta mkandarasi mpya kwa ajili ya kumalizia kazi zilizosalia katika Jimbo la Singida Kaskazini pamoja na majimbo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mchakato huu ambao umefanyika na Wakala wa Umeme Vijijini tumefanikiwa kumpata mkandarasi katika Mkoa wa Kilimanjaro ambaye ameshaanza kazi na mimi nimejiridhisha, nilienda nikamuona, lakini katika Mkoa wa Singida mchakato unaendelea kwa sasa kwa wakandarasi wale watarajiwa kuwasilisha *performance bond* na baada ya hapo mkataba wa awali ambao wameuwasilisha kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mapitio na tunatarajia mwezi Machi mwaka huu kazi zianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, na baada ya kikao hiki cha Bunge lako tukufu naomba tuonane naye kwa ajili ya kumweleza kazi zitakazofanyika na vijiji ambavyo vitafikiwa ili aweze kuwaambia wananchi wake. Nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninayo matangazo na pia baadaye nitatoa Mwongozo uliokuwa umeombwa hapa Bungeni mapema.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na matangazo ya wageni; tunao wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika na hawa ni wageni wa kwangu mimi ambao ni wanakwaya wa Kanisa Kuu la KKKT *Azania Front* lililopo Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali; kwanza ni wageni 15 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni wafanyakazi wa Gazeti la Majira kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tunao wageni 46 wa Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni ambao ni Wauguzi wa Afya kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati chini ya Chama cha Uuguzi Nchini (*TANA*) Mkoa wa Manyara. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambao ni viongozi na wajumbe wa *Development Entrustment and Neighborly Organization* kutoka Mkoa wa Pwani. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu ambao ni wanafunzi wa *UDOM* na waandishi wa habari kutoka Mkoa wa Tabora. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni wajumbe ya maandalizi ya *Miss Journalism World* kutoka Mkoa wa Arusha. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa ambao ni familia yake kutoka Amani Mkoa wa Mjini Magharibi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosomea Madini kutoka Ushetu Mkoa wa Shinyanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ally Ungando ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimboni kwake Kibiti, Mkoani Pwani. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa ambaye ni rafiki yake kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye ni mke wake kutoka Jijini Arusha. Karibu sana. Pia tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ambaye ni mpiga kura wake kutoka Kigamboni Mkoa wa dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni majirani zake hapa Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembela Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Mzumbe kilichopo Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Mkoani Dodoma. Karibuni sana. Tunao pia wanafunzi 75 na walimu watano kutoka shule ya *Independent School DIS* Mkoa wa Dar es Salaam, nadhani hawa pengine hawakufanikiwa kuingia asubuhi hii.

Tunao pia wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Dar es Salaam. Sijui kama wamefanikiwa kuingia. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni wetu na pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na naamini wageni mliokuja

kujifunza mtaweza kujifunza namna tunavyoendesha shughuli zetu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine ambao hawakupata nafasi kwenye hiyo karatasi niliyosoma. Mheshimiwa Mwamoto ana mgeni wake ambaye ni Diwani wa Kata ya Image, Kilolo, Mheshimiwa Joseph Muhuma. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Norman King na yeye ana wageni wawili ambao wanatoka Redio Kitulo, Makete, na huyu ni Ndugu Aldo Sanga na Veronica Mtauka. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeandaa mwongozo kwa watumiaji wa huduma mbalimbali za mawasiliano hapa nchini kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano na kulinda haki za watumiaji wa huduma hizo. Nakala za mwongozo huo pamoja na muhtasari wake zimewekwa katika maboksi yenu ya taarifa. Kwa hiyo, kila Mbunge akachukue kwa ajili ya rejea yake.

Waheshimiwa Wabunge, nakala hizi nilizipokea jana kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kwa ajili yenu ili muweze kufahamu lakini pia muweze kuwataarifu wapiga kura wenu kuhusu mawasiliano ndani ya nchi na sheria zimerahisihwa ukisoma kwenye hicho kitabu ama kwenye hiyo rejea. Kwa hiyo zitatusaidia ili tusingie katika matatizo na Mamlaka yetu ya Mawasiliano Tanzania lakini pia wananchi wetu wasikosee.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

### **Mwongozo Kuhusu Uvunjaji wa Kanuni ya 64(1)(d) na (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa Spika, uliombwa na Mheshimiwa Jenista Joakim

Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kuhusu uvunjaji wa Kanuni ya 64(1)(d) na (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi kilichofanyika tarehe 7 Februari, 2018 Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu baadhi wa Wabunge kuvunja Kanuni ya 64(1)(d) na (e) wakati wa mijadala Bungeni.

Mheshimiwa Jenista Mhagama katika maelezo ya kuomba Mwongozo wa Spika alimtaja Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea ambaye wakati akichangia katika mjadala alitumia jina la Rais kama kigezo cha kuhalalisha hoja yake. Nanukuu maelezo ya Mheshimiwa Jenista kama yalivyonyukuliwa katika Taarifa Rasmi za Bunge; *“Hivi katika mjadala wa leo asubuhi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa majibu mazuri sana akijibu hoja za Mheshimiwa Mtolea. Kumeanza kujitokeza tabia ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapochangia michango yao ndani ya Bunge ili kuhalalisha michango hiyo wakati mwingine wamekuwa wakitumia utendaji wa kazi ya Rais wetu kuwa ni kigezo cha kuhalalisha hoja zao ndani ya Bunge...”*

Waheshimiwa wawili mliosimama hapo naomba mkakae, Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Grace naomba mkae, Mheshimiwa Lwakatare naomba ukae. Mheshimiwa unayesimama naomba ukae pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu nikiwa nimesimama hapa na ninyi mmesimama ni kama na nyie mna hoja. Tafadhali. *(Makofi)*

Nitarudia kusoma maelezo ya Mheshimiwa Jenista Mhagama; *“Hivi katika mjadala wa leo asubuhi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa majibu mazuri sana akijibu hoja za Mheshimiwa Mtolea.”*

*“Kumeanza kujitokeza tabia ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapochangia michango yao ndani ya Bunge, ili kuhalalisha michango hiyo wakati mwingine wamekuwa wakitumia utendaji wa kazi wa Rais wetu kama ni kigezo cha kuhalalisha hoja zao ndani ya Bunge na wanapofanya hivyo, wakati mwingine uhalalishaji huo hauna uhakika na wakati mwingine unapotosha jamii katika ile misingi tuliyojiwekea ya Kikanuni ndani ya Bunge letu Tukufu.”*

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote kwa kufanya hivyo Kanuni ya 64(1) na hasa kanuni ndogo ya (d) na (e) imekuwa ikivunjwa mara nyingi sana ndani ya Bunge kwa tabia hiyo ya baadhi ya Wabunge kutumia utendaji kazi wa Rais wetu katika kuhalalisha michango yao na uhalalishaji huo wakati mwingine unapotosha maana halisi ya utendaji wa Rais katika nchi yetu na katika Serikali yetu.”*

Waheshimiwa Wabunge, nimesoma Taarifa Rasmi za Bunge hususan mchango wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea, wakati wa mjadala wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati hizo kwa mwaka 2017. Katika mchango wake Mheshimiwa Abdallah Mtolea alimtaja Mheshimiwa Rais kwamba wakati wa maadhimisho ya sherehe za uhuru alitoa msamaha kwa Babu Seya na wenzake ambao ni wabakaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Malembeka naomba urudi ukae.

Waheshimiwa Wabunge, katika mchango wake Mheshimiwa Abdallah Mtolea alimtaja Rais kwamba wakati wa maadhimisho wa sherehe za Uhuru alitoa msamaha kwa Babu Seya na wenzake ambao ni wabakaji. Nanukuu baadhi ya maelezo yake; *“...lakini mbaya zaidi kwenye maadhimisho ya uhuru wa Tanganyika ukatoka msamaha kwa Babu Seya na wenzake watu ambao pasipo na shaka Mahakama zilithibitisha kwamba hawa watu ni wabakaji. Sasa tunapokuwa tunasamehe wabakaji wapi ulinzi wa watoto*

*katika Taifa hili? Tunawafundisha nini? Misingi yetu ya kukomesha vitendo hivi imepotelea wapi sasa, lakini tunakwenda mbali zaidi tunawachukua tunawapeleka lkulu, tunawapandisha kwenye majukwaa wafanye show kwamba tunaona kwamba ni kioo cha jamii, wanafundisha nini, watoto wajifunze nini kutoka katika hilo? (Makofi)*

*“Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mamlaka makubwa ambayo Mheshimiwa Rais anayo chini ya Ibara ya 45 ya kuwafutia watu kifungo lakini kufuta kifungo hakuondoi kuwa wewe ni mkosaji wa kosa fulani.”*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64(1)(d) na (e) inatamka bayana kuwa nanukuu:

*“(d) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatumia jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kullishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.”*

*(e) hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote...”*

*(Hapa Mhe. Joshua S. Nassari alizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassari ninazungumza!

*“(e) hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, Jaji, Hakimu au mtu mwingine yeyote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahsusi kuhusu jambo husika”*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka na Katiba ya nchi chini ya Ibara ya 45 kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mbele ya Mahakama kwa kosa lolote. Hivyo, kitendo cha Mheshimiwa Abdallah Mtolea kuhoji mamlaka ya Rais kutoa msamaha kwa mtu yeyote ni kitendo cha kuingilia mamlaka ya Rais na

pia ni kitendo cha kutumia vibaya jina la Rais kinyume na Kanuni za Kudumu za Bunge kama zilivyonukuliwa hapo juu. Mheshimiwa Rais alitoa msamaha kwa wafungwa hao kwa mujibu wa Katiba na Sheria zilizopo. Pia kitendo cha Mheshimiwa Abdallah Mtolea Mbunge, kutaja jina la Rais kwamba anawapandisha wafungwa waliosamehewa kwenye majukwaa kufanya *show* ni kitendo cha kutumia jina la Rais kwa dhihaka. Mheshimiwa Rais hajawahi kufanya jambo kama hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na kauli hizo za uvunjaji wa Kanuni ya 64(1) (d) na (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa kutumia mamlaka ya Spika chini ya Kanuni ya 5 na Kanuni ya 72, naelekeza kuwa maneno yote yaliyomtaja Mheshimiwa Rais katika mchango wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea yafutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Pia nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 64(1) (d ) na (e ) kwa kuepuka kutumia jina la Mheshimiwa Rais kwa dhihaka au kuzungumzia mwenendo wa Rais katika mijadala kama Kanuni zetu zinavyotaka. Huo ndio mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ikienda sambamba na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani anajibu swali langu, swali Namba 114 hakujibu swali kikamilifu, maswali yangu yote mawili ya nyongeza lakini swali la pili hajagusia kabisa. Swali la kwanza amezungumza mambo mengi ambayo hayakuendana na lile swali nililomuuliza, swali la pili hajagusa kabisa.



Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu moja tu ya msingi. Hivi sasa nazungumza kiongozi wetu Husna Amri, ana hali mbaya yuko wodini ana-*bleed* sana, lakini bado ninavyozungumza hivi hakuna hatua yoyote imechukuliwa, lakini ushahidi tunao kwa sababu askari pia aliyemfanyia yale mambo ni mwanaume akamfanyia mwanamke. Pia alivyokuwa anaondoka mpaka namba zake ameziacha pale. Tunategemea Serikali kwenye mambo hayo iwe *serious*, huwezi kufanya siasa kwenye afya ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha ya watu wetu, tumekaa hapa kama wawakilishi wao, inapotokea tunauliza maswali kwa Serikali tunategemea majibu ya Serikal. Yanapokuja majibu kama haya mepesi kwenye maisha ya watu inatupa mashaka sana sisi ambao ni Wabunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu ushahidi upo ili Naibu Waziri kama hana uhakika na haya tumpe uhakika na Serikali itoe tamko na ichukue hatua kwa wale watu waliofanya mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7). Hiki ni kikao cha Tatu cha Bunge nimekuwa nikihudhuria hapa hali ya kuwa sijawahi kupata swali hata moja la kuuliza na nikijua kuna maswali zaidi ya 30 nimepeleka katika Ofisi ya Maswali na Majibu Bungeni. Nisingeuliza lakini nauliza kwa sababu nawaona ambao kila kikao cha Bunge wanapata maswali na wanajibiwa. Hivi kuna nini? Maana ikiwa maswali yetu tunayopeleka yana ukakasi na hayajibiki basi tungelewa barua tukaambiwa swali lako haliwezi kupata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukaa, mimi ni Mwakilishi wa wananchi, wananchi wanatupa maswali yao tuwaulizie hapa na wapate majibu, leo Mbunge nakuja narudi hakuna swali langu linaletwa, haileti picha nzuri, kuna *double standard* katika Ofisi ya Maswali na Majibu Bungeni jambo ambalo halikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako juu ya kinachofanyika katika Ofisi ya Maswali na Majibu hapa Bungeni, kuna nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 64(1) bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni hasa Bunge hili kumezuka mtindo ambao unataka kuligeuza hili Bunge liwe kama ni *Executive* badala ya kwamba sisi tuwe *representative*. Sisi ni wawakilishi wa watu (*taxpayers*) ambao wanatuleta hapa tusimamie kodi yao, lakini imefika mahali chochote tunachogusa humu ndani tukijaribu kuikosoa Serikali, tukikosoa mhimili wa Serikali na kujaribu kuisahihisha inakuja hii kinga na visingizio vya kwamba tunatumia jina la Rais vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ndiye anayesimamia kodi za wananchi, ndiyo zinakuwa *allocated*, anasimamia, lakini sisi ni *watchdogs* tuhakikishe hizo hela zinatumika vipi. Sasa kila tunachokifanya humu ndani ya Bunge tunaambiwa tunatumia jina la Rais vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, kazi ya Bunge hasa ni nini? Tuko hapa Bungeni kufanya nini? Kwa sababu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaruhusu uhuru wa mawazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais amekuwa *over protected* kiasi kwamba hawezi kuguswa katika Bunge hili kwa mujibu wa sheria. Ofisi ya Rais haipaswi ku-*allocate* fedha zozote bila idhini ya Bunge, lakini kuna ushahidi mwingi sana pesa nyingi zinatumiwa kinyume na utaratibu na sheria ya nchi hii tukijaribu kugusa Rais *is over protected, why* tuko hapa? Naomba mwongozo wako Bunge hili kazi yake ni nini? Sisi ni *Executive* au *Representative*? Kama ni *Representative how do we represent our people?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wiki ya kwanza ya Bunge niliomba mwongozo ambao niliahidiwa na Kiti chako kupata majibu lakini inavyoelekea leo ni siku ya mwisho hakuna majibu, mwongozo ulihusu hali mbaya ya uvuvi katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali la Mheshimiwa Joyce Sokombi na katika sehemu yake ya kwanza ya majibu ameeleza kwamba kila samaki ana nyavu yake na katika majibu yake akakiri katika uvuvi wa dagaa siyo bahati mbaya kukamata furu, sato na sangara wa *size* tofauti. Hata hivyo, wavuvi katika Ziwa Victoria na hasa wavuvi wa dagaa wanakamatwa wakiwa na samaki mchanganyiko, wadogowadogo wa *size* tofauti na kupigwa faini kubwa na kuwekwa ndani.

Naomba mwongozo wako sasa ni majibu yapi sahihi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ili wananchi wetu kule waweze kufahamu kwa sababu unyanyasaji huu unaendelea katika eneo zima la Ziwa Victoria. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ninataka

mwongozo wako hasa kwenye jambo ambalo linaendelea sasa hivi. Hapa karibuni wakulima wa korosho wamekuwa wakilipwa pesa zao kwa kutumia *bank account*. Kwa bahati mbaya kabisa umejitokeza wizi mkubwa sana wa kimitandao hasa katika Mikoa ya Mtwara na Lindi na tumeona uwezo kidogo wa Jeshi la Polisi katika kulisimamia hili na mara nyingi watu wale wakiibiwa pesa zao askari wamekuwa wakiwaambia watoe pesa kwa ajili ya kufuatilia wezi kule waliko na limekuwa likiendelea tatizo hili ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mwongozo wako ili uielekeze Wizara ya Mambo ya Ndani kuongeza nguvu ili kuweza kuwasaidia wakulima wale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7), lakini ni jambo ambalo sasa hivi linajadiliwa sana kwenye mitandao ya kijamii. Naomba Wabunge wenzangu tuache ushabiki kidogo juu ya jambo hili ambalo nitalisema kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, timu zetu za Simba na Yanga zinashiriki michuano ya Kimataifa, Yanga inashiriki michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Simba wanashiriki michuano ya kombe la shirikisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana na mimi kwamba mara nyingi timu zetu hizi zinaposafiri kwenda nje ya nchi wamekuwa wakifanyiwa vitimbi vya kunyimwa uwanja mzuri wa mazoezi wakati mwingine hata kupangiwa hoteli za hovyoo.

Sasa katika mazingira ya kushangaza jambo hili linafanyika kwetu, kwamba kuna timu inacheza na Yanga kesho na uwanja utakaotumika ni uwanja wa Taifa uliojengwa kwa kodi za Watanzania, badala ya ule uwanja kupewa timu ya Yanga wafanyie mazoezi na sisi wachezaji

wa mpira tunajua kwamba mazoezi ya siku mbili kabla ya mechi kwenye uwanja ule yana faida kubwa kuliko mazoezi ya siku zingine. Sasa badala yake *TFF* wamewakataza Yanga wasitumie Uwanja wa Taifa kufanyia mazoezi na wamewapa timu ngeni ndio wautumie wafanyie mazoezi ili wale jamaa wauzoe vizuri kuliko Timu ya Yanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako kwamba hizi ni hujuma za Wizara ama ndiyo mipango ya *TFF* ili Yanga itolewe katika mashindano. Naomba mwongozo wako. (*Kicheko/Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya watu wanapochangia Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa wanasema Serikali haijafanya kitu chochote, wakati kwenye Majimbo yao yako mambo makubwa ambayo yamefanyika. Kwa mfano, miundombinu ya barabara nchi hii sasa hivi, tunatembea kwa bajaji hata kutoka hapa kwenda Arusha, nchi nzima hali ni nzuri. Hali ya umeme *REA* Awamu ya I, II, III shughuli za umeme zitaendelea katika Majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya afya Serikali imeongeza fedha mpaka shilingi bilioni mia mbili na kitu, wakati huo huo Serikali imepeleka fedha kwa ajili ya vituo vya afya zaidi ya mia mbili na kitu katika nchi hii. Elimu, Serikali imefanya kazi nzuri, hali kadhalika maji, Wizara ya Maji wanapeleka maji katika miji na vijijini hali inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi naomba mwongozo wako kwa Mbunge anayesema Serikali haijafanya kitu chochote. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu

Spika, ahsante, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapozungumza jana katika Jimbo la Bunda kumetokea watu wanakwenda kwenye mashamba ya mgogoro kati ya Vijiji vitatu Mikomalio, Lemgololi na Silolisimba wanavuniana mashamba na wengine wawili katika kijiji changu cha Mkomalio wamekatwa mapanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 12 Januari watu wawili waliuawa kwenye mgogoro huo. Alikuwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Simbachawene mwaka jana tukamwambia mgogoro huo akatoa wiki tatu kuimaliza. Amekuja Waziri Mkuu watu wametoa mabango na maelezo wametoa waende kushughulikia mgogoro huo, mpaka tunavyozungumza hivi vijiji vitatu kila mtu ana mapanga anaenda kuvunia mashamba kwenye maeneo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, je, Serikali inasubiri watu wangapi wauawe ndipo mgogoro huo uishe?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo kadhaa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Nitaanza na mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Aida Khenani ambaye ametumia Kanuni ya 68(7) kuhusu majibu kwa maswali ya nyongeza aliyoyauliza kwenye swali namba 114.

Mheshimiwa Aida Khenani ametoa maelezo marefu ambayo sina haja ya kuyarudia, lakini kimsingi anasema maswali yake ya nyongeza yote mawili hayajajibiwa kikamilifu lakini zaidi swali la pili halikuguswa kabisa. Kwa hivyo, kwa maelezo yake anasema majibu yaliyotolewa kwa maswali yake hayaridhishi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa, jambo hili limetokea mapema leo na mimi sijajielekeza kujua kwamba, swali hilo liliulizwaje na limejibiwaje, lakini sasa hivi watu

wangu wa Ofisi wataniletea Taarifa Rasmi za Bunge hapa ili niweze kuona swali liliulizwa vipi na limejibiwa vipi. Kama majibu hayo yatakapokuja tutakuwa pengine tumeshamaliza Bunge, basi tutatoa maelekezo baadaye kama majibu yaletwe upya ama kwa namna itakavyotolewa, lakini maelezo yatatolewa hapa Mheshimiwa Aida Khenani kuangalia maswali yalivyotolewa.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Khatib Haji kuhusu maswali yake ambayo kwa maelezo yake ni zaidi ya 30 ambayo yako Ofisi za Bunge na amekuja hapa Bungeni halioni swali hata moja ambalo limejibiwa. Nadhani ukifuatilia maelezo aliyoyotoa anaona kana kwamba, wapo Wabunge ambao maswali yao yanaletwa Bungeni haraka kuliko Wabunge wengine kwa hiyo, ndio msingi wake na anataka kujua kama maswali yake yamekataliwa ama vipi.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuna Mbunge aliomba Mwongozo hapa kuhusu jambo hili na nililitolea maelekezo ya nini cha kufanya, Waheshimiwa Wabunge ambao maswali yao ni mengi na wanaona hawajawahi kuuliza swali ama wameuliza, lakini si kwa kiasi cha Wabunge wengine kwa ulinganifu kwa maana kwamba, wengine wameuliza mengi zaidi kuliko wao, waende Ofisi ya Bunge inayohusu Maswali, ili kujiridhisha kama maswali yao yanakuja Bunge lijalo ama kwa nini hayajaja kwa namna majibu watakayopewa huko. Kwa sababu, kila Mheshimiwa Mbunge akija hapa akaeleza maswali yake mimi hapa nakuwa sina kwa hiyo, kutoa kwangu mwongozo kwamba, kwa nini maswali hayapo inaniwia vigumu.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge naomba wale ambao wana malalamiko kuhusu maswali, waende ofisi inayohusu Maswali, lakini kama ataenda kwenye ofisi ya Maswali na akaona hapati majibu anaweza kuja ofisini badala ya kuuliza hapa ili nimwite huyo Afisa anayehusika nizungumze naye kuhusu maswali ya Mbunge husika. Kwa hiyo, maelezo hayo Waheshimiwa Wabunge ndiyo Mwongozo wangu kuhusu jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia, Mwongozo na Mheshimiwa Peter Msigwa ambaye anasema amesimama kwa Kanuni ya 64(1) na ametoa maelezo kwa kirefu ambayo pia sina haja ya kuyarejea, lakini amesema anataka, mwisho wa maelezo yake akasema anaomba Mwongozo kwamba, Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni tumekuja kufanya nini kwa kuwa, Rais ni kama amelindwa sana. Katika maelezo yake akatoa maelezo ya Kifungu hicho cha 64(1). Sasa hapa kuna mambo mawili, moja amezungumzia Mwongozo na wakati huohuo amesema anasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 64, Mbunge anayesimama kwa kutumia Kanuni hii Fasilii ya Pili inaeleza atasema nini. Mbunge huyo atasimama Kuhusu Utaratibu na wakati akisema ni Mbunge mwingine anakuwa akichangia ndiyo unaweza kutumia Kanuni ya 64 kusimama Bungeni. Huwezi kusimama kwa kutumia Kanuni ya 64 ikiwa hakuna Mbunge aliyesimama akizungumza.

Pamoja na hayo, Kanuni ya 64(1) inazungumzia, nitaisoma ili Wabunge twende vizuri, inasema:

“Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge...” inatoa sasa maelezo ikiwa ni pamoja na hayo maelezo ya kutokutumia jina la Rais kwa dhihaka ama kulitumia hilo jina kutumia jina la Rais katika mjadala kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani.

KKatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 100 inazungumzia uhuru wa majadiliano, lakini sitasoma yote kwa sababu ya muda, nitawasomea 101 ambayo huwa ni lazima isomwe na 100. 101 inasema:

“Kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa majadiliano...” ambao ndio uko kwenye Ibara ya 100 inasema hivi, “Bunge linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti na kuwezesha Mahakama na Sheria kuhifadhi na kutilia nguvu



uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu wa shughuli katika Bunge, ambao kwa mujibu wa Ibara ya 100 umedhaminiwa na Katiba hii.”

Waheshimiwa Wabunge, uhuru wa majadiliano sio kwamba hauna mipaka, ndiyo maana Bunge hili limetunga sheria, ili mtu akitumia uhuru huo kuingilia haki za mtu mwingine aweze kushtakiwa. Kwa hiyo, kwa namna hiyohiyo, Bunge hili limejiwekea utaratibu wa kutilia mkazo uhuru wa majadiliano ndio maana Kanuni ya 64 ipo kutuambia kwamba, mambo gani yanaruhusiwa kwenye majadiliano na mambo gani hayaruhusiwi. Kwa sababu, kama uhuru wa kujadiliana ungekuwa hauna mipaka maana yake humu ndani hata sisi tungekuwa tunaweza kutukanana na tukaona ni sawa ama tukatukana watu wengine walio nje ya Bunge tukaona ni sawa, lakini tumewekewa mipaka hiyo ili tuweze kukazia huo uhuru.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Msigwa pamoja na kwamba, alitumia Kanuni ambayo inamtaka asimame Mbunge mwingine akiwa anazungumza, Mwongozo wangu ni kwamba, majadiliano ya humu ndani tumeyawekea utaratibu kwenye Kanuni hizi. Kwa hivyo, lazima Kanuni hizi ndizo tuzifuate, hatuwezi kutumia uhuru uliotajwa kwenye Kifungu cha 100 cha Katiba kwamba, sasa tunaweza kuzungumza vyovyote tupendavyo kwa sababu, tumejiwekea utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa John Kanyasu kuhusu hali mbaya ya uvuvi wa Ziwa Victoria na anasema alishaomba Mwongozo huko mwanzo na leo ameuweka Mwongozo wake akiuhusisha na majibu yaliyotolewa katika swali Namba 119 kuhusu uvuvi, kwamba, wavuvi wanakamatwa wakikutwa na samaki ambao ni wa aina tofauti na viwango tofauti.

Hapa wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali hilo ameonesha kwamba, tofauti hizo wao kama Wizara na Watendaji wao wanazifahamu na wanazitambua. Kwa kuwa, amesema hapa kwamba, mtu hawezi kukamatwa

kwa kukutwa na hizo tofauti maana yake ni kwamba, nyavu zile zinakamata wote, ndio majibu aliyoyatoa hapa. Sasa kwa maelezo ya Mheshimiwa Kanyasu kwamba, wako watu kwenye eneo la Geita ama tuseme eneo lote linalozunguka Ziwa Victoria, wavuvi wanakamatwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri jambo hili mlitafutie ufumbuzi leo. Muwape maelekezo watu wenu ni watu gani wanaopaswa kupewa adhabu na watu gani wanapaswa kukamatwa na kufungwa ikiwa wamefanya makosa, lakini siyo watu wanaokamatwa na viwango vya ukubwa tofauti vya samaki, kwa sababu mtego ulio halali unaweza ukashika samaki aliyehalali na asiye halali. Sasa anapokamatwa asiye halali na mtego ulio halali hapaswi kukamatwa mtu huyo, Wizara itoe maelekezo leo hii kwa hao watu ili wananchi wasiendeleo kuteseka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Cecil Mwambe, ametumia Kanuni yetu ya 68(7) akizungumza kuhusu wakulima wa korosho kwamba, wanalipwa kupitia benki. Ameelezea changamoto zilizopo na akasema anaomba Mwongozo ikiwa Wizara ya Mambo ya Ndani inaweza kuwasaidia wale watu kwa kupeleka Askari. Kimsingi jambo hili halijatokea hapa Bungeni, hata hivyo, kwa kuwa, Serikali iko hapa Mheshimiwa Waziri tafadhali muwahakikishie usalama watu hawa ambao wanakuwa na fedha zao na wanapata hizo changamoto.

Nimeombwa pia, Mwongozo na Mheshimiwa Bobali kuhusu mambo yanayotokea katika michezo. Ametoa maelezo marefu sana, lakini kimsingi anashangaa kwa nini Yanga isipewe Uwanja wa Taifa kufanya mazoezi inapewa uwanja mwingine, lakini wageni ndyo wanapewa uwanja ambao watatumia kucheza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo hili halijatokea hapa Bungeni pia. Kwa hivyo, kuhusu Mwongozo hapa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuwa Serikali iko hapa hebu walitazame jambo hili kwa karibu, lakini Kiti hakina Mwongozo juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Deo Sanga kwa kutumia Kanuni ya 68(7) kwamba, wapo Waheshimiwa Wabunge wanaosema kwamba, Serikali haijafanya chochote, wakati kwa maelezo yake Serikali imefanya mengi katika umeme, kuna mradi wa REA ambao umeenda vijiji vingi, lakini pia miundombinu ya barabara na kenye afya pia, kwamba, bajeti imeongezeka mara dufu. Sasa anaomba Mwongozo pale ambapo Mbunge anasema Serikali haijafanya jambo lolote anakuwa anamaanisha nini.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo huu unanipa ugumu kidogo, lakini kimsingi ni kwamba, mwenye macho huwa haambiwi tazama kwa hiyo, yeye anatazama kile anachoamua yeye kukiona ndicho anachokiona. Kwa hivyo, yeye anaweza kuwa hajaona hata kama na yeye anatumia hicho ambacho kipo. Kwa hiyo, barabara anaweza kuwa hajaona hata kama gari lake linapita juu ya barabara. Sidhani kama hilo linahitaji maelezo marefu, kila mtu anaruhusiwa kuona kile ambacho macho yake yanachagua kuona, nadhani huo ndio Mwongozo wangu Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na yeye ametumia Kanuni yetu ya 68(7) kuhusu Jimboni kwake kwamba, kwenye mgogoro wa ardhi wapo wananchi ambao wanakatwa mapanga na ametaja vijiji mbalimbali na kwamba mpaka sasa wapo katika hali ya taharuki. Pia alikuwa anauliza kwamba ni mpaka wafariki watu wangapi ndio Serikali itachukua hatua. Pamoja na kuwa jambo hili kimsingi halijatokea Bungeni, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhali uwahakikishie usalama hawa watu ambao wanapigana huko, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Naibu Waziri mko hapa, mmalize huo mgogoro ili hivyo vijiji visiendelee kupigana. Nadhani itabidi mshirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii kuona namna bora ya kumaliza tatizo hili ili wananchi wasiendelee kuuawa.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio Mwongozo wangu kwa hivyo, tutaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lipokee, lijadili na likubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Februari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa tunapoelekea mwisho wa uhai wa Kamati katika nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 116(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe 26 wa Kamati ambao katika kipindi chote cha uhai wa Kamati wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, naomba

kuwatambua na kuwapongeza Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Mheshimiwa Juliana Shonza, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati hii kwa kuteuliwa katika nafasi hizo mwezi Novemba, 2017. Kwa niaba ya Kamati tunawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalaani vitendo vyote vya kihalifu vinavyohatarisha amani na usalama wa nchi, ambavyo vinafanywa na wananchi wachache wasiopenda amani na utulivu katika nchi hii. Aidha, Kamati inawapa pole wananchi wote walioathirika na kuguswa na vitendo mbalimbali vya kihalifu kwa kipindi kinachotolewa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imesikitishwa na kitendo cha kupigwa risasi Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki, mwezi Septemba, 2017 ambacho kilileta mshituko mkubwa kwetu Wabunge na wananchi wote kwa ujumla. Watanzania wote tunapaswa kuendelea kulaani kitendo hicho na Kamati inaendelea kumwomba Mheshimiwa Tundu Lissu kwa Mwenyezi Mungu amjalie uponyaji wa haraka na aweze kurudi katika hali ya kawaida na kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inatoa pole kwa Watanzania na familia zote za Wanajeshi 15 ambao walipoteza maisha yao kishujaa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo walipokuwa wakihudumia katika kikosi cha Umoja wa Mataifa cha Kulinda Amani, mwezi Disemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inaeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2017 hadi Januari, 2018 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo:-

Sehemu ya Kwanza, inayotoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati, mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza majukumu na shughuli zilizotekelezwa. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi wa matokeo na utekelezaji wa majukumu ya Kamati na Sehemu ya Tatu inayobainisha maoni na mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne na ya mwisho ni hitimisho la taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane Fasili ya 6(3) pamoja na Fasili ya 7(1) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa za Kudumu za Bunge za Kisekta inayosimamia Wizara tatu. Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Majukumu ya Kamati hii yameelezwa kwa kina katika taarifa iliyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Februari, 2017 mpaka 2018, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, imetekeleza shughuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kushiriki semina, kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya Wizara, kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti, kuchambua mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge na kufanya mapitio ya taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kipindi kilichotolewa taarifa hii kwa kutumia Kanuni ya 119 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati ilikabidhiwa jambo moja na Mheshimiwa Spika la kuishughulikia hali ya ulinzi na usalama nchini, ikiwemo ulinzi wa Viongozi, mwezi Septemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza shughuli hiyo kwa ukamilifu na kuandaa taarifa iliyotoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ambayo Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuainisha kwa kifupi maelezo ya jumla kuhusu shughuli zinazotekelezwa, naomba sasa niwasilishe kwa kifupi sana sehemu ya Pili ya taarifa hii ambayo inaainisha masuala mbalimbali yaliyobainika ambayo changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilipofanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ya mwaka 2016/2017, ilibaini kuwa ucheleweshwaji au kutokupatikana kabisa kwa fedha kutoka Hazina na wakati mwingine kutoka kwa Wizara Mama ilikuwa ni changamoto katika utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Mambo ya Ndani ilipokea asilimia 28; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ilipokea asilimia 43.6; na Wizara ya Ulinzi na JKT ilipokea asilimia 14.5 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ilichambua utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi. Kwa uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza majukumu yake likiwa na changamoto mbalimbali zinazosababishwa na kutopatikana kwa ukamilifu kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Jeshi hilo. Jambo hili limeathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa katika kipindi hicho hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu nchini, upelelezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za Baharini na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imechambua ajali za barabarani ambayo makosa yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria za Barabarani, ambayo yameendelea kusababisha ajali nyingi pamoja na juhudi zinazofanywa na kitengo cha

Usalama Barabarani katika kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kwamba, Serikali itekeleze ushauri uliotolewa na Kamati katika taarifa yake ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017, kuhusu kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ili iguse maeneo sita yenye upungufu ambao unachangia ajali za barabarani zinazosababisha vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii imechambua ulinzi na usalama wa raia na mali zao ambayo Kamati iliridhishwa na juhudi za Serikali katika kushughulikia matukio mbalimbali ya uhalifu, hususan matukio ya Kibiti, Mkuranga na Rufiji ambayo yalikusisha mauaji ya Viongozi mbalimbali, Askari Polisi na Raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kutoa taarifa kwamba kazi nzuri iliyofanywa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika maeneo hayo, hali ya usalama sasa ni shwari. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kiini cha mauaji hayo kinajulikana na kudhibitiwa ili mauaji ya aina hiyo yasijirudie tena nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imechambua udhibiti wa usalama wa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wabunge. Kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi, Sura 322, Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hupewa ulinzi wa jumla wanapokuwa Bungeni au kwenye safari zao za kikazi, utaratibu huu unaliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge katika makazi yao wakiwa kwenye shughuli za Bunge na kwenye maeneo yao ya uwakilishi kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa wafungwa pia umejadiliwa sehemu hiyo ya pili, Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwenye tatizo sugu la msongamano wa wafungwa linalosabaishwa na sababu mbalimbali zikiwemo utegemezi wa adhabu za kifo, kifungo



gezani na matumizi hafifu ya sheria zinazohusu adhabu mbadala kwa wafugwa kama vile kifungo cha nje na huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hii pili pia imechambua Utekelezaji wa majukumu ya Kikosi cha Zimamoto ambayo imegundua kwamba fedha ambazo zilitakiwa kutolewa katika kipindi hicho hazikuweza kutolewa na Serikali kupitai Hazina ilitoa shilingi milioni 117 tu za miradi ya maendeleo licha ya kuwa katika mwaka huo wa fedha Kikosi hicho kilikusanya Sh. 31,725,254,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu hiyo pia imechambau mambo ya Wakimbizi ambayo ni miongoni mwa nchi 11 zilizopendekezwa kutekeleza Mpango jumuishi wa Umoja wa Mataifa ujulikanao kama '*Comprehensive Refugee Response Framework*'. Mpango huu ambao unasaidia wakimbizi pamoja na jamii wenyewe katika maeneo ambayo wakimbizi wanahifadhiwa na kunufaika na miradi mbalimbali. Kamati imebaini kuwa bado upo umuhimu wa Serikali yetu kuendelea kutafuta suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imejadili suala la Idara ya Uhamiaji ambayo inakabiliwa na madeni makubwa ya wazabuni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu kuanzia Mwaka 2013/2014 hadi 2016/2017 yanayofikia kiasi cha Sh.10,291,374,513.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Ulinzi pia imejadiliwa sana kwenye para hiyo *The National Defence Policy* ambayo imebaini kuwa mchakato wa sera hiyo bado haujakamilika. Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (*Beacons*) na uwepo wa makazi na shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo ya mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za mipakani tumejadili na ubovu wa barabara za mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka

yetu kwa nyakati zote. Suala la Shirika la SUMA JKT pia tumejadili kwa kirefu na moja ya mambo ambayo Kamati ilibaini katika utendaji wa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT ni changamoto inayokabili mradi wa matrekta na zana za kilimo kuhusu urejeshwaji wa madeni takribani shilingi bilioni 40. kutoka kwa Wakulima, Halmashauri za Wilaya na Viongozi waliokopa matrekta haya. Madeni haya yanaathiri sana utendaji wa SUMA JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi kwa JKT yamejadiliwa kwa kirefu sana. Kamati imebaini kwamba kwa kuwepo kwa migogoro ya ardhi katika Vikosi vya Jeshi hilo, migogoro hiyo inasababishwa na kuwepo kwa wavamizi wa ardhi ya Jeshi ambao hawataki kuhama katika maeneo hayo na wananchi kutokulipwa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi. Aidha, Mafunzo ya JKT yamejadiliwa na yameonekana kwamba fedha ambazo zinapekwa kwa ajili ya mafunzo hayo ni kidogo sana ni sawa na asilimia 12.5 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi pia umejadiliwa kwa kirefu na kuna kigezo cha uhaba wa fedha. Kamati inaamini mafunzo haya ni muhimu hivyo ni vema Wizara zote zikapeleka Maafisa Waandamizi kama ambavyo Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimekuwa vikifanya hivyo. Mafunzo hayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Tathmini ya Utawala Bora (*APRM Tanzania*); kwa kipindi cha takriban miaka mitano mfululizo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuipatia *APRM* fungu lake la kibajeti ili kukabiliana na changamoto yake ya muda mrefu ya mgao mdogo wa fedha za bajeti inazopangiwa, hata hivyo ushauri huu bado haujatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Diplomasia; kwa takribani miaka 36 Chuo hiki kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kuacha kabisa kuchangia bajeti na kushiriki katika shughuli zote za uendeshaji wake mwaka 1982. Suala hili

limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Chuo na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo imeendelea kubeba jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia umejadiliwa Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) pia tumejadili kwa kirefu kwenye *paragraph* hiyo balozi zetu za Tanzania nje ya nchi ambazo zimeendelea kuwa na ukwasi wa kutokupatiwa fedha licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii mara kwa mara kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo badala ya kupeleka Wizarani. Bado ushauri huo haujatekelezwa. Aidha Uchakavu wa majengo kwenye Balozi hizo unasababisha athari mbalimbali kwa Taifa letu ikiwa ni pamoja na kuliondolea Taifa heshima na kuharibu twasira ya Tanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki; bado Serikali haina Sera mahsusi inayotoa mwongozo kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki, licha ya kwamba suala hili limekuwa likishauriwa na Bunge tangu hivyo. Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje *Foreign Policy* bado linakwenda taratibu sana na tunashauri mchakato huo ufanywe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limetokea hivi karibuni, imejitokeza changamoto ya baadhi ya meli zilizokuwa usajili wake ukizoea kukamatwa zikifanya vitendo vya kihalifu ikiwemo kubeba madawa ya kulevya na vifaa vya kutengeneza silaha kali za kivita. Jambo hili limeitia aibu nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kama ilivyoahidi Bungeni tarehe 2 Mei, 2017 na kusawazisha kasoro za msingi zinazosababisha jambo hili ili lisitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipitia Kamati ilipitia na kujadili taarifa za wawakilishi *ACP-EU, CPA, SADC-PF* na kubaini kuwa kutokupatikana kwa fedha kwa ajili ya Wabunge kushiriki mikutano kumeendelea kuwa

changamoto iliyoathiri fursa ya Wawakilishi kushiriki ipasavyo katika mikutano hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye maoni na mapendekezo ya taarifa yote. Masuala ya Jumla; Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii. Kwa mfano, Wizara ya Mambo ya Ndani:

(i) Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali za kibajeti zinazoathiri utendaji wa Jeshi hilo katika kusimamia usalama wa raia na mali zake;

(ii) Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ina upungufu unaochangia uwepo wa tatizo sugu la ajali za barabarani;

(iii) Ucheleweshwaji wa kutoa taarifa rasmi kwa umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu na yanayovuta hisia za jamii kama vile matukio ya mauaji, kutekwa na kupotea kwa Viongozi na wananchi mbalimbali kunasababisha wananchi kutokujua hatua za upelelezi zilizofikiwa;

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu rasmi wa ulinzi kwa Wabunge katika makazi yao kunahatarisha usalama wao hasa kwa kuzingatia kuwa, baadhi ya majukumu yao katika kuisimamia Serikali yanagusa maslahi ya watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;

(v) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole* na matumizi hafifu ya sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

(vi) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(vii) Kutokutolewa kwa fedha za miradi kwa Jeshi la Zimamoto kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo kunaathiri utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na mifumo na juhudi za uokoaji na zimamoto;

(viii) Kutokuwa na suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi nchini kunaendelea kuhatarisha usalama katika maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguka; na

(ix) Madeni makubwa ya Wazabuni kwa Idara ya Uhamiaji yanasababisha Idara hiyo kushindwa kupata na kutoa Hati za Kusafiria kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na JKT:-

(a) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (*National Defence Policy*) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;

(b) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (*beacons*) kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;

(c) Ubovu wa barabara za mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi;

(d) Madeni kwa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa shirika hilo;

(e) Wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya wananchi na vikosi vya Jeshi hilo;

(f) Muda wa miezi mitatu kwa ajili ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria haukidhi katika kuwajengea moyo wa uzalendo vijana wala kuwaandaa kuwa Jeshi la Akiba; na

(g) Baadhi ya Wizara kutokutenga fedha kwa ajili ya

mafunzo ya Maafisa Waandamizi katika Chuo cha Ulinzi kunasababisha Maafisa hao kutohudhuria kozi muhimu za usalama na uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:

(a) *APRM* Tanzania kutokuwa na Fungu lake la Kibajeti kunaathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti;

(b) Kutokutoa kipaumbele katika kushughulikia changamoto zinazokikabili Chuo cha Diplomasia kunahatarisha Chuo hicho kufutiwa Usajili;

(c) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kunaikosha nchi fursa ya kuvutia mikutano na maonesho ya Kimataifa mengi zaidi kufanyika hapa nchini;

(d) *A/ICC* kutokuwa na majengo ya kutosha kwa ajili ya shughuli za Mikutano unakiondolea Kituo hicho ufanisi kwa kushindwa kushindana katika soko;

(e) Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo;

(f) Kutokukarabati majengo ya Balozi zetu si tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia kunaathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

(g) Kukosekana kwa Sera ya Taifa kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki ni jambo la hatari katika mustakabali wa nchi;

(h) Sera ya Mambo ya Nje ni ya muda mrefu na mchakato wa kuifanyia marekebisho unachukua muda mrefu kukamilika;

(i) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa na Itifaki iliyosainiwa kunachelewesha nchi/wananchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye mikataba hiyo; na

(j) Kutoainisha sheria za nchi na mikataba au Itifaki za Kimataifa zilizoridhiwa kunasababisha mkanganyiko kati ya Sheria ya Kimataifa na Mfumo wa Sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wawakilishi wa Vyama vya Kibunge:

(a) Kutokupatikana kwa fedha kwa ajili ya kushiriki mikutano kumeendelea kuwa changamoto iliyoadhiri fursa wa Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge kushiriki ipasavyo katika masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika mikutano hiyo;

(b) Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge kutoshiriki kikamilifu mikutano ya vyama hivyo, kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge; na

(c) Wawakilishi wa Bunge kutokukutana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama kabla ya kuhudhuria mikutano ya Vyama vya Kibunge kunaweza kusababisha wawakilishi hao kutokuwa na msimamo wa pamoja na Bunge katika masuala wanayoenda kujadili katika mikutano hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya taarifa hii. Baada ya kueleza maoni, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Kutokutolewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo:-

Kwa kuwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi

kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hazikutolewa kwa ukamilifu, jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wake;

Na kwa kuwa kutokutekelezwa kwake kumesababisha hasara kutokana na madeni ya kimkataba na riba na kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi;

Kw ahiyo basi Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma yake kwa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu:-

Kwa kuwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya mafuta, magari, operesheni mbalimbali na vitendeakazi;

Na kwa kuwa ufinyu huo wa bajeti unaathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu, upelelezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za baharini na Maziwa Makuu;

Kwa hiyo basi Serikali iongeze bajeti ya Jeshi la Polisi na kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili Jeshi hilo liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, mikoa ambayo takwimu zinaonesha kiwango cha uhalifu kipo juu, ipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao:-

Kwa kuwa matukio yanayohatarisha hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao yamekuwa yakijirudia na hivyo kujenga hofu miongoni mwa Wananchi;

Na kwa kuwa taarifa za hatua zilizofikiwa katika



upelelezi wa matukio hayo zimekuwa hazitolewi mara kwa mara kwa umma na hivyo kusababisha wananchi kutokujua hatua za upelelezi zilizofikiwa;

Kwa hiyo basi Jeshi la Polisi liwe na utaratibu mahsusi wa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua zinazofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu ambayo yamevuta hisia za jamii kama vile mauaji na kupotea kwa wananchi mbalimbali, unyang'anyi wa kutumia silaha na dhalika. Aidha, Jeshi la Polisi lihakikishe likamilisha upelelezi wa kesi zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulinzi na Usalama wa Wabunge:-

Kwa kuwa hakuna Sheria wala Kanuni inayoelekeza Wabunge kupewa ulinzi katika makazi yao na hivyo kuliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe;

Na kwa kuwa kazi za Wabunge katika kuisimamia Serikali zinagusa maslahi ya watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;

Kwa hiyo basi, Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la Wabunge kupewa ulinzi hususan katika makazi yao wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kibunge Mjini Dodoma na katika maeneo yao ya Uwakilishi. Pili, kuweka utaratibu wa kutoa namba maalum za usajili wa magari ya Wabunge, kama vile (MB) Muheza, (MB) Viti Maalum Mbeya na kadhalika. Aidha, Serikali iboreshe na kuimarisha ulinzi katika maeneo ya maegesho ya magari hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani:-

Kwa kuwa tatizo la msongamano wa Wafungwa na Mahabusu katika Magereza nchini limeendelea kuwa sugu;

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu vile vile kuiongezea Serikali gharama za kuwatunza;

Hivyo basi (i) Serikali itekeleze Sheria inayowataka wahalifu wenye makosa madogo kupewa adhabu mbadala kama vile vifungo vya nje na huduma kwa jamii; (ii) Izingatie kuwapeleka Mahabusu mahakamani kwa tarehe walizopangiwa; (iii) Itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole*; (iv) Ihakikishe kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi kutolewa kwa wakati; (v) Yatolee maamuzi kwa suala la wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu za nje:-

Kwa kuwa utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu unataka fedha hizo zipitishwe katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

Na kwa kuwa utaratibu huo umebainika kuwa na urasimu usio wa lazima na hivyo kuchelewesha kutuma fedha kwa mtiririko unaotakiwa;

Kwa hiyo basi Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka fedha katika Balozi moja kwa moja bila kupitisha Wizarani kama ilivyo kwa Halmashauri zote nchini ambapo fedha hutumwa moja kwa moja bia kupitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania:-

Kwa kuwa majengo mengi ya Balozi zetu nje ya nchi ni chakavu sana;

Na kwa kuwa kutokarabati majengo hayo kumeendelea kuiongezea gharama Serikali kwani baadhi ya Balozi zinalazimika kukodi majengo mengine mbadala;

Kwa hiyo basi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itoe fedha za ukarabati wa majengo ya Balozi kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa kuanza na Balozi ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uendeshaji wa Chuo cha Diplomasia:-

Kwa kuwa kwa takribani miaka 36 Chuo cha Diplomasia kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kujitoa;

Na kwa kuwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imefanya jitihada mbalimbali za kuwasiliana na Serikali ya Msumbiji ili ishiriki kikamilifu katika uendeshaji wa Chuo hicho bila mafanikio;

Kwa hiyo basi Serikali isisitize Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (*Joint Permanent Commission*) ambayo ndiyo yenye dhamana ya kushughulikia tofauti za makubaliano ya uundwaji wa Chuo hicho, hatimaye kuweka wazi kwa mujibu wa sheria kwamba chuo hicho sasa kimilikiwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wawakilishi katika Vyama vya Kibunge:-

Kwa kuwa Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Mabunge ya Vyama mbalimbali vya Kibunge wameshindwa kushiriki kikamilifu mikutano ya Mabunge kutokana na ufinyu wa Bajeti;

Hivyo basi Kamati inashauri Serikali kuipatia kupitia Ofisi ya Bunge fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwawezesha Wawakilishi wa Vyama vya Kibunge kushiriki mikutano yao kama ilivyopangwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera Mtengamano ya Afrika Mashariki:-

Kwa kuwa tangu mwaka 1969 Tanzania ilipojiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki haijawahi kuwa na sera maalum kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki;

Hivyo basi Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2017 na Januari 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba; Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi; na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Mashariki Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walionesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu nawashukuru watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Angellina Sanga, Makatibu wa Kamati hii ambayo wamefanya kazi kubwa sana Ndugu Ramadhani Abdallah na Bi Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vyema shughuli zetu za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa kifupi kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Februari, 2017 hadi Februari, 2018 na kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa kwa heshima naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, lijadili na hatimaye

kuikubali taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nchi za Nje Ulinzi na Usalama, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA  
NJE, ULINZI NA USALAMA KWA MWAKA 2017 -  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2017 hadi Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, Kamati inalaani vitendo vyote vya kihalifu vinavyohatarisha amani na usalama wa nchi ambavyo vinafanywa na wananchi wachache wasiopenda amani na utulivu katika Nchi yetu. Aidha, Kamati inawapa pole wananchi wote walioathirika na kuguswa na vitendo mbalimbali vya kihalifu kwa kipindi kinachotolewa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imesikitishwa na kitendo cha kupigwa risasi Mbunge mwenzetu Mhe. Tundu A. Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mwezi Septemba, 2017, ambacho kilileta mshtuko mkubwa kwetu Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla. Watanzania wote tunapaswa kuendelea kulaani kitendo hicho. Kamati inaendelea kumuomba Mheshimiwa Tundu Lissu (Mb) kwa Mwenyezi Mungu amjalie uponyaji wa haraka na aweze kurudi katika hali yake ya kawaida na kulitumikia Taifa.

Aidha, Kamati inatoa pole kwa Watanzania na familia zote za Wanajeshi 15 waliopoteza maisha yao kishujaa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo walipokuwa wakihudumu katika Kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda Amani, mwezi Disemba, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa tunapoelekea mwisho wa uhai wa Kamati katika nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Ninawashukuru Wajumbe wote Ishirini na Sita (26) wa Kamati ambao katika kipindi chote cha uhai wa Kamati wametumia Taaluma, Uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni wafuatao:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb- "
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb- "
5. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb- "
6. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb- "
7. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb- "
8. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb- "
9. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb- "
10. Mhe. Cosato David Chumi, Mb- "
11. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb- "
12. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb- "
13. Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb- "
14. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb- "
15. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb- "
16. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb- "
17. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb- "
18. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb- "
19. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb- "
20. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb- "
21. Mhe. Stephen J. Masele, Mb- "
22. Mhe. Machano Othman Said, Mb- "
23. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb- "
24. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb- "
25. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb- "

26. Mhe. Janeth Masaburi, Mb-

“

Aidha, naomba kuwatambua na kuwapongeza Mhe. George Huruma Mkuchika, Mb, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Kangi Aphaxad Lugola, Mb, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Mhe. Juliana Shonza, Mb, Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati hii, kwa kuteuliwa katika nyadhifa hizo mwezi Novemba, 2017. Kamati inawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inaeleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 na imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Kwanza inayotoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;
- ii. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu inayobainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- iv. Sehemu ya Nne ambayo ni hitimisho la taarifa hii.

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) ambazo ni:- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati hii ni yafuatayo:-

- i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazosisimamia;
- ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosisimamia;
- iii. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati ina majukumu ya nyongeza matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni yafuatayo:-

- i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
- ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
- iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
- iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama; na
- v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imetoa ruhusa kwa Kamati yoyote ikiwemo



Kamati hii, kupendekeza kwa Spika majukumu mengine ya nyongeza. Majukumu hayo ya nyongeza yanatekelezwa kwa namna mbili zifuatazo:-

a) Kamati kupendekeza ipewe jukumu la nyongeza; na

b) Mheshimiwa Spika kukabidhi Kamati jambo lingine lolote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Septemba, 2017, Kamati ilikabidhiwa jambo moja na Mheshimiwa Spika la kushughulikia hali ya Ulinzi na Usalama nchini ikiwemo ulinzi wa Viongozi. Kamati ilitokeleza shughuli hiyo kwa ukamilifu na kuandaa Taarifa iliyotoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ambayo Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Spika kwa ajili ya utekelezaji wake.

### **1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2016/2017 na 2017/2018. Njia zilizotumika ni:-

i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;

ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Vyama hivyo;

iii. Kuwataka Mawaziri kutoa maelezo na ufafanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi;

iv. Ziara za kuangalia na kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini

ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; na

v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018; na

#### **1.4 Shughuli zilizofanyika**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2017 - Januari, 2018 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

##### **1.4.1 Semina**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Februari, 2017 hadi Januari, 2018, Kamati ilishiriki na kuongoza Semina tatu zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, chini ya Mradi wa Awamu ya Pili wa kuliwezesha Bunge unaodhaminiwa na UNDP. Semina hizo zilihusu:-

i) Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyofanyika tarehe 28 na 29 Oktoba, 2017;

ii) Dhana na Utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau iliyofanyika tarehe 13 na 15 Septemba, 2017; na

iii) Namna ya kuchambua Miswada ya Sheria na Udhhibiti wa Sheria Ndogo katika Bunge la Tanzania iliyofanyika tarehe 04 na 05 Novemba, 2017.

##### **1.4.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo zimeainishwa katika Kiambatisho namba 1.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

**1.4.3 Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara inazosisimamia ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya Miradi Nane (8) ilikaguliwa katika kipindi cha Mwezi Machi, 2017. Miradi hiyo pamoja na vifungu vyake ni ifuatavyo:-

Fungu	Simbo ya Mradi	Jina la Mradi	Mahali Mradi ulipo	Thamani ya Mradi
14	6311	Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la zimamoto	Dar es Salaam	1,500,000,000.00
	6582	Ununuzi wa magari mawili ya Zimamoto		2,000,000,000.00
28	6107	<i>Offenders Management system</i> na <i>Digital mobile radio</i>	Dar es Salaam	100,000,000.00
	6302	Ufungaji wa lift katika jengo la Makao Makuu		300,000,000.00
34	6391 (411000)	Ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Ubalizi, Makazi ya Balizi na Mkuu wa Utawala	Maputo, Msumbiji	1,316,435,000.00
		Ukarabati wa Makazi ya Balizi na nyumba za Watumishi	Stockholm, Sweden	2,172,880,000.00
51	6501	Usajili na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa	Dar es Salaam	30,000,000,000.00
57	6103	Mkopo ya Mikataba ya ununuzi wa vifaa vya utafiti	Nyumbu, Pwani	177,500,000,000.00

**Mheshimiwa Spika**, mbali na kukagua Miradi iliyokuwa imetengewa fedha katika Mwaka 2016/2017, Kamati pia ilikagua majengo ya Ubalozi wa Tanzania yaliyoko katika Majiji ya Pretoria na Johannesburg nchini Afrika Kusini. Kamati ilifanya ziara hiyo ya ukaguzi kutokana na umuhimu wa ubalozi huo katika mahusiano ya Kiuchumi na Kidiplomasia kati ya nchi hiyo na Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, katika ukaguzi uliofanywa, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yalioathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

#### **1.4.4 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazosisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

#### **1.4.5 Kuchambua Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati hii ilishughulikia Mikataba miwili ya Kimataifa ifuatayo:-

i) Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula (The East African Community Protocol on Sanitary and phytonisnary Measures); na

ii) Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (The East African Community Protocol on Peace and Security)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua kwa kina Itifaki hizo na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake kuhusu Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati haikuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula kwa kuwa ilibainika kuwa na changamoto kadhaa ambazo Serikali iliomba muda zaidi wa kuzishughulikia.

#### **1.4.6 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge; na katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Januari 2017- Januari, 2018, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC - PF, CPA na ACP/EU.

Taarifa zilizopitiwa ni zifuatazo:-

i) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA);

ii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Bunge la Pamoja la Nchi za *Africa, Carribean na Pacific* (ACP) na Umoja wa Ulaya (ACP/EU); na

iii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC- PF).

Nakala za taarifa za wawakilishi wa Mabunge na Vyama hivyo zimeambatishwa katika Taarifa hii (Viambatisho 2-4).

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

#### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari, 2018, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni:-

#### a) Masuala ya Ujumla

Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

#### b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- i) Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi;
- ii) Ajali za Barabarani;
- iii) Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao;
- iv) Udhhibiti na usalama wa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wabunge;
- v) Msongamano wa mahabusu na wafungwa katika magereza;
- vi) Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto;
- vii) Huduma za Wakimbizi nchini; na
- viii) Utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uhamiaji.

**c) Wizara ya Ulinzi na JKT**

- i) Kukosekana kwa Sera ya Taifa ya Ulinzi;
- ii) Kukosekana kwa alama za Mipaka ya Nchi;
- iii) Ubovu wa barabara za Mipakani;
- iv) Utendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT);
- v) Migogoro ya ardhi katika Jeshi la Kujenga Taifa;
- vi) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria; na
- vii) Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC).

**d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

- i) Utendaji wa *African Peer Review Mechanism* (APRM);
- ii) Utendaji wa Chuo cha Diplomasia;
- iii) Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC);
- iv) Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC);
- v) Balozi za Tanzania kutopata fedha za miradi kwa wakati;
- vi) Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania;
- vii) Hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- viii) Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje; na
- ix) Mawasilisho ya Maazimio ya Bunge.

**e) Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge**

Ushiriki wa Wawakilishi wa Tanzania katika Mabunge mengine na Vyama mbalimbali vya Kibunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu katika sehemu ya taarifa inayofuata.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

### 2.2.1 Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2016/2017 ilibaini kuwa ucheleweshwaji au kutokupatikana kabisa kwa fedha kutoka Hazina na wakati mwingine kutoka kwenye Wizara Mama, ilikuwa ni changamoto katika utekelezaji wa miradi iliyotembelewa. Kutokana na changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi uligawanyika katika makundi matatu.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la kwanza ni miradi ambayo haikutekelezwa kabisa kutokana na kutokupelekewa fedha. Taarifa mbalimbali zilizotolewa mbele ya Kamati zilionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hazikutolewa kabisa, jambo lililokwamisha utekelezaji wake. Mfano wa Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6311** kuhusu ukamilishaji wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto uliotengewa Shilingi Bilioni 2. Mfano mwingine ni **Mradi Na. 6302** kuhusu ufungaji wa lift katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi uliotengewa Shilingi Milioni 300.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la Pili ni miradi ambayo ilitekelezwa kwa sehemu kutokana na kupelekewa fedha pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mfano wa Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6103** kuhusu malipo ya Mikopo ya Ununuzi wa vifaa vya Utafiti katika Shirika la Nyumbu.

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Mradi huu ulitengewa Shilingi Bilioni 151.1 kwa ajili ya kulipa madeni ya Mikataba ya ununuzi wa vifaa vya utafiti. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi 2017, mradi huu ulikuwa umepokea Shilingi Bilioni 30 ikiwa ni asilimia 20 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kutokutolewa kwa fedha hizi kwa ukamilifu kuliathiri ratiba za malipo ya Mikataba hiyo na hivyo kuzalisha madeni ya kimkataba na riba.



**Mheshimiwa Spika**, kundi la tatu ni miradi ambayo haikupelekewa fedha za utekelezaji wake kutoka Wizara mama. Mfano wa Mradi huo ni **Mradi Na. 6391** kuhusu Ukarabati wa Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi Jijini Stockholm nchini Sweden. Maelezo yaliyotolewa na Ubalozi mwezi Mei, 2017 yalibainisha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 2,172,880,000/= . Kamati ilibaini kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilipokea fedha hizo kutoka Hazina tarehe 2/12/2016. Hata hivyo, hadi Kamati inakagua mradi huo Mwezi Mei, 2017, fedha hizo zilikuwa hazijawasilishwa. Kamati iliarifiwa baadae kuwa fedha hizo ziliwasilishwa katika Ubalozi wa Sweden tarehe 07/06/2017.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hazikupokea kwa ukamilifu fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Taswira ya mtiririko wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo unaonekana katika Jedwali namba. 1

**Jedwali Na. 1: Hali ya upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

Wizara	Bajeti iliyochinishwa	Fedha zilizopokelewa	% ya fedha zilizotolewa	% ya fedha isiyotolewa
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	8,000,000,000	3,489,315,000	43.6	56.4
Ulinzi na JKT	248,000,000,000	35,900,000,000	14.5	85.5
Mambo ya Ndani ya Nchi	47,923,421,105	13,466,336,364	28	72
<b>JUMLA</b>	<b>303,923,421,105</b>	<b>52,855,651,364</b>	<b>17</b>	<b>83</b>

**Chanzo:-** Randama za Wizara husika 2017/2018

## 2.2.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2002, likiwa na Jukumu la kulinda amani na utulivu, kubaini, kupeleleza na kuzuia uhalifu, kuwakamata wahalifu na kuwaweka chini ya ulinzi, kulinda mali na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi hilo kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2017. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza majukumu yake likiwa na changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, na upungufu wa mafuta na vilainishi kwa ajili ya magari machache yaliyopo.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto hizo zinasababishwa na bajeti ndogo inayopangwa vilevile kutokutolewa kwa ukamilifu kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Jeshi hilo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Jeshi la Polisi lilitengewa Shilingi Bilioni 247,111,051,682/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Bilioni 5,000,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2017 Jeshi lilipokea Shilingi Bilioni 124,637,484,397/= sawa na asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na Shilingi Milioni 193,000,000/= za Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 3.9 tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutopatikana kwa fedha kwa ukamilifu kumeathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa katika kipindi hicho hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu nchini, upelelezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za Baharini na Maziwa Makuu.

## 2.2.3 Ajali za Barabarani

**Mheshimiwa Spika**, makosa yanayotokana na ukiukwaji wa

Sheria za usalama barabarani yameendelea kusababisha ajali za barabarani nchini. Kwa kipindi cha Oktoba - Disemba, 2017 jumla ya ajali 1428 ziliripotiwa ambapo kati ya hizo, ajali 562 zilisababisha vifo.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa vifo hivi ni pungufu ya ajali 91 zilizosababisha vifo ikilinganishwa na idadi ya vifo vya aina hiyo katika kipindi kama hicho Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Jeshi la Polisi hususan kitengo cha Usalama Barabarani kwa kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani ipasavyo. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali itekeleze ushauri uliotolewa na Kamati katika taarifa yake ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 kuhusu kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ili iguse maeneo sita yenye mapungufu ambayo yanachangia ajali za barabarani zinazosababisha vifo. Maeneo hayo ni:-

- i) Mwendokasi;
- ii) Uvaaji wa kofia ngumu;
- iii) Ufungaji wa mikanda;
- iv) Matumizi ya kilevi;
- v) Matumizi ya simu za mkononi; na
- vi) Matumizi ya vizuizi vya Watoto.

#### **2.2.4 Ulinzi na usalama wa Raia na mali zao**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa vipindi tofauti vya Mwezi Septemba, 2017 na Januari, 2018 kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Usalama wa Raia na mali zao. Taarifa hizo, pamoja na mambo mengine, zilibainisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa Raia na mali zao nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliridhishwa na juhudi za Serikali katika kushughulikia matukio mbalimbali ya uhalifu hususan matukio ya Kibiti, Mkuranga na Rufiji ambayo yalikusishwa

mauaji ya Viongozi mbalimbali, Askari Polisi na Raia. Nafurahi kutoa taarifa kuwa, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika maeneo hayo, hali ya usalama sasa ni shwari. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kiini cha mauaji hayo kinajulikana na kudhibitiwa ili mauaji ya aina hiyo yasijirudie tena nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada zinazofanywa na Jeshi la Polisi katika kudhibiti uhalifu nchini, Kamati ilibaini kuwa kumekuwana ucheleweshwaji wa kutoa taarifa rasmi kwa Umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu na yanayovuta hisia za Jamii kama vile matukio ya mauaji, kutekwa na kupotea kwa Viongozi na Wananchi mbalimbali, unyang'anyi wa kutumia silaha na makosa makubwa ya uhujumu uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Wakuu wa Wilaya wanawaweka mahabusu Wananchi na Watumishi wa Umma kinyume cha matakwa ya Kifungu cha 15 cha Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 1997. Ni wajibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na TAMISEMI kuendelea kuwaelimisha Wakuu wa Wilaya kuhusu matumizi sahihi ya Sheria hiyo ingawa kwa sasa vitendo hivyo vimepungua.

## **2.2.5 Udhhibiti wa Usalama wa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wabunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Mwezi Novemba, 2017 Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Udhhibiti wa Usalama wa Viongozi wakiwemo Wabunge. Kamati ilichambua na kujadili Taarifa hiyo ambapo ilibainika kuwa Viongozi wanaolindwa na Jeshi la Polisi kwa Mujibu wa Sheria ni wafuatao:-

- i) Viongozi Wakuu wa Nchi ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waziri Mkuu na Viongozi Wakuu Wastaafu;
- ii) Viongozi waandamizi wa Serikali ambao ni Mawaziri na Manaibu Mawaziri;

- iii) Wakuu wa Mikoa na Wilaya;na
- iv) Spika na Naibu Spika wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322, Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hupewa ulinzi wa jumla wanapokuwa Bungeni au kwenye safari zao za kikazi. Utaratibu huu unaliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge katika makazi yao wakiwa kwenye shughuli za Bunge na kwenye maeneo yao ya uwakilishi kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe.

### **2.2.6 Msongamano wa wafungwa katika Magereza**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Magereza kwa kipindi cha Januari - Septemba, 2017, ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ulionesha kuwa hali hii imeendelea kuchangiwa na:-

- i) Uchache wa magereza nchini ikilinganishwa na idadi ya wafungwa;
- ii) Utegemezi wa adhabu ya kifungo Gerezani na matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na huduma kwa Jamii;
- iii) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *parole*;
- iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu;
- v) Kasi ndogo ya kusikiliza mashauri yanayohusu mauaji na dawa za kulevya;na
- vi) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na msongamano wa wafungwa, Kamati ilibaini changamoto nyingine mbalimbali zinazolikabili Jeshi la Magereza katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i. Upungufu wa Watumishi takribani 11,395;
- ii. Ufinyu wa Bajeti na hivyo kulifanya Jeshi hilo kushindwa kujenga nyumba za Watumishi zinazolingana na mahitaji ya Jeshi, kushindwa kununua vitendea kazi kama vile magari na sare za Watumishi na wafungwa, kukarabati majengo ya Ofisi za Magereza, na kushindwa kupima maeneo ya Jeshi hivyo kusababisha migogoro ya ardhi na Jamii inayoizunguka kama vile katika magereza ya King'ang'a - Dodoma, Morogoro Mjini, Namajani- Mtwara na Mollo- Rukwa.

### 2.2.7 Utekelezaji wa majukumu ya Kikosi cha Zimamoto

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa Taarifa hii, Kamati ilibaini kuwa Serikali imeendelea kutolipa Jeshi la Zimamoto uzito unaostahili kwa kuzingatia majukumu ya Jeshi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Mei, 2017 Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kuhusu kutoa kwa ukamilifu Shilingi Bilioni 3.5 za Miradi ya Maendeleo ya Jeshi hilo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 2 ziliidhinishwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu yake uliokwama tangu Mwaka 2013, na Shilingi Bilioni 1.5 zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzimia moto. Hata hivyo, ilibainika kuwa, hadi kufikia Mwezi Juni, 2017, Serikali kupitia Hazina ilitoa Shilingi 117,045,000/= tu za Miradi ya Maendeleo licha ya kuwa katika Mwaka huo wa fedha Kikosi hicho kilikusanya Shilingi 31,725,254,500/=. Kutokutolewa kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Mifumo na juhudi za uokoaji na zimamoto.

**Mheshimiwa Spika**, mbali na changamoto ya upatikanaji wa fedha za maendeleo, Kikosi hicho kimeendelea kukabiliwa na uhaba wa dawa za kuzimia moto na uchakavu wa magari ya kuzimia moto na uokoaji jambo linalozorotesha utaratibu na juhudi za zimamoto na uokoaji.

### 2.2.8 Huduma za Wakimbizi Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Wakimbizi kwa kushirikiana na

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa Wakimbizi nchini kwa kuzingatia Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Wakimbizi ya Mwaka 2003 na Mikataba mbalimbali ambayo nchi yetu imeridhia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya kuwahudumia wakimbizi kwa kipindi cha Januari- Septemba, 2017. Taarifa hiyo ilionesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 11 zilizopendekezwa kutekeleza Mpango jumuishi wa Umoja wa Mataifa ujulikanao kama '*Comprehensive Refugee Response Framework*'. Mpango huu utawasaidia wakimbizi pamoja na Jamii wenyeji katika maeneo ambayo wakimbizi wanahifadhiwa kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya Umoja wa Mataifa, Kamati ilibaini kuwa bado upo umuhimu wa Serikali yetu kuendelea kutafuta suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi hapa nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu za kudumu katika nchi zenye machafuko, kuwahamishia wakimbizi katika nchi ya tatu, kuwapa uraia na kuwatawanya katika maeneo mbalimbali nchini.

#### **2.2.9 Idara ya Uhamiaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni, 2017, Idara ya Uhamiaji ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa huduma ya pasipoti na hati za dharura za safari kwa watazania wanaosafiri nje ya nchi, na ununuzi wa mafuta ya magari kwa ajili ya doria na matumizi mengine ya Idara.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Idara ya Uhamiaji kwa kipindi tajwa, Kamati ilibaini kuwa uhaba wa fedha uliathiri utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa ikiwemo Idara kushindwa kufanya misako na doria ya mara kwa mara kwa kutokua na vitendea kazi kama vile magari na uhaba wa mafuta.

Aidha, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Idara inakabiliwa na madeni makubwa ya wazabuni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu kuanzia Mwaka 2013/2014 hadi 2016/2017 yanayofikia kiasi cha Shilingi Bilioni 10,291,374,513.46. Jambo hili limesababisha Idara kushindwa kupata huduma kwa wakati ikiwemo upatikanaji wa vitabu vya Pasipoti na malighafi zake.

### **2.2.10 Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeendelea kuishauri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuharakisha Mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy) tangu Kamati hii ilipoanza kutekeleza majukumu yake Mwezi Januari, 2016. Ushauri huu ni mwendelezo wa jitihada za iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika Bunge la Tisa na Bunge la Kumi katika kuisisitiza Serikali kuona umuhimu wa kuwa na Sera ya Ulinzi.

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vya Mwezi Oktoba, 2017, Kamati ilielezwa kuwa mchakato huo bado unaendelea. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mchakato wa Sera hiyo bado haujakamilika. Jambo hili linaathiri utekelezaji wa masuala mengine ya msingi yanayotegemea uwepo wa Sera hiyo kama vile maboresho ya fidia kwa Askari wanaoumia au kufariki wakiwa kazini.

### **2.2.11 Alama za Mipaka ya Nchi (Beacons)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Mipaka ya Nchi Mwezi Oktoba, 2017, ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa alama za Mipaka (Beacons), na uwepo wa makazi na shughuli za Kilimo na Ufugaji katika maeneo ya Mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na imekuwa ikiripotiwa Bungeni tangu Bunge la Nane. Ni wazi kuwa tatizo hili lisiposhughulikiwa litahatarisha usalama wa Taifa.



### 2.2.12 Barabara za Mipakani

**Mheshimiwa Spika**, ubovu wa barabara za mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati zote. Mwezi Disemba, 2013, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ya Bunge la Kumi iliishauri Serikali kuhusu changamoto hiyo, Nanukuu:

‘Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba suala la ujenzi na ukarabati wa barabara za usalama mipakani linawekewa mkakati maalumu wa kitaifa. Moja ya mikakati hiyo iwe ni kuziweka barabara hizi chini ya TANROADS, na tenda za matengenezo zitolewe kwa vitengo vya uhandisi vya Jeshi na JKT kwa vile wana wataalamu na zana za kutengeneza barabara’<sup>1</sup>

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, hadi sasa ikiwa ni Miaka Mitano (5) tangu ushauri huo utolewe jambo hilo bado halijatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha.

### 2.2.13 Shirika la SUMA JKT

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa Mwaka 1982 kwa Sheria ya Makampuni namba 23 ya Mwaka 1974. Jukumu kuu la Shirika hili ni kuchochea shughuli za uzalishaji mali ili kusaidia gharama za malezi ya Vijana wanaopitia JKT.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa ya Utendaji wa Shirika la SUMA JKT mwezi Oktoba, 2017, ilibaini kuwa Kampuni ya SUMAJKT GUARD inakabiliwa na changamoto ya muda mrefu ya madeni kutoka kwa washitiri ambapo gharama kubwa hutumika katika kufuatilia madeni hayo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, mradi wa matrekta na Zana za Kilimo (Agrimachinery) una changamoto ya urejeshwaji wa madeni kutoka kwa Wakulima, Halmashauri za Wilaya na Viongozi waliokopa matrekta. Hadi taarifa hiyo ilipokuwa inawasilishwa mbele ya Kamati, madeni hayo yalikuwa takribani Shilingi Bilioni 40.

---

<sup>1</sup> Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa kuanzia Machi hadi Novemba, 2013

**Mheshimiwa Spika**, madeni haya kwa Mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri utendaji wa Shirika hilo hususan katika kutimiza jukumu lake la kuchochea shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kusaidia gharama za malezi ya Vijana wanaopita JKT.

#### **2.2.14 Migogoro ya Ardhi katika JKT**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikijadili taarifa ya utekelezaji wa JKT ilibaini kuwepo kwa migogoro ya ardhi katika baadhi ya Vikosi vya Jeshi hilo. Migogoro hiyo inasababishwa na kuwepo kwa wavamizi wa ardhi ya Jeshi ambao hawataki kuhama katika maeneo hayo na Wananchi kutokulipwa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa wakati uvamizi katika maeneo ya Jeshi unachangiwa na ongezeko la idadi ya watu na mahitaji makubwa ya ardhi, Wananchi kutolipwa fidia kunasababishwa na kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya suala hilo.

#### **2.2.15 Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria kwa Vijana wanaohitimu Elimu ya Sekondari yalirejeshwa Mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na mihula ya kumaliza Kidato cha Sita kutoendana na muda wa Vijana kujiunga na mafunzo ya JKT, Vijana hao hulazimika kupata mafunzo hayo kwa miezi Mitatu tu badala ya Mwaka Mmoja. Kamati inaona kuwa muda huo ni mchache kuwajengea moyo wa uzalendo Vijana vilevile kuwaandaa kuwa Jeshi la Akiba.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na nia njema ya kurudisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, Kamati imebaini kuwa bado Serikali haijalipa kipaumbele Jeshi hilo katika kuboresha miundombinu yake. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, JKT lilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni 8 ikiwa ni fedha za maendeleo kwa ajili ya shughuli za ujenzi na ukarabati vikosini. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2017 fedha iliyokuwa imetolewa ni Shilingi Bilioni 1 sawa na asilimia 12.5 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Aidha, katika Mwaka wa Fedha

2017/2018, JKT limetengewa Shilingi Billioni 6 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo hadi kufikia Mwezi Januari 2018, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

### **2.2.16 Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Taifa cha Ulinzi (National Defence College) kilianza rasmi Mwaka 2012. Chuo hiki maalum kimejikita katika kutoa mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa Maafisa Waandamizi kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Vyombo vya Usalama, Watumishi wa juu wa Serikali pamoja na Maafisa Waandamizi kutoka majeshi ya nchi rafiki za Afrika na nje ya Afrika. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea washiriki wa kozi maarifa katika Nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijeshi, kisayansi, mahusiano ya kimataifa na kuwaongeza weledi wa uongozi kwa kiwango cha kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya NDC, ilibaini kuwa, uchache wa vyumba vya kulala, vyumba vya kuendeshea Semina na majadiliano ni changamoto inayokikabili Chuo. Changamoto hii imesababisha Chuo kuchukua washiriki wachache tofauti na idadi iliyokusudiwa na vilevile kushindwa kuendesha Kozi ndefu na fupi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kutatua changamoto hiyo ambapo maandalizi yote ya ujenzi wa jengo jipya la Chuo (awamu ya pili) yameshakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilibaini upatikanaji wa washiriki hususan kutoka katika Wizara mbalimbali ni changamoto nyingine ya Chuo hicho. Jambo hili linasababishwa na baadhi ya Wizara kutopeleka washiriki katika mafunzo hayo muhimu kwa Maafisa Waandamizi kwa kigezo cha uhaba wa fedha. Kamati inaamini mafunzo haya ni muhimu hivyo Wizara zote zinatakiwa kupeleka Maafisa Waandamizi kama ambavyo Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimekuwa vikifanya.

**Mheshimiwa Spika**, ipo haja ya Serikali kuandaa utaratibu wa kuwafanya Maafisa waandamizi wa Wizara zote kushiriki

Mafunzo hayo muhimu. Aidha, upo umuhimu wa Wabunge kupewa mafunzo ya usalama na stratejia yanayotolewa na Chuo hicho.

### **2.2.17 Utekelezaji wa Shughuli za Mpango wa Tathmini ya Utawala Bora (APRM Tanzania)**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni miongoni mwa nchi 36 kati ya 54 za Umoja wa Afrika zilizojiunga na Mpango huu wenye lengo la kuzisaidia Serikali za Afrika, ikiwemo Tanzania, kuimarisha Utawala Bora kwa kuwashirikisha Wananchi kubaini changamoto za kufanyiwa kazi na mambo mazuri ya kuigwa na kuendelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopokea taarifa ya utendaji ya APRM Tanzania, ilielezwa kuwa changamoto kubwa inayoikabili Taasisi hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake ni mgao mdogo wa fedha za Bajeti zinazopangwa. Hali hiyo imesababisha Taasisi hiyo, pamoja na mambo mengine, kushindwa kutekeleza kikamilifu Mkakati wa mawasiliano unaolenga kuendelea kuhamasisha Umma kuhusu APRM na hivyo kutofahamika vema kwa Wananchi walio wengi.

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa nguzo muhimu ya Mpango wa APRM ni ushirikishwaji mpana wa Wananchi ili kupata maoni kutoka kwa Wadau wote muhimu.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati, kwa kipindi cha miaka takribani mitano mfululizo, imekuwa ikiishauri Serikali kuipatia APRM Fungu lake la kibajeti, ushauri ambao haujatekelezwa.

### **2.2.18 Utendaji wa Chuo cha Diplomasia**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam kilianzishwa mwaka 1978 kwa ushirikiano wa nchi mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji. Tangu kuanzishwa kwake, Chuo hiki kimeendelea kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika Nyanja

za mahusiano ya Kimataifa, Diplomasia, Diplomasia ya Uchumi, Itifaki, Lugha za Kigeni na nyinginezo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takribani Miaka 36 Chuo hiki kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kuacha kabisa kuchangia bajeti na kushiriki katika shughuli zote za uendeshaji wake Mwaka 1982. Suala hili limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Chuo na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo imeendelea kubeba jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za Chuo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto iliyoelezwa hapo juu, Kamati ilibaini kuwa Chuo kimekuwa na changamoto nyingine ya kutimiza na kutekeleza viwango vilivyowekwa na NACTE kutokana na ukosefu wa pesa za kutosha. Viwango hivyo ni pamoja na:-

- i) Kuwa na wataalamu wenye vigezo vinavyotambulika;
- ii) Kuboresha majengo na Miundombinu ya Kitaalamu;
- iii) Matumizi ya teknolojia katika Taaluma na Utawala.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa changamoto hii isipopewa uzito unaostahili inaweza kusababisha Chuo hicho kufutiwa usajili wa NACTE.

#### **2.2.19 Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)**

**Mheshimiwa Spika**, Dhana ya Diplomasia ya Mikutano (Conference Diplomacy) inatambua Vituo vya Mikutano vya Kimataifa kutumika kutangaza nchi zao Kimataifa kwa ajili ya ujio wa wageni katika vituo hivyo. Kwa sababu hiyo, nchi nyingi mbalimbali zimekuwa na utaratibu wa kuwekeza kwenye vituo vya Mikutano ya Kimatifa kwa ajili ya Utalii wa Mikutano. Kwa upande wa Tanzania, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kimekuwa sababu ya vivutio vya Utalii katika mzunguko wa Kaskazini kupata Watalii wengi.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kilianza rasmi Mwaka 1978 kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwaka 1977. Katika kutekeleza shughuli zake, Kituo kinachukua sura ya kuitangaza Tanzania katika Utalii wa Mikutano na matukio (business tourism) na hivyo kuchangia katika pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mchango wake muhimu katika Sekta ya Utalii, Kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- i) Matumizi ya majengo ambayo hayakujengwa rasmi kwa shughuli za mikutano;
- ii) Ukiritimba katika kupata Hati Miliki za baadhi ya viwanja vyake;
- iii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kwa ajili ya kuitangaza nchi, kuvutia Mikutano na maonesho ya Kimataifa kufanyika nchini; na
- iv) Utata wa umiliki wa Kiwanja Na. 45 eneo la corridor 1 kuwa cha ESAMI au AICC

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza wazo la AICC la kuwa na tawi lake katika Makao Makuu ya Nchi Mjini Dodoma. Ni vema Wizara ikafuatilia kwa karibu maombi ya kupatiwa Kiwanja cha kujenga Kituo cha kisasa cha Mikutano cha Kimatifa kitakachokuwa na eneo la kutosha kwa ajili Mikutano, maonesho na Hoteli za kisasa. Aidha, kwa siku za usoni, Kituo kiwe na mpango wa kufungua tawi lake Zanzibar, ambako kuna fursa nyingi za kitalii.

#### **2.2.20 Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere kinasimamiwa na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) tangu Aprili, 2014. Dhima ya

kituo hiki ni kukuza na kutoa huduma bora za Utalii wa Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya kukuza maendeleo ya Taifa kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hiki kimekuwa na mafanikio mbalimbali tangu kilipoanzishwa. Moja ya mafanikio hayo ni kuongezeka kwa mapato<sup>2</sup> kutokana na shughuli za mikutano ambazo ndio hasa zinazotangaza Kituo, Jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla.

**Mheshimwa Spika**, pamoja na mafanikio ya Kituo hicho, Kamati ilibaini kuwa JNIC inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i) Kutokuwepo kwa eneo la maonesho;
- ii) Kutokuwepo kwa eneo la chakula kwa wageni wa mikutano;
- iii) Kutokuwa na Hati Miliki ya Kiwanja chake;na
- iv) Ubovu wa miundombinu ya maji, majitaka, umeme na viyoyozi.

**Mheshimiwa Spika**, ni vema Serikali ikashughulikia changamoto hizo ili Kituo hicho kiweze kutoa huduma bora zaidi za Utalii wa Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Serikali iwe makini inapopewa misaada inayohusu ujenzi wa majengo kwa kuhakikisha kuwa majengo yanayojengwa yanakidhi vigezo.

#### **2.2.21 Balozi za Tanzania kutopata fedha kwa wakati**

**Mheshimiwa Spika**, Balozi zetu zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya kutopata fedha kwa wakati jambo ambalo linaathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo. Licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii mara kwa mara kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo badala ya kupeleka Wizarani, bado ushauri huo haujatekelezwa.

---

<sup>2</sup>Mapato yameongezeka kutoka Sh. 2,023,350 Mwaka 2013/2014 hadi kufikia 2,738,009 Mwaka 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya ziara katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden na Msumbiji ilibaini kuwa Balozi hizo zimeendelea kupelekewa fedha kutoka Wizarani na si Hazina, jambo ambalo linasababisha fedha hizo kuchelewa kutumwa. Hali hii imeathiri utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo ikiwa ni pamoja na gharama za utekelezaji wa mradi uliopo Maputo kuongezeka hadi kufikia USD 3,056,839.15 kutoka gharama za awali za USD 2,107,028.89 wakati Mkataba wa utekelezaji uliposainiwa Mwaka 2012.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa Serikali bado haijaupa ushauri huo uzito unaostahili kwani upatikanaji wa fedha katika Balozi nyingi umeendelea kuwa katika mtiririko usio wa kuridhisha.

#### **2.2.22 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania**

Mheshimiwa Spika, majengo ya baadhi ya Balozi zetu yameendelea kuwa chakavu kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Kamati hii ilipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ukarabati wa majengo katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden Mwezi Mei, 2017, ilishuhudia uchakavu uliokithiri wa majengo ya Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi wa Ubalozi huo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, majengo hayo hayajafanyiwa ukarabati kwa takribani Miaka Tisa.

**Mheshimiwa Spika**, uchakavu wa majengo ya Balozi unasababisha athari mbalimbali kwa Taifa letu. Athari hizo ni pamoja na:-

- i) Kuliondolea Taifa heshima na kuharibu taswira ya Tanzania nje ya nchi;
- ii) Serikali kulipa gharama kubwa kwa ajili ya Kodi ya Pango ya nyumba za makazi kwa Mabalozizi na Watumishi wa Ubalozizi; na
- iii) Kuondolewa kwa kinga ya ubalozizi kwenye majengo hayo.



### **2.2.23 Hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya hali ya ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki ilibaini kuwa, pamoja na faida zinazopatiwa ndani ya Jumuiya za Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki, zipo changamoto mbalimbali ambazo zisiposhughulikiwa zinaweza kuathiri hali ya Ushirikiano na Mtangamano uliopo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Kasi Ndogo ya kuridhia Itifaki mbalimbali za SADC kwa nchi Wanachama. Kati ya Itifaki 31 za SADC, Tanzania imesaini Itifaki 28 na kuridhia 25;

ii. Migogoro ya kisiasa ndani ya nchi Wanachama wa SADC kama vile Lesotho, Madagascar na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo; na

iii. Kuwepo na vikwazo mbalimbali visivyo vya kiushuru miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikwazo hivyo vinadhooifisha ufanyaji wa biashara baina ya nchi na nchi.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kikao hicho Kamati ilihoji na kubaini kuwa bado Serikali haina Sera mahsusi inayotoa mwongozo kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki, licha ya kwamba suala hili limekuwa likishauriwa tangu Bunge la Tisa na Serikali kutoa maelezo kuwa mchakato wa uandaaji wa Sera hiyo unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa jambo hili halijapewa uzito unaostahili na Serikali kwani Tanzania imekuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa takribani Miaka Kumi na Nane na mpaka sasa hakuna Sera hiyo muhimu. Ni lazima Serikali itambue kuwa ipo hatari ya kutekeleza jambo lisilokuwa na mwongozo bora wa kisera.

### **2.2.24 Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutekeleza Sera ya Mambo

ya Nje (2001) inayoweka msisitizo katika kukuza uchumi wa nchi kupitia Diplomasia ya Uchumi iliyo endelevu. Hata hivyo Sera hiyo tangu iundwe mwaka 2001, imeendelea kutumika bila kufanyiwa marekebisho yanayozingatia mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipowasilisha taarifa yake ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017, ilishauri Mchakato wa marekebisho wa Sera hiyo uharakishwe ili iendane na mazingira ya sasa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kasi ya mchakato wa marekebisho ya Sera hiyo bado hairidhishi.

#### **2.2.25 Meli za Nchi za Nje zilizopewa Usajili Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Siku za karibuni imejitokeza changamoto ya baadhi ya Meli zilizopewa usajili Tanzania kukamatwa zikifanya vitendo vya kihalifu ikiwemo kubeba madawa ya kulevya na vifaa vya kutengenezea silaha kali za kivita. Jambo hilo limeitia aibu nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kama ilivyoahidi Bungeni tarehe 02/05/2017 na kusawazisha kasoro za msingi zilizosababisha jambo hili ili lisitokee tena.

#### **2.2.26 Kuwasilisha Maoni kuhusu Azimio la Bunge**

**Mheshimiwa Spika**, katika Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Nane wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliwasilisha Bungeni maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Protocol on Peace and Security). Lengo la Itifaki hii ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake, ilibaini kuwa Itifaki hiyo ilisainiwa na nchi Wanachama tarehe 15 Februari, 2013. Hivyo, Itifaki hii ilichukua Miaka Minne

hadi ilipoletwa Bunge kwa ajili ya kuridhiwa licha ya kuonekana kuwa ina manufaa makubwa katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Ni vyema Serikali ikashughulikia dosari zote za aina hii kwa kuwasilisha Itifaki zote zilizosainiwa ambazo zinahitaji kuridhiwa na Bunge ili ziridhiwe na utekelezaji wake uanze mara moja kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Sambamba na hilo, Kamati inaisisitiza Serikali kuzingatia maoni na ushauri ulitolewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia Azimio hilo.

### **2.2.27 Taarifa za Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge**

**Mheshimiwa Spika**, uwakilishi wa Bunge katika Mabunge na Vyama mbalimbali vya Kibunge ni njia mojawapo ya kutekeleza Diplomasia ya Kibunge katika kuongeza ushirikiano miongoni mwa nchi mbalimbali, kuboresha uchambuzi wa taarifa za Serikali na kuwawakilisha vema Wananchi wa nchi Wanachama kwa kutetea maslahi yao Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia dhana ya Diplomasia ya Kibunge, Bunge lako ni miongoni mwa Mabunge mengi Duniani yanayoheshimu na kuthamini nafasi yake katika kuwezesha ushawishi mzuri wa mambo ambayo ni ajenda ulimwenguni vilevile kuchochea kasi ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo Mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge ni dhahiri, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapaswa kuendelea na utaratibu huu kwa maslahi ya Taifa na Wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wetu kama ifuatavyo:-

i) **ACP – EU**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge la pamoja la nchi za ACP (African Carribean Pacific) na Umoja wa Ulaya (European Union) ni matokeo ya makubaliano ya Cotonue (The ACP-EU Patnership Agreement) ambapo nchi 78 za ACP isipokuwa Cuba ziliweka makubaliano ya kushirikiana na nchi 28 za Umoja wa Ulaya katika masuala ya Kisiasa, Kijamii, Kiuchumi, fedha, biashara na mazingira. Makubaliano hayo yalisainiwa tarehe 23 Juni, 2000 Jijini Cotonue Benin.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kujadili taarifa ya wawakilishi hao, Kamati ilibaini kuwa ushiriki wa Bunge letu kwenye ACP/ EU unapaswa kuendelezwa kwa kuzingatia kuwa jukwaa hili ni sehemu pekee ambayo sauti ya pamoja kwa nchi zinazoendelea inaweza kusikika.

**Mheshimiwa Spika**, naomba ifahamike kuwa Mkataba wa Ushirikiano kati ya Nchi za ACP na Umoja wa Ulaya unatarajwa kumalizika mwezi Februari 2020. Kamati inaamini kuwa kumalizika kwa Mkataba huu ni fursa kwa nchi za ACP kuhakikisha kuwa makubaliano mapya yanalenga kunufaisha pande zote za ushirikiano na si Umoja wa Ulaya tu kama ilivyo sasa.

ii) **SADC PF**

**Mheshimiwa Spika**, Jukwaa hili ka Kibunge lilianzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, na kuwa moja ya Taasisi za SADC kwa mujibu wa kifungu cha 9 (2) cha Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika (SADC).

**Mheshimiwa Spika**, Jukwaa hili lilianzishwa kwa dhumuni la kupata sehemu ambayo Mabunge na Wabunge wa nchi Wananchama wanaweza kubadilishana uzoefu na mawazo chanya ili kuimarisha mshikamano wa nchi husika Kisiasa, Kijamii na Kiuchumi. Aidha, kwa siku za usoni, inategemewa Jukwaa hili kuwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika kama ilivyo kwa Kanda nyinginezo ambazo tayari zina Mabunge yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofuatilia uwakilishi wa Bunge letu katika SADC PF ilibaini kuwa Bunge letu linadaiwa Randi 2,552,852/= ikiwa ni mchango wa Uanachama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati inaona kuwa deni hili lisipolipwa mapema linaweza kuathiri taswira ya Bunge letu katika Jukwaa hilo.

iii) **Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola- CPA**  
**Mheshimiwa Spika**, CPA ni mojawapo ya Vyama vya Kibunge vya muda mrefu. Chama hiki kilianzishwa Mwaka 1911 nchini Uingereza kwa ajili ya kuunganisha Mabunge katika nchi ambazo zilikuwa chini ya Himaya ya Uingereza. Lengo la Chama hiki, pamoja na mambo mengine, ni kuwasaidia Wanachama kujenga Mifumo ya Utawala wa Kidemokrasia na Utawala wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ndio Makao Makuu ya Chama hiki kwa upande wa Afrika, na kwa mujibu wa Katiba ya CPA Tawi la Afrika, Mtendaji Mkuu wa Chama hiki kwa upande wa Afrika ni Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili limeiweka Tanzania, hususan Bunge lako Tukufu kuwa na nafasi ya kipekee katika CPA na inapaswa kutunzwa na kuheshimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia na kujadili taarifa zote za wawakilishi hao, Kamati ilibaini kuwa kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya kushiriki Mikutano kumeendelea kuwa changamoto iliyoathiri fursa ya Wawakilishi kushiriki ipasavyo katika masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika Mikutano hiyo.

### 2.3 Matokeo ya Semina zilizofanyika

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilishiriki na kuongoza Semina tofauti Tatu katika kipindi cha Septemba, Oktoba na Novemba, 2017. Semina hizo zilihusu Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa; Dhana na utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau; na Uchambuzi wa Miswada ya Sheria na udhibiti wa Sheria Ndogo katika Bunge la Tanzania.

Katika Semina hizo, pamoja na mambo mengine, Wajumbe walijadili hatua na mbinu za kuchambua Miswada ya Sheria; hatua za utungaji wa Sheria Ndogo na nafasi ya Bunge katika uhibitaji wake; hatua za utayarishaji wa Mikataba ya Kimataifa; na aina za utekelezaji wa dhana na namna ya kutekeleza utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau.

**Mheshimiwa Spika**, katika Semina hizo, changamoto mbalimbali zilibainika kwenye baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

**a) Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa**

i) Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa kuchukua muda mrefu kuridhiwa jambo ambalo linachelewesha Nchi/Wananchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye Mikataba hiyo;

ii) Sheria za nchi kutoanishwa na Mikataba au Itifaki za Kimataifa zilizoridhiwa jambo linalosababisha mkanganyiko kati ya Sheria ya Kimataifa (International Law) na Mfumo wa Sheria za Nchi; na

iii) Wawakilishi wa Bunge kutokutana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kabla ya kuhudhuria Mikutano ya Vyama vya Kibunge jambo ambalo linasababisha wawakilishi hao kutokuwa na msimamo wa pamoja na Bunge katika masuala yanayoenda kujadiliwa katika mikutano hiyo.

**b) Dhana na Utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau**

i) Hisia kwamba maoni ya Wadau yanakusanywa kwa jambo ambalo uamuzi wake unajulikana na kwamba maoni yatakayotolewa hayawezi kuathiri uamuzi huo jambo ambalo linasababisha utaratibu huo kutohaminiwa na baadhi ya Wananchi; na

ii) Tofauti ya kiuielewa miongoni mwa Wataalamu na Wananchi wengine (expert-citizen divide).

**c) Udhhibiti wa Sheria Ndogo**

i) Upungufu wa Wataalam wa uandishi wa Sheria (Legislative Drafters) katika Serikali na vyombo vyake jambo ambalo lina sababisha Sheria Ndogo nyingi kuwa na dosari. Wataalamu wanaotegemewa kuboresha maudhui ya Sheria Ndogo ni wale waliopo kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria ambao nao ni wachache ikilinganishwa na majukumu waliyonayo; na

ii) Serikali kuchelewa kuchapisha Sheria Ndogo zilizofanyiwa marekebisho jambo linalosababisha Sheria Ndogo zenye dosari kuendelea kutumika na hivyo kuleta athari kwa watumiaji.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0**

**MAONI NA MAPENDEKEZO**

**3.1 Maoni**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

**a) Masuala ya Jumla**

Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kuna athiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii.

**b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

(i) Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali za kibajeti zinazoathiri utendaji wa Jeshi hilo katika kusimamia usalama wa Raia na mali zao;

(ii) Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ina mapungufu yanayochangia uwepo wa tatizo sugu la ajali za barabarani;

(iii) Ucheleweshwaji wa kutoa taarifa rasmi kwa Umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu na yanayovuta hisia za Jamii kama vile matukio ya mauaji, kutekwa na kupotea kwa Viongozi na Wananchi mbalimbali kunasababisha Wananchi kutokujua hatua za upelelezi zilizofikiwa;

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu rasmi wa ulinzi kwa Wabunge katika makazi yao kunahatarisha usalama wao hasa kwa kuzingatia kuwa, baadhi ya majukumu yao katika kuisimamia Serikali yanagusa maslahi ya Watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;

(v) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole* na matumizi haffu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

(vi) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo;

(vii) Kutokutolewa kwa fedha za miradi kwa Jeshi la Zimamoto kwa kipindi cha Miaka Miwili mfululizo kunaathiri utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na Mifumo na juhudi za uokoaji na zimamoto;

(viii) Kutokuwa na suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi nchini kunaendelea kuhatarisha usalama katika maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguuka; na

(ix) Madeni makubwa ya Wazabuni kwa Idara ya Uhamiaji yanasababisha Idara hiyo kushindwa kupata na kutoa Hati za Kusafiria (Passports) kwa wakati.

**c) Wizara ya Ulinzi na JKT**

(i) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;



- (ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (beacons) kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;
- (iii) Ubovu wa barabara za mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi;
- (iv) Madeni kwa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa Shirika hilo;
- (v) Wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya Wananchi na vikosi vya Jeshi hilo;
- (vi) Muda wa miezi Mitatu kwa ajili ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria haukidhi katika kuwajengea moyo wa uzalendo vijana wala kuwaandaa kuwa Jeshi la akiba; na
- (vii) Baadhi ya Wizara kutokutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya Maafisa waandamizi katika Chuo cha Ulinzi kunasababisha Maafisa hao kutohudhuria Kozi hizo muhimu za usalama na uongozi.

**d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

- (i) APRM Tanzania kutokuwa na Fungu lake la Kibajeti kunaathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti;
- (ii) Kutokutoa kipaumbele katika kushughulikia changamoto zinazokikabili Chuo cha Diplomasia kunahatarisha Chuo hicho kufutiwa Usajili wa NACTE;
- (iii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kunaikoshesha nchi fursa ya kuvutia Mikutano na maonesho ya Kimataifa mengi zaidi kufanyika hapa nchini;
- (iv) AICC kutokuwa na majengo yakutosha kwa ajili ya

shughuli za Mikutano unakiondolea Kituo hicho ufanisi kwa kushindwa kushindana katika soko;

(v) Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo;

(vi) Kutokarabati majengo ya Balozi zetu si tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia kunaathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi;

(vii) Kukosekana kwa Sera ya Taifa kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki ni jambo la hatari katika mustakabali wa nchi;

(viii) Sera ya Mambo ya Nje ni ya muda mrefu na mchakato wa kuifanyia marekebisho unachukua muda mrefu kukamilika;

(ix) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa na Itifaki iliyosainiwa kunachelewesha nchi/Wananchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye mikataba hiyo; na

(x) Kutooanisha Sheria za Nchi na Mikataba au Itifaki za Kimataifa zilizoridhiwa kunasababisha mkanganyiko kati ya Sheria za Kimataifa na Mfumo wa Sheria za nchi.

#### **e) Wawakilishi wa Vyama vya Kibunge**

(i) Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge kutoshiriki kikamilifu Mikutano ya Vyama hivyo kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu ya Diplomasia ya Kibunge;

(ii) Wawakilishi wa Bunge kutokutana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kabla ya kuhudhuria Mikutano ya Vyama vya Kibunge kunaweza

kusabisha wawakilishi hao kutokuwa na msimamo wa pamoja na Bunge katika masuala yanayoenda kujadiliwa katika mikutano hiyo.

## **3.2 Mapendekezo**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza maoni, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

### **3.2.1 Kutokutolewa kwa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Kwa kuwa** fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hazikutolewa kwa ukamilifu, jambo ambalo lilikwamisha utekelezaji wake,

**Na kwa kuwa** kutokutekelezwa kwake kumesababisha hasara kutokana na madeni ya kimkataba na riba, na kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi,

**Kwa hiyo basi**, Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma yake kwa miradi hiyo.

### **3.2.2 Jeshi la Polisi kukabiliana na Uhalifu**

**Kwa kuwa** bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya mafuta, magari, operesheni mbalimbali na vitendea kazi,

**Na kwa kuwa** ufinyu huo wa bajeti unaathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu, upelelezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za baharini na Maziwa Makuu,

**Kwa hiyo basi**, Serikali iongeze Bajeti ya Jeshi la Polisi na kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili Jeshi hilo liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Aidha, Mikoa ambayo takwimu zinaonesha kiwango cha uhalifu kipo juu, ipewe kipaumbele.

### 3.2.3 Hali ya ulinzi na usalama wa Raia na mali zao

**Kwa kuwa** matukio yanayohatarisha hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao yamekuwa yakijirudia na hivyo kujenga hofu miongoni mwa Wananchi;

**Na kwa kuwa**, taarifa za hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio hayo zimekuwa hazitolewi mara kwa mara kwa Umma na hivyo kusababisha wananchi kutokufahamu hatua zilizofikiwa;

**Kwa hiyo basi**, Jeshi la Polisi liwe na utaratibu mahsusi wa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu ambayo yamevuta hisia za Jamii kama vile mauaji na kupotea kwa Wananchi mbalimbali.

### 3.2.4 Ulinzi na Usalama wa Wabunge

**Kwa kuwa**, hakuna Sheria wala Kanuni inayoelekeza Wabunge kupewa ulinzi katika makazi yao na hivyo kuliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe;

**Na kwa kuwa**, kazi za Wabunge katika kuisimamia Serikali zinagusa maslahi ya Watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;

**Kwa hiyo basi**, Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ifanyiwe Marekebisho ili:-

i) Kuweka sharti kwa Wabunge kupatiwa ulinzi hususan katika makazi yao wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kibunge Mjini Dodoma na katika maeneo yao ya uwakilishi; na

ii) Kuweka utaratibu wa kutoa namba maalum za usajili wa magari ya Wabunge.

Aidha, Serikali iboreshe na kuimarisha ulinzi katika Maeneo ya Maegesho ya Magari Bungeni.

### **3.2.5 Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani**

**Kwa kuwa** tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza nchini limeendelea kuwa sugu kutokana na:-

i) Matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na huduma kwa Jamii;

ii) Mahabusu kutokupelekwa Mahakamani kwa muda uliopangwa;

iii) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa Parole;

iv) Kasi ndogo ya kusikiliza mashauri yanayohusu mauaji na dawa za kulevyu; na

v) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa;

**Na kwa kuwa** hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu vilevile kuiongozea Serikali gharama za kuwatunza;

**Kwa hiyo basi**, Serikali:-

(i) Itekeleze Sheria inayowataka wahalifu wenye makosa madogo kupewa adhabu mbadala kama vile vifungo vya nje na huduma kwa jamii;

(ii) Izingatie kuwapeleka Mahabusu mahakamani kwa tarehe walizopangiwa;

(iii) Itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole*;

(iv) Ihakikishe kuwa Kamati za Kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi kutolewa kwa wakati;

(v) Itolee maamuzi suala la wafungwa waliohukumwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

### **3.2.6 Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi**

**Kwa kuwa** utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu unataka fedha hizo zipitishwe katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,

**Na kwa kuwa** utaratibu huo umebainika kuwa na urasimu usio wa lazima na hivyo kuchelewesha kutuma fedha kwa mtiririko unaotakiwa,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka fedha katika Balozi moja kwa moja bila kupitisha Wizarani kama ilivyo kwa Halmashauri zote nchini ambapo fedha hutumwa moja kwa moja bia kupitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

### **3.2.7 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania**

**Kwa kuwa** majengo mengi ya Balozi zetu nje ya nchi ni chakavu sana,

**Na kwa kuwa** kutokarabati majengo hayo kumeendelea kuiongezea gharama Serikali kwani baadhi ya Balozi zinalazimika kukodi majengo mengine mbadala,

**Kwa hiyo basi**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali itoe fedha za ukarabati wa majengo ya Balozi kama zilivyo idhinishwa na Bunge kwa kuanza na Balozi ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya zaidi.

### **3.2.8 Uendeshaji wa Chuo cha Diplomasia**

**Kwa kuwa** kwa takribani Miaka 36, Chuo cha Diplomasia

kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kujitoa katika kuchangia bajeti na kushiriki katika shughuli zote za uendeshaji,

**Na kwa kuwa** Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imefanya jitihada mbalimbali za kuwasiliana na Serikali ya Msumbiji ili ishiriki kikamilifu katika uendeshaji wa Chuo hicho bila mafanikio,

**Kwa hiyo basi**, Serikali iisitize Tume ya Pamoja ya Ushirikiano yaani *Joint Permanent Commission* ambayo ndiyo yenye dhamana ya kushughulikia tofauti za makubaliano ya uundwaji wa Chuo hicho, kulishughulikia suala hilo kikamilifu kufikia Mwezi Mei, 2018 na hatimaye kuweka wazi kwa mujibu wa Sheria, kwamba Chuo hicho sasa kimilikiwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### **3.2.9 Uwakilishi katika Vyama vya Kibunge**

**Kwa kuwa** Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Mabunge na Vyama mbalimbali vya Kibunge wameshindwa kushiriki kikamilifu Mikutano ya Mabunge na Vyama hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti;

**Na kwa kuwa** kutoshiriki vikao hivyo kunaweza kuleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine na Vyama vya Kibunge kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Ofisi ya Bunge fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwawezesha Wajumbe wa Vyama vya Kibunge kushiriki Mikutano husika kama ilivyopangwa kwa mujibu wa Ratiba.

### **3.2.10 Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki**

**Kwa kuwa** tangu Mwaka 1999 Tanzania ilipojiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki haijawahi kuwa na Sera maalum kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki,

**Na kwa kuwa** kutokuwa na Sera hiyo kunaifanya Serikali kutekeleza masuala mbalimbali ya Jumuiya hiyo bila ya kuwa na mwongozo wa Kisera jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa Taifa;

**Kwa hiyo basi**, Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0

### HITIMISHO

#### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, Mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema



shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika taarifa hii kwa wakati.

#### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO  
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

**09 Februari, 2018**

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya katika kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi 2018. Taarifa hii ina sehemu Saba na inaanza na utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi wote afya na uzima pia napenda

kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Haki Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kuniadini kuwa Makamu Mwenyekiti na kuendelea kuiongoza Kamati yetu baada ya aliyekuwa Mwenyekiti kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Wajumbe wote kwa ushirikiano mkubwa walionipa katika utekelezaji wa shughuli za Kamati yetu. Kwa namna ya kipekee kabisa kwa niaba ya Kamati nampongeza Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri, hii inatokana na Uongozi wake mahiri hasa katika kipindi chote akiwa Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nachukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Tabora Kaskazini kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano wao na msaada wanaonipa ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Majukumu hayo yalitekelezwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2017 hadi Januari, 2018. Masharti ya Kanuni hii yanataka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge iwasilishe Bungeni taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli zake ili zijadiliwe na Bunge lako Tukufu katika mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imeundwa chini ya Kanuni ya 118 (1) na (2) ikisomwa pamoja na Fasili ya 1(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kwa mujibu wa Fasili ya 4(1) ya Nyongeza ya Nane, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakapoteleka na Spika; na

(b) Kushughlika mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yanayoteleka na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya kuundwa Kamati, Wajumbe wa Kamati walipatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kwa sasa Wajumbe wa Kamati wanao uzoefu mkubwa wa kutekeleza majukumu waliyonayo kutokana na mafunzo hayo ya kusikiliza mashauri mbalimbali yaliyoteleka kwenye Kamati. Aidha, Kamati imejizatiti katika kufanya utafiti wa uchambuzi mambo yaliyorahisisha kutoa ushauri kuhusu mashauri hayo kwa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa orodha ya ufanunuzi wa mashauri yaliyoshughulikiwa na Kamati. Kamati ilitekeleza majukumu ya kiuchunguzi na wa mashauri kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia shauri la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge na Mheshimiwa Joshua Nassari Mbunge, kudharau Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika Mkutano wa Tatu Kikao cha 32 kilichofanyika tarehe 30 Mei 2016, Mheshimiwa Ester Bulaya (Mbunge) na Mheshimiwa Joshua Nassari (Mbunge), walionesha vitendo vya kudharau Kiti chini ya Spika kwa kupiga kelele, kupiga makofi na kusambaza makaratasi na vitabu hovyoyakumbini, jambo ambalo lilifanya Naibu Waziri wa Maji aliyekuwa ameruhusiwa kuzungumza kushindwa kuendelea kuzungumza kutokana na vitendo hivyo vya vurugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilisikiliza shauri hilo na ilijiridhisha bila kuacha shaka yoyote kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Joshua Nassari kuwa, walifanya vitendo vya dharau kwa Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26 (c), (d), na (e), cha Sheria ya Kinga, Madaraka

na Haki za Bunge na Kanuni ya 77 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Bunge liliazimia na iliwapa Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Joshua Nassari karipio kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri la pili, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka dhidi ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza (Mbunge) kuhusu kusema uwongo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka Mbunge wa Jimbo la Muleba, alitoa malalamiko dhidi ya Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza (Mbunge) kwamba alisema uwongo dhidi yake Bungeni, wakati alipokuwa akichangia mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilielezwa mbele ya Kamati kuwa Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza alieleza kuwa, Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka alipokuwa Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alitumia madaraka yake vibaya kwa kujimilikisha zaidi ya hekari 4,000 katika Kijiji cha Kyamnyorwa na kwamba kiasi hicho cha ardhi ni zaidi ya kiasi alichokiomba kihalali ambacho kilikuwa ni hekari 1,098.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulifanyia uchunguzi suala hili, Kamati ilibaini kuwa kauli za Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza hazikuwa na ukweli wowote hivyo ilimtia hatiani na kumshauri Mheshimiwa Spika kuwa Mheshimiwa Rwamlaza Mbunge asimamishwe kuhudhuria vikao vitatu vya Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti. Bunge lilikubali ushauri huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri la tatu, ni kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mbunge) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika.

Mheshimiwa Freeman Mbowe alituhumiwa kuwa akiwa nje wa Ukumbi wa Bunge mara baada ya kumalizika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) mwezi Aprili 2017, alinukuliwa na Vyombo vya Habari akitoa kauli za kudharau Bunge na Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26 (d), cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbowe alikiri mbele ya Kamati kutenda kosa hilo na aliomba radhi, baada ya kupokea mapendekezo ya Kamati, Bunge liliazimia kumsamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shauri la nne, ni kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Halima Mdee, kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika. Katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge uliofanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), wakati uchaguzi ukifanyika katika Ukumbi wa Bunge, Mheshimiwa Halima Mdee alizungumza Bungeni bila kupata idhini ya Spika kinyume na Kanuni za majadiliano. Aidha, alitumia lugha ya matusi kuudhi na kudhalilisha Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusikiliza shauri hilo Kamati ilijiridhisha kuwa Mheshimiwa Halima Mdee alitenda vitendo alivyotuhumiwa navyo, Kamati kwa kuzingatia kuwa Mheshimiwa Halima Mdee alishawahi kufanya kosa kama hilo Kamati ilishauri asihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba. Hata hivyo, Bunge lilimsamehe Mheshimiwa Halima Mdee baada ya kukiri makosa yake na kumwomba radhi Spika na Bunge na kuahidi kutorudia tena kutenda kosa kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shauri la tano, ni kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Ndugu Paul Makonda Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Ndugu Alexander Mnyeti wakati huo akiwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru kuhusu kuingilia Uhuru na Haki za Bunge. Mnamo tarehe 8 Februari, 2017, katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na hoja iliyotolewa na

Mheshimiwa Mwita Waitara (Mbunge) aliyetoa hoja kwamba Ndugu Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Ndugu Alexander Mnyeti Mkuu wa Wilaya ya Arumeru walinukuliwa na Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii wakitoa kauli za kuingilia uhuru na haki za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchunguzi Kamati iliridhika bila ya kuacha shaka yoyote kwamba Ndugu Paul Christian Makonda na Ndugu Alexander Mnyeti walitenda kosa waliotuhumiwa nalo kutokana na kukiri kwao kosa na kuomba radhi. Kwa kuzingatia ushirikiano uliooneshwa kwa Kamati, kukiri makosa na kuomba radhi Kamati ilipendekeza Bunge liazimie kuwapa onyo kali (*reprimand*) ambapo Bunge lilikubali pendekezo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sita, kusikiliza na kutoa mapendekezo shauri la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Halima Mdee ya kudharau Mamlaka ya Spika. Katika Kikao cha Bunge cha 40 kilichofanyika tarehe 2 Julai, 2017 wakati wa majadiliano ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini, kwa mwaka 2017/2018, Mheshimiwa John Mnyika alitolewa nje na Askari kwa amri ya Spika kwa kitendo chake cha kusimama bila utaratibu na kuanza kusema bila ruhusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alifanya vurugu ukumbini ambapo aliwakimbilia Askari hao na kuwavuta sare zao. Wakati hayo yakitokea Mheshimiwa Ester Bulaya alisimama ukumbini bila ruhusa na alisema bila utaratibu huku akihamasisha Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani watoke Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchunguzi wa shauri hili na ilijiridhisha bila shaka yoyote kuwa Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Halima Mdee walitenda makosa waliyotuhumiwa nayo. Kamati ilizingatia kuwa Wabuge hao walikuwa na kumbukumbu za kurejea makosa hayo hivyo ilipendekezwa wasihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba na Mkutano wa Nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge kutafakari mapendekezo hayo Bunge lilijadili na kuamua kuongezea adhabu ya kuwa Wabunge hao wasihudhurie vikao vilivyobaki vya Mkutano wa Saba, Mkutano wote wa Nane na Mkutano wa Tisa kutokana na mwenendo wao wa kukiuka Sheria na Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri la saba, ilikuwa ni kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mheshimiwa Saed Kubenea kuhusu kudharau Mamlaka. Mnamo tarehe 7 Septemba, 2017 kulitokea tukio la kupigwa risasi Mheshimiwa Tundu Lissu Mwenyezi Mungu ampe ahueni haraka na watu wasiojulikana. Siku ya tarehe 8 Septemba, 2017, Mheshimiwa Spika alitoa taarifa kwa Bunge kuhusu tukio hilo, pamoja na mambo mengine alieleza kuwa kwa maelezo wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa SACPGilles Muroto kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu alipigwa risasi 30 katika maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa hiyo Mheshimiwa Saed Kubenea alinukuliwa na Vyombo mbalimbali vya Habari ikiwemo mitandao ya kijamii akiwa katika Kanisa la Ufufuo na Uzima siku ya Jumamosi tarehe 10 Septemba, akiongea kuhusu idadi ya risasi alizopigwa Mheshimiwa Tundu Lissu kuwa zilikuwa 38 na siyo 30 kama Mheshimiwa Spika alivyolieleza Bunge na Taifa. Kamati ilifanyia kazi shauri hili na kumshauri Mheshimiwa Spika wa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri namba nane, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mheshimiwa Saed Kubenea kuhusu kumkashfu Balozi Ami Mpungwe. Mnamo tarehe 30 Juni, 2017, Balozi Mstaafu ndugu Ami Mpungwe aliandika barua ya malalamiko dhidi ya Mheshimiwa Saed Kubenea kuwa wakati alipokuwa akichangia mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini na siku ya tarehe 15 Juni, 2017, alidai kwamba Balozi Ami Mpungwe alipokuwa Balozi nchini Afrika Kusini aligeuka kuwa dalali wa makampuni ya Makaburu yaliyonunua Benki ya *NBC* na kuchimba *Tanzanite*.

Mheshimiwa Naibu Spika, alieleza ilidaiwa kuwa alipostaafu akawa mmoja wa wamiliki wa makampuni makubwa ya uwekezaji ya *AFGEM* ya *Tanzanite*. Baada ya kufanya uchambuzi wa shauri hili, Kamati ilijiridhisha kuwa malalamiko ya Boloji Ami Mpungwe, hayakukidhi masharti ya Kanuni ya 71(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016. Kanuni hiyo inatamka malamiko yawasilishwe ndani ya siku 14 toka siku maelezo dhidi yake yalipotolewa. Barua ya Boloji iliandikwa baada ya siku 14 kupita, hivyo Kamati ilimshauri Mheshimiwa Spika kutozingatia malamiko ya Boloji Ami Mpungwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri la tisa ni kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mheshimiwa Zitto Kabwe kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika. Katika Mkutano wa Nane wa Bunge baada ya Mheshimiwa Spika kupokea na kukabidhi Serikali taarifa ya Kamati alizoziunda kwa ajili kufanya uchunguzi na kutoa ushauri kuhusu mfumo wa uchimbaji, usimamizi na umiliki na uhibitaji wa biashara ya madini ya *tanzanite* na almasi nchini, Mheshimiwa Zitto Kabwe aliandika katika mtandao wake wa *twitter* maneno ya dharau kwa Spika, Bunge na shughuli za Bunge. Kamati ilifanya uchunguzi wa shauri hili na kukamilisha kisha kumfahamisha na kumshauri Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, shauri la kumi, kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la magazeti ya Mtanzania, Mwananchi, Nipashe, kuhusu kuchapisha na kusambaza taarifa za Kamati. Mnamo tarehe 22 Septemba, 2017 baadhi ya magazeti ya hapa nchini yalichapisha habari zenye maudhui ya ushahidi alioutoa Mheshimiwa Zitto Kabwe, mbele ya Kamati ya Haki, Maadili, Madaraka ya Bunge siku ya tarehe 21 Septemba 2017. Mheshimiwa Zitto alikuwa akijibu tuhuma zilizomkabili za kudharau Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kwa kitendo cha cha kuandika kwenye ukurasa wake wa *twitter* maneno yaliyoshushia hadhi Bunge. Wahariri na Waandishi wa makala hizo, walifika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-



Ndugu Denis Msaki - Mhariri wa Mtendaji wa Gazeti la Mtanzania; Ndugu Bakari Kimwanga, Mwandishi wa Gazeti la Mtanzania; Ndugu Angetile Hosea; Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwananchi; Ndugu Elias Msuya, Mwandishi wa Gazeti la Mwananchi; Ndugu Edmund Msangi, Mhariri wa Gazeti la Nipashe; na Ndugu Gwamaka Alipipi, Mwandishi wa Gazeti la Nipashe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilikiliza Mashahidi hao, Kamati iliwatia hatiani wote kwa makosa waliyokuwa wameshtakiwa nayo. Kamati, kuzingatia kuwa Mashahidi walikiri makosa na kuomba radhi Kamati ilipendekeza ifuatavyo:-

(a) Mashahidi wote wapewe onyo kali (*reprimand*) wasirudie kufanya makosa hayo tena;

(b) Mashahidi ambao ni Wahariri wa magazeti husika wahakikishe wanachapisha habari za kumwomba radhi Mheshimiwa Spika na Bunge katika kurasa za mbele za magazeti yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wahariri wote waliotuhumiwa walichapisha taarifa za kumwomba radhi Mheshimiwa Spika na Bunge katika kurasa za mbele za magazeti yaliyofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitayataja mafanikio ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Katika kushughulikia mashauri ya ukiukwaji wa Kanuni uliofanywa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ni maoni ya Kamati kuwa mafanikio yafuatayo yamefanikiwa:-

(a) Kutokana na majukumu yaliyotekelezwa na Kamati uelewa wa Kamati kuhusiana na majukumu yake umeongezeka. Vilevile uelewa huo umeongezeka miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge na kwa umma na hivyo kuleta heshima kwa Bunge na shughuli za Bunge kwa ujumla.

(b) Kwa kiasi kikubwa nidhamu, ustahimilivu,

heshima, utulivu na uzingatiaji wa Kanuni za majadiliano Bungeni umeimarika kuliko tulivyokuwa mwanzoni mwa Bunge hili wakati Kamati hii ilipoanza kutekeleza majukumu yake.

(c) Kupitia majukumu ya Kamati hii umma umeweza kufahamu kuwa Bunge ni chombo kinachoendeshwa kwa mujibu wa sheria na kwamba chombo hiki kinastahili kupata heshima inayostahili na bila kuingiliwa na chombo chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo changamoto. Katika kushughulikia mashauri haya Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(1) Mashahidi kukwepa kupokea hati za wito. Baadhi ya Mashahidi walioitwa mbele ya Kamati walikwepa kupokea hati za wito yaani (*summons*) hivyo kuchelewesha kuanza na kukamilika kwa shughuli za Kamati.

(2) Mahitaji ya Kamati, baadhi ya Wajumbe wa Kamati walipata mafunzo ya awali mara baada ya Kamati kuundwa. Kamati hii haijapata mafunzo mengine tena hadi sasa kutokana aina ya majukumu yanayofundishwa kwenye Kamati. Imeonekana ipo haja ya kupewa mafunzo ya mara kwa mara kwa kuzingatia kuwa kwa nyakati tofauti kumekuwa na mabadiliko ya Wajumbe wa Kamati hii kwa sababu mbalimbali.

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya Tatu ni ufinyu wa muda; mara nyingi katika kazi ya kushughulikia masuala yanayoletwa kwenye Kamati hufanywa kipindi cha Bunge ambapo shughuli nyingine za Bunge huwa zinaendelea. Kwa mantiki hiyo, Wajumbe wa Kamati wanapaswa kutekeleza majukumu ya Kamati na wakati huo huo kutekeleza majukumu mengine ya Kibunge. Katika mazingira haya na katika kuhakikisha majukumu yanakamilishwa kwa wakati, Kamati imekuwa inatafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kutumia muda wa ziada na siku za mapumziko.

(4) Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya nne ukosefu wa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Kibunge. Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja kumejitokeza mashauri yanayowahusu watu wasiokuwa Wabunge. Wakati wa mahojiano na raia hao ilibainika wazi kuwa walihitaji elimu sahihi ya masuala mbalimbali ya Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo, ili Kamati iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuondokana na changamoto zilizotajwa hapo juu, Kamati inapendekeza mambo yafuatayo:-

(1) Wajumbe wa Kamati wapewe mafunzo zaidi ya weledi na ya mara kwa mara kuhusu wajibu wao. Mafunzo hayo yatawasaidia kujenga uelewa wa Wajumbe katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

(2) Wajumbe wapatiwe fursa ya kutembelea na kujifunza kutoka Kamati za Haki, Maadili na Madaraka ya Mabunge katika nchi nyingine zenye utamaduni unaofanana na wetu ili kuweza kujifunza kupata uzoefu wao hasa Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola.

(3) Wabunge wote wapewe mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Haki, Kinga na Maadili pamoja na ufafanuzi wa majukumu ya Kamati hii ili waweze kutoa ushirikiano kwa Kamati pale inapobidi.

(4) Kamati ipewe muda wa kutosha kushughulikia mashauri yanayoletwa na Spika na kuyakamilisha kwa wakati.

(5) Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge kupitia vyombo mbalimbali vya habari litoe elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Bunge ikiwemo miiko kuhusu Bunge ili kuepuka mgongano kati ya Bunge na raia.

(6) Mheshimiwa Naibu Spika, Mashahidi wanaoitwa mbele ya Kamati kwa ajili ya kuisaidia Kamati

katika uchunguzi wafike mapema ili kuwezesha Kamati kukamilisha kazi yake mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati hii. Kwa niaba ya Kamati, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi ulivyollongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema shughuli za Bunge na kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati yetu iliyoiwzesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili, kuchambua kwa umakini mkubwa mashauri yote yaliyoletwa mbele yetu na Mheshimiwa Spika. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki na usawa bila kumwonea au kumpendelea mtu yeyote. Kwa heshima naomba niwataje na kwa sababu ya ufinyu wa muda naomba majina yao wote Wajumbe wa Kamati hii yaingie kwenye *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndugu Pius Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria; Ndugu Prudence Rweyongeza, Naibu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria; Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Seraphine Tamba, Ndugu Mariam Mbaruku Makatibu wa Kamati na Ndugu Anna Bukosi, Ndugu Joyce Chuma na Ndugu Editruda Kilapilo Wasaidizi wa Kamati na Ndugu Emmanuel Mdidi, Mtalaam wa *Hansard* kwa kuratibu vema kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema yote hayo na kuwasilisha taarifa yangu, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI,  
MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU UTEKELEZAJI  
WA MAJUKUMU KATIKA KIPINDI CHA KUENZIA  
JANUARI 2017 HADI JANUARI 2018 –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya na uzima. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kuniadini kuwa Makamu Mwenyekiti na kuendelea kuiongoza Kamati hii baada ya aliyekuwa Mwenyekiti kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nawashukuru sana wajumbe wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa kwa niaba ya Kamati nampongeza Mhe. Capt. (Mst) George Huruma Mkuchika (Mb) kwa kuteuliwa kuwa waziri, hii ni kutokana na uongozi wake mahiri hasa katika kipindi chote alichokuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Vilevile, nachukua fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la uchaguzi la Tabora Kaskazini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano na msaada wanaonipa ambao unaniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kibunge kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Majukumu hayo yalitekelezwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2017 hadi mwezi Januari 2018. Masharti ya Kanuni hii yanataka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge iwasilishe Bungeni Taarifa

kuhusu Utekelezaji wa shughuli zake ili zijadiliwe na Bunge lako tukufu katika Mkutano wa Mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imeundwa chini ya Kanuni ya 118 (1) & (2) ikisomwa pamoja na fasili ya 1(c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa mujibu wa fasili ya 4 (1) ya Nyongeza ya Nane, Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakatayopelekwa na Spika;

(b) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakatayopelekwa na Spika.

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya kuundwa Wajumbe wa Kamati walipatiwa mafunzo awali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kwa sasa wajumbe wa Kamati wamepata uzoefu mkubwa wa kutekeleza majukumu waliyonayo kutokana na kusikiliza mashauri mbalimbali yaliyopelekwa kwenye Kamati kufanya utafiti, uchambuzi na kutoa ushauri kuhusu mashauri hayo kwa Bunge.

## **2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka huu, Kamati ilitekeleza majukumu ya kikanuni kama ifuatavyo:-

2.1 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri linalomhusu Mhe. Ester A. Bulaya (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika;

2.2 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri lililomhusu Mhe. Joshua S. Nasari (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika;

2.3 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (Mb), kuwa Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) alisema uongo Bungeni dhidi yake;

2.4 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri linalomhusu Mhe. Freeman Mbowe (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika;

2.5 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri linalomhusu Mhe Halima Mdee(Mb), kudharau Mamlaka ya Spika;

2.6 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Ndg. Paul Makonda (Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam) kuhusu kuingilia Uhuru, Haki na Kinga za Bunge;

2.7 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Ndg. Alexander Mnyeti (Mkuu wa Wilaya ya Arumeru), kuhusu kuingilia Uhuru, Haki na Kinga za Bunge;

2.8 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Pili lililomhusu Mhe. Ester A. Bulaya(Mb) kudharau Mamlaka ya Spika;

2.9 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Pili lililomhusu Mhe. Halima Mdee(Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika;

2.10 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Saed Kubenea(Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika;

2.11 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Pili lililomhusu Mhe. Saed Kubenea(Mb) kuhusu kumkashifu Balozi Ami Mpungwe asiye mbunge, wakati akichangia Bungeni;

2.12 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Zitto Kabwe(Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika;

2.13 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Pili lililomhusu Mhe. Zitto Kabwe(Mb) kuhusu kusambaza Taarifa za Kamati bila utaratibu;

2.14 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la malalamiko dhidi ya vyombo vya Habari ambavyo ni Magazeti ya Mtanzania, Mwanachi na Nipashe kuhusu kuchapisha na kusambaza Taarifa za Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge bila idhini ya Bunge.

### **3.0 UFAFANUZI WA MASHAURI YALIYOSHUGHULIKIWA NA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuorodhesha shughuli zilizofanywa na Kamati, ni vema sasa kutoa ufafanuzi wa shughuli hizo kama ifuatavyo:-

#### **3.1 Kushughulikia shauri la Mhe. Ester A. Bulaya (Mb) kudharau Mamlaka ya Spika**

**Mheshimiwa Spika**, katika mkutano wa Tatu Kikao cha Thelathini na Mbili kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 Mheshimiwa Ester Amos Bulaya (Mb) alidharau kiti cha Spika kwa kupiga kelele na kupiga makofi kwa vurugu jambo ambalo lilimfanya Naibu Waziri wa Maji aliyekuwa ameruhusiwa kuzungumza kushindwa kuendelea kuzungumza kutokana na vitendo hivyo. Vilevile alikaidi kuacha vitendo hivyo na kendelea kusimama na kupiga kelele na Kusambaza karatasi na vitabu hovy kwa makusudi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilisikiliza shauri na kujiridhisha bila ya kuacha shaka yoyote kwamba Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alidharau Mamlaka ya Spika kinyume na Kifungu cha 26(c) (d) (e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 pamoja na Kanuni ya 74 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 33(1) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge Bunge liliazimia na kumpa Mhe. Ester Bulaya (Mb) Karipio kali.

#### **3.2 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Joshua S. Nasari (Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika**

**Mheshimiwa Spika**, katika mkutano wa Tatu Kikao cha Thelathini na Mbili kilichofanyika tarehe 30 Mei, 2016 Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari (Mb) alituhumiwa kudharau kiti cha Spika kwa kupiga kelele na kupiga makofi kwa vurugu jambo ambalo lilimfanya Naibu Waziri wa Maji aliyekuwa ameruhusiwa kuzungumza kushindwa kuendelea



kuzungumza kutokana na vitendo hivyo. Aidha alikaidi maelekezo yaliyomtaka kutulia bali aliendeleza vitendo vyake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimwona Mhe. Nassari ana hatia na hivyo Bunge hili liliazimia kumsamehe kwa kumpa karipio kali baada ya kukiri na kuomba radhi mbele ya Kamati.

### 3.3 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya malalamiko ya Mhe. Prof. Anna Tibaijuka (Mb), dhidi ya Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) kuhusu kusema uongo Bungeni

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, Mbunge wa jimbo la Muleba alitoa malalamiko dhidi ya Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) kwamba alisema uongo dhidi yake Bungeni wakati alipokuwa akichangia mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) alieleza kuwa Mhe. Prof. Anna K. Tibaijuka alipokuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alitumia madaraka yake vibaya kwa kujimilikisha zaidi ya ekari 4,000 katika Kijiji cha Kyamyorwa na kwamba kiasi hicho cha ardhi ni zaidi ya kiasi alichokiomba kihalali ambacho ni ekari 1,098.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kulifanyia kazi shauri hili Kamati ilibaini kuwa kauli za Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) hazikuwa na ukweli wowote hivyo ilimtia hatiani.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilikubali pendekezo la Kamati kuwa Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) asimamishwe kuhudhuria vikao vitatu vya Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti.

### 3.4 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Aikael Freeman Mbowe (Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika

**Mheshimiwa Spika**, Mhe. Freeman Mbowe (Mb), alituhumiwa

kuwa, akiwa nje ya Ukumbi wa Bunge mara baada ya kumalizika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, alinukuliwa na vyombo vya habari akitoa kauli za kudharau dhidi ya Bunge na Mamlaka ya Spika, kinyume na Kifungu cha 26 (d) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296 R.E 2015*]. Mhe. Mbowe ilikiri kutenda kosa hilo na kuomba radhi hivyo, Kamati ilijiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa alitenda kosa alilotuhumiwa nalo. Baada ya Bunge kupokea mapendekezo ya Kamati na kuzingatia matakwa ya kifungu cha 33(1) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, liliazimia kumsamehe.

### **3.5 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Halima Mdee (Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika**

**Mheshiwa Spika**, katika Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika tarehe 4 Aprili, 2017 ulifanyika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA). Wakati uchaguzi ukifanyika katika Ukumbi wa Bunge Mhe. Halima Mdee alizungumza Bungeni bila idhini ya Spika, kinyume na Kanuni za Majadiliano chini ya Kanuni za 59 na 60 za Kanuni za Kudumu za Bunge na Kutoa lugha ya matusi, kuudhi na kudhalilisha Mbunge mwingine, kinyume na Kanuni ya 64(1) (f) na (g) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Baada ya kusikiliza shauri hili, Kamati ilijiridhisha kuwa Mhe. Halima Mdee (Mb) alitenda vitendo alivyotuhumiwa navyo. Kamati katika kupendekeza adhabu ilizingatia kuwa Mhe. Halima Mdee (Mb) alishawahi kutenda kosa kama hilo, Kamati ilishauri asihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba (Bunge la Bajeti) kuanzia tarehe ya Azimio la Bunge. Hata hivyo, Bunge ilimsamehe Mhe. Halima James Mdee (Mb) baada ya kukiri makosa na kumwomba radhi Spika na Bunge na kuahidi kutorudia kutenda tena kosa kama hilo.

**3.6 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Ndg. Paul Makonda (Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam), kuhusu kuingilia Uhuru na Haki za Bunge;**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na hoja iliyotolewa na Mhe. Mwita Waitara (Mb) alitoa hoja kwamba Ndg. Paul Christian Makonda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam alinukuliwa na kituo cha televisheni cha *Clouds* akisema Wabunge wanasinzia Bungeni. Kwa maoni ya Mhe. Waitara (Mb) lilikuwa ni dharau kwa Bunge na pia kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchunguzi na ilijiridhisha bila ya kuacha shaka yoyote kwamba Ndg. Paul Christian Makonda alitenda kosa alilotuhumiwa nalo baada ya kukiri na kuomba radhi mbele ya Kamati. Kwa kuzingatia ushirikiano wake wakati wa kusikiliza shauri, kukiri makosa na kuomba radhi, Kamati ilipendekeza Bunge linaazimie kumpa onyo kali (*reprimand*) ambapo Bunge lilikubali pendekezo hilo na kumsamehe.

**3.7 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Ndg. Alexander Mnyeti (Mkuu wa Wilaya ya Arumeru) kuhusu kuingilia Uhuru na Haki za Bunge;**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha Maazimio yaliyotokana na hoja iliyotolewa na Mhe. Mwita Waitara (Mb) alitoa hoja kwamba Mkuu wa wilaya ya Arumeru Ndg. Alexander Pastory Mnyeti aliandika katika mtandao wa kijamii wa *Facebook* kuwa Azimio la Bunge lililotokana na pendekezo la Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa la kuwapatia semina Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuhusu namna ya kutekeleza majukumu yao ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi na anashauri wafanye kazi zao na za wengine waachiwe wenyewe, jambo ambalo kwa maoni ya Mhe. Waitara (Mb) lilikuwa ni dharau kwa Bunge na pia kuvunja haki na kuingilia uhuru wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchunguzi na ilijiridhisha bila ya kuacha shaka yoyote kwamba Ndg. Alexander Mnyeti alitenda kosa walilotuhumiwa nalo baada ya kukiri na kuomba radhi mbele ya Kamati. Kwa kuzingatia ushirikiano wake wakati wa kusikiliza shauri, kukiri makosa na kuomba radhi, Kamati ilipendekeza Bunge linaazimie apewe onyo kali (*reprimand*) ambapo Bunge lilikubali pendekezo hilo na kumsamehe.

### 3.8 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Ester Amos Bulaya(Mb) na Halima Mdee (Mb) ya kudharau Mamlaka ya Spika**

**Mheshimiwa Spika**, katika Kikao cha Bunge cha Arobaini kilichofanyika tarehe 2 Juni, 2017, wakati wa Majadiliano ya Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mhe. Livingstone Joseph Lusinde (Mb) alipewa nafasi ya kuchangia katika mjadala huo. Wakati akiendelea na mchango wake, Mhe. John John Mnyika (Mb) alisimama kuomba kutoa taarifa kuhusu utaratibu. Mhe. Spika alimruhusu atoe taarifa yake.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kutoa taarifa hiyo, Mhe. Spika alimruhusu Mhe. Livingstone Lusinde (Mb) aendelee kuchangia. Lakini kabla hajaendelea na mchango wake, Mhe. John Mnyika (Mb) alisimama bila utaratibu na kuanza kusema bila ruhusa ya Spika akidai kuwa kuna Mbunge aliyemuita mwizi. Mhe. Spika alimtaka Mhe. Mnyika (Mb) akae chini ili mjadala uendelee. Hata hivyo aliendelea kufanya fujo. Ndipo Mhe. Spika aliamuru Mpambe wa Bunge (*Sergeant at Arms*) amtoe Mhe. Mnyika (Mb) nje ya Ukumbi wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati Mhe. Mnyika (Mb) akitolewa nje ya Ukumbi wa Bunge na askari wa Bunge, Mhe. Halima James Mdee (Mb) aliwakimbilia askari hao huku akivuta sare (makoti) ya askari wawili kati ya askari waliokuwa wakimtoa nje Mhe. John Myika (Mb). Wakati huo, Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) alisimama Ukumbini huku akisema bila utaratibu na kuhamasisha Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka nje ya Ukumbi. Mhe. Spika alimuonya Mhe. Ester Bulaya

(Mb) kuacha vitendo alivyokuwa akifanya Ukumbini, lakini Mhe. Bulaya (Mb) aliendelea kusimama na kuendelea kuhamasisha Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutoka nje. Mhe. Bulaya na Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni walitoka nje ya Ukumbi wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanyia uchunguzi shauri hili na ilijiridhisha bila ya shaka yoyote kuwa Mhe. Ester Amos Bulaya (Mb) na Mhe. Halima Mdee. walitenda makosa waliyotuhumiwa nayo. Kamati ilizingatia kuwa wabunge hawa ni wakosaji wa mara kwa mara hivyo ilipendekeza Mhe. Ester Amosi Bulaya (Mb) na Mhe. Halima James Mdee (Mb) wasihudhurie vikao vyote vilivyobaki vya Mkutano wa Saba, vikao vyote vya mkutano wa Nane.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Bunge kutafakari mapendekezo ya Kamati, Bunge liliazimia kuwa wabunge hao wasihudhurie vikao vilivyobaki vya Mkutano wa Saba, Bunge lote la Nane na Bunge la Tisa kutokana na tabia zao za mara kwa mara za kufanya vitendo vya kudharau Mamlaka ya Spika.

3.9 **Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Saed Kubenea (Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika**  
**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 7 Septemba, 2017, kulitokea tukio la kupigwa risasi Mhe Tundu Lissu na watu wasiojulikana. Siku ya tarehe 8 Septemba 2017 Mheshimiwa Spika, alitoa taarifa kwa Bunge kuhusu tukio hilo. Pamoja na mambo mengine Mhe. Spika alieleza kuwa kwa maelezo ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa SACP Giles Mloto ni kwamba Mhe.Tundu Lissu alipigwa risasi Thelathini katika maeneo mbalimbali ya mwili wake.

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia taarifa hizo Mhe Saed Kubenea alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii ukiwa katika Kanisa la Ufufuo na Uzima siku ya Jumapili tarehe 10 Septemba, 2017 akiongea kuhusu idadi ya risasi alizopigwa Mhe.Tundu Lissu kuwa Mheshimiwa Tundu Lissu alipigwa risasi 38 na sio 30 kama Mhe.Spika alivyolieleza Bunge na Taifa

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanyia kazi shauri hili na kumshauri Mhe. Spika kwa mujibu wa Kanuni.

**3.10 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Saed Kubenea(Mb) kuhusu kumkashifu Balozi Ami R. Mpungwe**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 30 Juni 2017 Balozi Mstaafu Ami R. Mpungwe aliandika barua ya malalamiko dhidi ya Mhe. Saed Kubenea (Mb) kuwa, wakati alipokuwa akichangia mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini siku ya tarehe 15 Juni, 2017 alidai kwamba Balozi Ami R. Mpungwe alipokuwa Balozi nchini Afrika Kusini aligeuka kuwa dalali wa makampuni ya makaburu yaliyonunua Benki ya NBC, yaliyochimba Tanzanite na alipostaafu akawa mmoja wa wamiliki wa makampuni makubwa ya uwekezaji wa AFGEM ya Tanzanite.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa shauri hili, Kamati ilijiridhisha kuwa malalamiko Balozi Ami R. Mpungwe hayakukidhi masharti ya Kanuni ya 71(1) (b) ya Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 inayotaka malalamiko kuwasilishwa kwa Spika ndani ya siku 14. Aidha Kamati ilishauri kuwa malalamiko ya Balozi Ami R.Mpungwe yasizingatiwe na Bunge wala kufikiriwa kuingizwa katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) kwa sababu hayajatimiza masharti yaliyowekwa na kanuni ya 71 (1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**3.11 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe(Mb) kuhusu kudharau Mamlaka ya Spika**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, baada ya Mhe. Spika kupokea na kukabidhi Serikalini taarifa za Kamati alizoziunda kwa ajili ya kufanya uchunguzi na kutoa ushauri kuhusu mfumo wa uchimbaji, usimamizi, umiliki na udhibiti wa biashara ya madini ya Tanzanite na Almasi nchini, Mhe. Zitto Kabwe (Mb) aliandika katika mtandao wa *twitter* maneno ya dharau kwa Spika, Bunge na Shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchunguzi wa shauri hili na kukamilisha kisha kumshauri Mhe.Spika kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge.

### 3.12 Kusikiliza na kutoa mapendekezo ya shauri la Magazeti ya Tanzania, Mwanachi na Nipashe kuhusu kuchapisha na kusambaza taarifa za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 22 Septemba, 2017 baadhi ya magazeti ya hapa nchini yalichapisha habari zenye maudhui ya ushahidi aliooa Mhe. Zitto Kabwe (Mb) katika Kamati ya Haki, Madili na Madaraka ya Bunge siku ya tarehe 21 Septemba, 2017 wakati akijibu tuhuma zilizomkabili za kudharau Mamlaka ya Spika na shughuli za Bunge kutokana na kitendo chake cha kuandika kwenye ukurasa wake wa Twitter maneno ya kulishushia hadhi Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, magazeti yaliyochapisha habari hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Gazeti la Tanzania, Toleo Na. 8676 liliandika kichwa cha habari kifuatacho: *"BUNGE LIMEKOSA MSHAWASHA"*.

(b) Gazeti la Mwananchi, Toleo Na. 6265 liliandika kichwa cha habari kifuatacho: *"ZITTO ASHUSHA NYUNDO 10 KAMATI YA BUNGE"*.

(c) Gazeti la Nipashe, Toleo Na. 0579345 liliandika kichwa cha habari kifuatacho: *"ZITTO AMWAGA MBOGA"*.

**Mheshimiwa Spika**, wahariri na waandishi wa makala hizo kutoka katika kila gazeti walifika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:- **Ndg. Denis Msaki**, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Tanzania, **Ndg. Bakari Kimwanga** Mwandishi wa Gazeti la Tanzania, **Ndg. Angetile Osiah**, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Mwananchi, **Ndg. Elias Msuya**, Mwandishi wa Gazeti la Mwananchi, **Ndg. Edmond Msangi**, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, na **Ndg. Gwamaka Alipipi**, Mwandishi wa Gazeti la Nipashe.

**Mheshimiwa Spika**, Wahariri na Waandishi hao wa Magazeti tajwa, walifika mbele ya Kamati na walipohojiwa walikiri makosa yao na kuomba msamaha. Walieleza kuwa habari hizo walizipata kutoka kwa Mhe. Zitto Kabwe (Mb) aliyewatumia utetezi wake wa maandishi. Mashahidi waliomba radhi kwa Bunge kwani walipotoshwa na Mhe. Zitto Kabwe (Mb) ambaye walianini ni mtu sahihi kuwapatia habari hizo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasikiliza mashahidi, Kamati iliwatia hatiani wote kwa makosa waliyokuwa wameshtakiwa nayo. Adhabu wanayostahili kupewa kwa mujibu wa Kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 ni kulipa faini isiyozidi laki tano, au kifungo jela kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu, au vyote kwa pamoja (faini na kifungo).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kuzingatia Masharti hayo ya Sheria, kwa kuzingatia kuwa mashahidi walikiri makosa yao mbele ya Kamati, na kwa kuzingatia mashauri Mbalimbali ya nyuma yenye mazingira ya makosa kama haya yaliyoamuliwa na Bunge (*precedents*); Kamati ilipendekeza na kukushauri, ushauri ambao uliukubali na kuamua ifuatavyo:-

(a) Mashahidi (watuhumiwa) wote wamesamehewa makosa yao kwa kuzingatia kwamba wamekiri makosa yao bila kuleta usumbufu kwa Kamati, wametoa ushirikiano kwa Kamati pale walipoitwa na kuitikia wito wa Kamati bila kuleta usumbufu;

(b) Mashahidi wote wapewe onyo kali (*reprimand*) wasirudie kufanya makosa kama hayo;

(c) Mashahidi ambao ni wahariri wa magazeti husika wahakikishe wanachapisha habari ya KUMUOMBA RADHI MHE. SPIKA WA BUNGE katika kurasa za mbele za magazeti yao.



#### 4.0 MAFANIKIO

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia makosa ya ukiukwaji wa Kanuni uliofanywa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, ni maoni ya Kamati kuwa mafanikio yafuatavyo yamefikwa:-

(a) Kutokana na majukumu yaliyotekelezwa na Kamati, kamati na majukumu yake kwa kiasi fulani yameweza kufahamika kwa waheshimiwa wabunge na kwa umma na hivyo, kuleta heshima kwa Bunge na shughuli za Bunge kwa ujumla;

(b) Kwa kiasi kikubwa nidhamu, ustahimilivu, heshima, utulivu na uzingatiaji wa Kanuni za Majadiliano bungeni umeimarika kuliko ilivyokuwa mwanzoni mwa Bunge hili.

(c) Kupitia majukumu ya Kamati hii umma umeweza kufahamu kuwa Bunge ni chombo kinachoendeshwa kwa mujibu wa Sheria na kwamba chombo hiki kinastahili kupata heshima inayostahili

#### 5.0 CHANGAMOTO WAKATI WA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Katika kushughulikia mashauri haya, Kamati ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

##### 5.1 Ukwepaji wa kupokea Hati za wito

Baadhi ya Mashahidi walioitwa mbele ya Kamati walikwepa kupokea Hati za Wito (Summons) hivyo, kuchelewesha shughuli za Kamati. Katika mazingira haya Kamati lililazimika kuwapatia mashahidi hao hati za wito kutumia Jeshi la Polisi kwa mujibu wa kifungu cha 15(3) cha sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge

##### 5.2 Ukosefu wa Mafunzo kwa Kamati

Baadhi ya wajumbe wa Kamati walipata mafunzo ya awali

mara baada ya Kamati kuundwa na haijapatiwa mafunzo mengine hadi sasa. Kwa nyakati tofauti kumekuwa na mabadiliko ya wajumbe wa Kamati kutokana na sababu mbalimbali. Kutokana na Kamati kutopatiwa mafunzo mengine, wajumbe walioletwa katika Kamati baada ya Kamati kupatiwa mafunzo ya awali, hawajapata mafunzo yoyote. Suala la elimu ni endelevu ili kuwezesha kuongeza ujuzi katika utekelezaji wa majukumu.

### 5.3 Ufinyu wa muda

Mara nyingi Kazi ya kushughulikia masuala yanayoletwa na Spika hufanyika kipindi cha Bunge ambapo shughuli nyingine za Bunge huwa zinaendelea. Kwa mantiki hiyo, Wajumbe wa Kamati hupaswa kutekeleza majukumu mengine ya Kibunge kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika mazingira haya Kamati imekuwa inatafuta ufumbuzi wa tatizo hili kwa kutumia muda wa ziada na siku za mapumziko ili kukamilisha shughuli za Kamati.

### 5.4 Ukosefu wa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya kibunge

Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja kumejitokeza mashauri yanayowahusu raia ambao sio wabunge. Wakati wa mahojiano na raia hao ilibainika wazi kuwa kuna baadhi ya raia wameingia katika mashauri hayo kwa kukosa elimu sahihi ya masuala mbalimbali ya Bunge ikiwemo miiko ya Bunge.

## 6.0 MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuondokana na changamoto zilizotajwa, Kamati ina mapendekezo yafuatayo:-

6.1 Wajumbe wa Kamati wapewe mafunzo zaidi kuongeza weledi na ya mara kwa mara kuhusu wajibu wao. Mafunzo hayo yatawasaidia kujenga weledi zaidi kwa Wajumbe katika utekelezaji wa majukumu ili kutekeleza kazi yao kwa ufanisi zaidi.

6.2 Aidha, wajumbe wapatiwe fursa ya kutembelea na kujifunza kutoka Kwa Kamati Kama hii ya Haki, Maadili na Madaraka katika Nchi zenye utamaduni unaofana na wetu.

6.3 Wabunge wapewe mafunzo kuhusu Haki, Kinga, na Maadili pamoja na ufafanuzi wa majukumu ya Kamati ili waweze kutoa ushirikiano kwa Kamati pale inapobidi.

6.4 Kamati inashauri mchakato wa kutunga Kanuni za Maadili kwa Wabunge uanzishwe ili kuweza kupata mwongozo wa usimamizi wa maadili ya Wabunge kwa lengo la kuendelea kuimarisha na kudumisha utulivu Bungeni.

6.5 Kamati ipewe muda wa kutosha kushughulikia mashauri yanayoletwa na Spika na kuyakamilisha kwa wakati.

6.6 Bunge kupitia vyombo mbalimbali vya habari litoe elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo miiko kuhusu Bunge ili kuepuka mgongano kati ya Bunge na raia.

6.7 Watu wote wanaoitwa kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kuisaidia Kamati au kwa ajili ya uchunguzi wafike mapema ili kuwezesha Kamati hiyo kukamilisha kazi yake mapema.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati hii. Kwa niaba ya Kamati, napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhiti kwa jinsi unavyoliongoza Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuongoza vyema shughuli za Bunge na kwa kutoa ushirikiano kwa Kamati yangu uliyoiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Mashauri yote yaliyoletwa na Mhe. Spika. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki na usawa bila kumwonea au kumpendelea mtu

yeyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- (i) Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)-M/ Mwenyekiti
- (ii) Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)- Mjumbe
- (iii) Mhe. Amina Nassoro Makilagi (Mb)-Mjumbe
- (iv) Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma (Mb)-Mjumbe
- (v) Mhe. Othman Omar Haji (Mb)-Mjumbe
- (vi) Mhe. Rose Kamili Sukum (Mb)- Mjumbe
- (vii) Mhe. George Malima Lubeleje (Mb)-Mjumbe
- (viii) Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb)-Mjumbe
- (ix) Mhe. Susan Anselm Lyimo (Mb)- Mjumbe
- (x) Mhe. Tunza Issa Malapo (Mb)- Mjumbe
- (xi) Mhe. Asha Abdallah Juma ( Mb)- Mjumbe
- (xii) Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb)-Mjumbe
- (xiii) Mhe. Innocent Sebba Bilakwate (Mb)-Mjumbe
- (xiv) Mhe. Ali Hassan Omar King (Mb)-Mjumbe
- (xv) Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)-Mjumbe
- (xvi) Mhe. Eng. Ramo Makani (Mb)-Mjumbe

Napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Ndugu. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudence Rweyongeza, Naibu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Maria Mdulugu, Ndugu Seraphine Tamba, Ndugu Mariam Mbaruku Makatibu wa Kamati pamoja na Ndugu Joyce Chuma, Katibu Muhtasi na Ndugu Editruda Kilapilo Msaidizi wa Kamati na Ndugu Emmanuel Mdidi, mtalaamu wa Hansard kwa kuratibu vyema kazi za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)

**MAKAMU MWENYEKITI**

**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**

Februari, 2018

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji kwa mujibu wa majina niliyonayo hapa, lakini pia uwiano tulionao nimeletewa majina tayari hapa na Vyama vyote vyenye uwakilishi Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Katani Ahmad Katani, atafuatiwa Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji ni dakika Tano nakumbushwa hapa na Katibu. Mheshimiwa Katani, atafuatiwa Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma ajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru wewe lakini pia nimpongeze Mzee wangu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika kwa kupewa dhamana hii ya kuongoza Wizara ya Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la Wizara hii ya Ulinzi, kwangu kule Tandahimba kuna mambo yanafanywa na Askari wa Jeshi la Polisi, mambo ya hovyoy kabisa. Mfano mdogo miezi mitatu iliyopita Askari Polisi wa Usalama Barabarani wamekuwa wakiwakamata vijana na kuwapiga. Sasa sijajua *PGO* ndiyo inataka hivyo au namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo mara kadhaa nimewahi kumwambia Waziri mwenye dhamana kwamba *DTO* wa Tandahimba mambo anayofanya Tandahimba hayako sahihi. Sasa sijui kama kuna sheria inamwongoza Askari Polisi anapokamata mtuhumiwa ampige. Hili limekuwa ni jambo ambalo linalojirudia kwa Jimboni kwangu, mara kadhaa anawachomekea magari vijana wa bodaboda. Hii ni hali ya hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wakati atakapokuja

atatuambia kwamba maelekezo aliyoyatoa sasa yamekaa namna hii au namna gani. Hata hivyo, ukienda Dar es Salaam pale sijajua au *operation* au ni kitu gani, ukiingia Mtaani Askari ambao hawana *uniform* wanakamata dereva bodaboda, ananyang'anya funguo kabla ya kumwambia jambo lolote lile, wakati mwingine hawajulikani kama hawa ni Askari au lah! Sasa ni vema kwa sababu mna bodaboda ambazo Askari wake wanavaa *uniform* wale wanafahamika vizuri mnaporuhusu Askari wanakwenda mtaani hawana *uniform*, wanakamata hovyoy, mnahatarisha hata usalama wa raia wale wanaoishi mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumzwa hapa wakati wanazungumza suala la ulinzi wa Wabunge, jambo lililotokea kwa Mheshimiwa Lissu ni jambo la fedheha kubwa sana kwa Taifa letu. Ni jambo ambalo kwa namna moja au nyingine sijui kama Wabunge tunaona uzito wake. Limezungumzwa sana kwenye Bunge hili, lakini bado Wizara mpaka leo waliofanya matukio yale hakuna maelezo yanayojitosheleza kwamba wale watu wakoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ambayo yako *clear* kabisa, eneo la tukio ambalo Mheshimiwa Lissu amepigwa risasi ni eneo ambalo wanakaa Mawaziri, Mheshimiwa Naibu Spika unaishi pale, lakini vyombo vya ulinzi vinakuwepo pale, lakini mpaka leo jambo hili la Mheshimiwa Lissu limekuwa kizungumkuti halizungumzwi kwa mapana na kuonekana ufumbuzi wake unakuwaje. Leo kama Mheshimiwa Waziri jambo la Mheshimiwa Lissu analiona ni la masihara hili leo linatokea kwa Wapinzani kesho inawekana Wapinzani tukachukua nchi. Je, likitokea kwenu tuliangalie kama tunavyoliona hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati nimeona imeshauri jambo jema sana na nione sasa kuwe na umuhimu kama wenzetu wa Kenya, Wabunge wanalindwa mpaka majumbani kwao kuna ulinzi wa Jeshi la polisi kwa nini Tanzania tusiige majirani zetu pale. Kamati imeshauri vizuri imezunguza kwa uhalisia kwamba Wabunge wakati mwingine tunapotekeleza majukumu yetu tunapotetea

rasilimali za nchi, wapo watu wanaoiba hawawezi kutuacha salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vema tuone kwamba Bunge hili linaona na Wizara zione kabisa kwamba kuna umuhimu wa Wabunge kuwa na ulinzi wanapokuwa Majimboni lakini ikiwezekana hata tunapokuwa Dodoma hapa. Haya matukio mengine yanayotokea kama tunakuwa na ulinzi wa Jeshi la Polisi yawezekana kabisa yasitokee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine zipo Balozi zetu ukienda China kule kuna Maafisa wa Ubalози hawapo, lakini bado hakuna hawajawapeleka watu wa kwenda kuziba nafasi zile. Sasa sijui kwenye Diplomasia ya uchumi kwenye jambo hili likoje, Waziri wa Mambo ya nje nadhani anaweza kutusaidia na hii siyo China tu, zipo nchi hata ukienda *South Africa*, mambo haya yako hivyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani. Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Dkt. Ishengoma, Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hii hoja. Mimi ni Mjumbe pia wa Kamati hii ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge. Kwanza naipongeza Kamati hii kwa kazi ambazo imekuwa ikizifanya pamoja na ugumu wake na changamoto zake, lakini imekuwa ikifanya kazi bila kumwonea mtu yeyote kama taarifa ambavyo imeweza kusomwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge hili liweze kuelewa Kamati ile ya Maadili ina Vyama vyote, tuko mle ndani Vyama vyote na hatujawahi kupiga kura kutoa hukumu yoyote ile, tumetoa hukumu zote tukiwa tumekubaliana na hii inamaanisha kwamba hukumu zile hazikuwa na

upendeleo wa aina yoyote. Kama ingekuwa siyo Kamati ile ya Maadili ambayo Mheshimiwa Naibu Spika unaiielewa kazi mnayotuletea pamoja na Mheshimiwa Spika, kusingekuwa na Kamati ile sijui Bunge hili lingekuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka hasa sisi ambao ni Wabunge wageni, Bunge hili wakati tunaanza nidhamu ilikuwa siyo kabisa ambayo Mheshimiwa Mbunge anapaswa kuwa nayo kwa baadhi ya Wabunge wenzetu. Hata hivyo, baada ya mashauri mbalimbali leo hii hata ukiliangalia Bunge lina nidhamu kubwa. Nawashukuru sana Wabunge pia kwa kutuwezesha sisi kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hata unaona hata ukimwambia mtu anayevunja taratibu labda ukimwambia kaa chini, hurudii hata mara mbili, mara tatu, anakaa. Haikuwepo hiyo mwanzoni na nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba mmeona umuhimu wa kuwa na nidhamu humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka hata uhuru wa kuzungumza kama ambavyo watu wamekuwa waki-*quote* Katiba kwamba wana uhuru wa kuzungumza. Uhuru wowote ule siyo *absolute*, kwa maana kwamba siyo timilifu kuna mipaka yake hata katika kuongea, sasa ukiwa umetumia vibaya uhuru huo basi unajikuta unafika mahali ambapo sipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hata wakati Mbunge mmoja anaongea hapa jana, Mheshimiwa Mbunge mmoja alikuwa anaongea suala ambalo limekatazwa hata kwenye vifungu hivi vya Kanuni zetu huruhusiwi kutumia lugha ambayo ni ya matusi au ya dhihaka hata kwa Mbunge mwenzio, siyo Mheshimiwa Rais tu kama ambavyo kila kitu Mheshimiwa Rais amekuwa *over protected* siyo kweli, hata kwa Mbunge mwenzio huruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni zetu hizi na hasa hiyo ya 64(1)(f) na (g), inakataza kabisa hata kwa Mbunge mwenzio. Kwa hiyo siyo Rais tu hata sisi tunapaswa kuheshimiana. Pia kuzungumza uongo



imekatazwa, kila jambo unalozungumza humu basi uwe una ushahidi nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa amezungumza suala la kwamba Mheshimiwa Rais alimwita Mheshimiwa Lowasa kumrudisha kwenye Chama cha Mapinduzi. Sijaona hata kwenye *clip* yoyote kama ambavyo huwa mnatuma *clip*, je, mtu angekwambia uje Kamati ya Maadili uthibitise unayo *clip* hiyo au mtu anaongea tu ili kufurahisha na kujaribu kutaka wananchi waamini hivyo. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuwe tunaangalia tunachokizungumza ili msije mkajikuta mnaletwa kwenye Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kusingekuwa hata na *Code of Conduct* unaweza ukaona humu ndani kwenyewe, hivi mavazi ya humu ndani yangekuwaje! Sasa kwa sababu kuna *Code of Conduct* Waheshimiwa Wabunge wanachagua mavazi ya kuvaa. Hata hizi sheria kama tunavyosema hatuhitaji kumwonea mtu yeyote, tunafanya kazi kwa ajili ya kuweka mambo sawa Bungeni kama ambavyo sasa tumeendelea kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya watu ni wachochezi wapo humu, lakini Waheshimiwa Wabunge wale ambao wanawachochea wenzao natoa rai tu kwamba jaribuni kuwaangalia wale mnaowachochea, wengine wanachochea anayepewa adhabu ni mwingine, sasa wewe unapata faida gani? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Victor Mwambalasa ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia.

Kwanza kabisa nitoe pongezi kwa vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kutunza amani. Pili, nashukuru sana na natoa pongezi kwa viongozi wote waliotangulia na waliopo kwa kutunza amani ya nchi yetu kwa sababu nchi ya Tanzania licha ya matatizo mbalimbali yaliyopo lakini bado ina amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba sana tena sana na nashukuru tuwe na amani na utulivu humu Bungeni mara tunapochangia hoja zetu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuchangia ni Wabunge wote tuweze wakati wowote tunapochangia tuweze kufuata Kanuni, Sheria na Taratibu za Bunge. Tukiweza kufuata Kanuni, Sheria na Taratibu za Bunge halitajitokeza tatizo lolote humu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililoongelewa kwenye Kamati nasi wenyewe tunaliongelea hasa Wabunge wote naamini wataafiki ni Wabunge wote kupewa semina kuhusu mambo ya Kanuni, kwa sababu Wabunge wote wakipewa semina kuhusu mambo ya Kanuni Kiti kitakachokuwa kimekaa hapo ulipokaa naamini hakitasumbuliwa kwa sababu wote wataheshimu Kanuni na Taratibu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilikuwa linasumbua ni Shahidi kuitwa alafu Shahidi haonekani. Ili utunze amani na utulivu na haki ya binadamu unapoitwa kwenye Kamati ya Maadili ni vizuri uheshimu, ufike kwa wakati muafaka ambao unapangiwa, kuliko kuanza kutumiwa Polisi kukamatwa siyo vizuri. Kwa hiyo, naomba kuwa licha ya Wabunge kupewa Semina naamini kuwa tutafuata Kanuni na Taratibu za Bunge kuweza kufika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jinsi unavyoendesha Bunge wewe mwenyewe na Wabunge tukifata, narudia tena tukifata Kanuni na Sheria na Taratibu za Bunge na upendo ukitawala humu Bungeni tutakuwa na amani na utulivu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee hayo, ila kwa kumaliza nirudie kuwashukuru na kuwapa pongezi vyombo vya ulinzi kwani hivi karibuni lilikuwepo wimbi la watoto kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha, ila nashukuru sasa hivi naona wimbi hili la watoto kupotea limepungua. Kwa hiyo, hii inadhihirisha kuwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja, namaliza kwa kusema kuwa naomba tufuate Kanuni, Taratibu na Sheria za Bunge tutaendesha vizuri Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Peter Msigwa atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Augustino Masele ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati nzima kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya kama Kamati, lakini kwa usimamizi mzuri wa Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa kwanza kwenye kitabu chetu, Kamati katika aya ya tatu imesikitishwa kwa kitendo cha kupigwa risasi Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Tundu Lissu. Jambo hili lilisikitisha, lilitua, vilevile nimeshtuka sana wakati Wabunge wengine wakipongeza kitendo cha Kamati kusikitishwa na jambo hili niliona Wabunge wengine wamenuna, isipokuwa tu walipotajwa Wanajeshi 15 ndiyo watu wakapiga makofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu binafsi imenisikitisha sana, ubaguzi wa wazi. Mbunge mwenzetu ameumizwa watu wamekaa kimya, hili jambo hatupaswi kulifumbia macho. Kwa sababu ya muda mdogo wengine watalizungumza, lakini hili ni jambo baya sana. Ninaiomba Serikali, sasa ni zaidi ya miezi mitano hakuna *suspect* hata mmoja! Tumeomba

Vyombo vya Kimataifa vitusaidie kuwapata hao watu, Serikali inakataa. Ni lini Serikali itatuambia kuhusu tatizo hili ambalo lilifanyika mbele ya macho ya watu juu ya mwenzetu aliyepigwa risasi. Hili ni jambo la aibu na hatupaswi kulifumbia macho katika Taifa letu, ni jambo la hovyoo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Heche juzi alizungumza hapa, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii ambayo tunachangia, kuhusiana na suala *e-passport* ambalo Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mwigulu alizungumza kwamba kilichoinduliwa siku ile ni *e-immigration*. Nataka nipate majibu halisi kwamba siku ile Mheshimiwa Rais alizindua *e-immigration* au ni *e-passport*?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tujue jambo hilo kiundani. Kwa sababu Serikali hii imekuwa ikijipambanua kwamba ni Serikali inayokomesha ufisadi, lakini kiundani kama Kambi ya Upinzani tunazo nyaraka za kutosha, ambazo tutaziweka wakati muafaka. Nyaraka za kutosha ambazo hazina mashaka juu ya ufisadi na harufu kubwa ya ufisadi ndani ya jambo hili katika Serikali hii ambayo inayojipambanua kwamba ni Serikali inayopingana na ufisadi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano; katika mkataba ambao waliingia kwenye *Memorandum of Understanding*, bei ya *passport* moja ilikuwa inagharimu *Pound* za Uingereza 6.84, lakini hii *e-passport* iliyozinduliwa inagharimu *Dollar* 68 na ndiyo maana bei ime-*shoot* kutoka Sh.50,000 mpaka Sh.150,000. Mkurugenzi anasema kwamba hii ni ya miaka 15 hata ya Sh.50,000 tuliyokuwa tunatoa ilikuwa ni ya miaka 15 *anyway*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, wananchi wa Watanzania hebu tuione hii Serikali inayojipambanua inakomesha ufisadi wakati kuna harufu kubwa na kwa kichaka cha Usalama wa Taifa. Pia niseme haya mambo ya kusema hela inayoenda Usalama wa Taifa Wabunge tusijue, hiyo siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tufuatilie nchi kama Israel, tufuatilie nchi kama Uingereza, Bunge tunayo haki ya kujua hela inayokwenda Usalama wa Taifa, isipokuwa hatuna haki ya kujua wanafanyaje ndani ya Usalama wa Taifa. Hata hivyo, kutudanganya kwamba tusijue hela inayokwenda Usalama wa Taifa ndiyo wizi unakopigiwa huko kwa kigezo cha kwamba haya ni mambo ya siri, masuala ya *passport* siyo mambo ya siri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na watu waliopewa kazi *Memorandum of Understanding* ni kwa nini walitolewa akaja akapewa mtu mwingine kinyemela nyemela? Hii ni hoja ya Mheshimiwa Heche....

## T A A R I F A

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza, anasema Serikali hii inajipambanua kuwa inapigana vita na ufisadi. Nataka nimpe mifano, aliyekuwa Mkurugenzi wa *NIDA* saa hizi yuko ndani, aliyekuwa Kiongozi wa *TFF* saa hizi yuko ndani, Wakurugenzi mbalimbali wako ndani saa hizi au anataka Serikali iingilie *CHADEMA* wanavyofisadi ruzuku ndiyo atajua Serikali hii inapigana vita na ufisadi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukicheza na nguruwe kwenye matope mtachafuka wote, lakini nguruwe atachekelea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumze ...

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Hebu muulize nguruwe ni yupi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jaku taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba rafiki yangu Mheshimiwa Msigwa, sisi Waislam afute kauli yake, nguruwe kwetu ni haramu, sasa ajue lugha ya kuitumia, kama kwake yeye sawa na tumo mchanganyiko humu ndani. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Msigwa unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka nizungumze Polisi wamekuwa wakisema kwamba tutii sheria bila shuruti, lakini Polisi ndiyo wa kwanza wenyewe kuvunja sheria. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, inamtaka Polisi akimkamata Mtuhumiwa ampeleke Mahakamani ndani ya masaa 24, lakini mimi ni shahidi nimekuwa mhanga wa kuingia mara nyingi Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *I am not criminal, I am a Politician*, lakini kuna watu ambao wameomba niwasemee na Mheshimiwa Waziri unasikia hapa, wamekaa ndani ya Kituo cha Polisi kwa mfano lringa Mjini, kabla ya *Christmas* miezi miwili wako ndani, hawatoi maelezo, hawapelekwi Mahakamani. Kwa nini tunawatesa watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mmezungumza hapa asubuhi nimeuliza swali la kupiga watu, Polisi wanapiga watu wanawavunja mpaka miguu, wanawaonea! Anakamatwa mtu hana makosa, amekamatwa mzima akifika ndani ya Kituo cha Polisi anapigwa, akipelekwa hospitali wanawaambia wasiwaandikie hata matibabu. Hii nchi tunaipeleka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine humu ndani

tunapozungumza masuala ya Polisi mnaona kama vile hakuwahusu, wengine hata hamna *legitimacy* ya kuongea masuala ya Polisi. Kwa sababu *you have never been there*, hujawahi kwenda Magereza, hujawahi kwenda Polisi, unajaribu kuchangia, unadhani labda hakukuhusu! Hata kina Mramba walidhani hakuwahusu, lakini siku moja walienda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya kule ndani ni ya hovyoy, Mbunge ambaye sina makosa nimechaguliwa na wananchi, natimiza majukumu yangu ya Kibunge ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa Peter Msigwa. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea sana, Mheshimiwa Msigwa amemaliza kuchangia, wataendelea Wabunge wengine.

Waheshimiwa Wabunge, ili kuzitendea haki Kanuni zetu, kwa sababu hili jambo linazungumzwa humu Bungeni ni mara ya pili sasa. Kama alivyosema Mheshimiwa Msigwa na hapo nyuma alizungumza Mheshimiwa Heche kuhusu ufisadi ulioko katika *passports* ama tuseme upande wa Uhamiaji kwenye hili zoezi zima la utoaji *passport* mpya ama mfumo mpya uliozinduliwa.

Kwa sababu Kanuni ya 63 inatutaka Waheshimiwa Wabunge kutokusema uongo Bungeni na kwa kuwa Mheshimiwa Heche alishazungumza na Mheshimiwa Msigwa amezungumza, sisi kama Bunge hatuwezi kuwa tunasikia habari za ufisadi tukazifungia macho. Kwa hivyo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maadili itusaidie sisi kama Bunge, Mheshimiwa Msigwa taarifa ulizonazo kuhusu ufisadi uliofanyika kwenye hili zoezi, uzipeleke kwenye hii Kamati.

Kamati itakuja ilishauri Bunge tufanye nini na huo ufisadi unaoendelea katika hayo maeneo. Kwa hiyo, naiagiza Kamati imwite Mheshimiwa Msigwa na namuagiza Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa apeleke huko hizo

nyaraka ili Bunge liweze kushauriwa na kuchukua hatua mahsusi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye taarifa hizi mbili ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti. Napenda niwashukuru Wenyeviti wamewasilisha taarifa zao hizi kwa weledi na umakini mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge la Tisa tulifanyiwa semina na watu wa Usalama wa Taifa, kuna mfano mmoja walileta wale watu wa Usalama wa Taifa, Kiongozi mmoja wa nchi hapa Tanzania amepelekewa zawadi ya *Qurani*, kitabu cha Mungu cha *Qurani* kapelekewa. Kwa kuwa ni Kiongozi mkubwa watu wa katikati waliingilia kuifungua kwanza ile *Qurani*, kumbe lilikuwa ni bomu tulioneshwa hapo. Sasa juzi Mheshimiwa Spika Mbunge mwenzetu amepigwa risasi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, Jenerali mmoja Mstaafu wa Jeshi kapigwa risasi hicho ni kiashiria kwamba silaha zipo 'bwelele' nchini kwetu. Zipo bwelele kwa sababu tuna changamoto nyingi sana, hali ya majirani zetu Sudan, Somalia, Congo vita iliyoko huko inafanya na mipaka yetu ipo *porous*, silaha nyingi zipo nchini hapa sana; pia utandawazi uliopo duniani; tatu, kukosa ajira kwa vijana wetu ambao wanarubuniwa na watu wanaopigana vita huko na kuwafundisha ugaidi. Hizi ni changamoto ambazo zinaonesha kwamba usalama wa Viongozi hapa Tanzania *is an issue of the sense* kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Bunge lichukue hatua madhubuti kuhakikisha Wabunge, Wabunge ambao ni baadhi ya Viongozi, Wabunge ambao hapa Bungeni tunaongea mambo ambayo yanawagusa wengine



huko nje ambao wana uwezo wao kifedha na kigaidi, wawekewe usalama. Usalama hapa Dodoma kwenye makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Kumi lilianzisha mchakato wa kuwa na...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 28(2), nakusudia kuongeza muda, kwa hivyo nitawahoji Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kumaliza shughuli zilizopo mbele yetu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda, kwa hivyo tutaendelea. Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa malizia muda wako.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema kwamba, naliomba Bunge lichukue hatua madhubuti sana kuhakikisha usalama wa Wabunge kwa sababu ni Viongozi. Kwa sababu mambo ambayo wanaongea Wabunge hapa ndani yanawagusa watu wengine huko nje ambao wana uwezo wa kifedha na uwezo wa kigaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Kumi lilianzisha mchakato wa kuwa na Kijiji cha Wabunge hapa, naomba wazo hilo liendeleo, nyumba zijengwe Wabunge wote wake sehemu moja ili waweze kupatiwa ulinzi. Huko kwenye Majimbo yetu Wabunge wapewe ulinzi kama anavyopewa ulinzi Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Wabunge magari yao yatambuliwe, yawe na namba ambazo zipo sawasawa na

zinajulikana kwamba huyu ni Mbunge wa Lupa, namba yake ipo pale, vinginevyo Wabunge wengi wataanza kupigwa risasi, Viongozi wengi wataendelea kupigwa risasi. Usalama wa Wabunge, usalama wa Viongozi wote nchini Tanzania sasa hivi ni *issue* ambayo ipo top of the agenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Lema. Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye. Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Kwanza niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa kazi nzuri wanayofanya, naomba nijikite kwenye ripoti ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inatekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa sasa na tumeshuhudia Rais Magufuli akitangaza kuongeza nguvu ya vita ya kiuchumi kwa nchi yetu ambayo ni jambo zuri sana, litaisaidia nchi yetu kutoka hapa ilipo, kwa sababu tumeshapata uhuru wa kisiasa ni vizuri tukapata uhuru wa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita hii na Diplomasia hii haiwezi kutekelezwa vizuri kama Taasisi yetu ya Usalama wa Taifa itaendelea kusimamiwa na sheria tuliyonayo inayoismamia Taasisi hii ya Usalama wa Taifa. Kwa muda mrefu, Taasisi hii imekuwa inashughulika na usalama wa Viongozi zaidi, kuliko kushughulikia usalama wa nchi kwa ujumla na hasa masuala yanayohusu uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko *scandal* mbalimbali ambazo zimekuwa zikitokea katika nchi yetu, ukianza kwenye *EPA, ESCROW, RICHMOND*, kwenye Madini na

Mikataba mbalimbali mibovu ambayo nchi yetu imekuwa ikiingia. Kwa muda mrefu mambo haya yakitokea tumekuwa tukishuhudia Wanasisa wakiadhibiwa na Watendaji ndani ya Serikali wengine wakiadhibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taasisi hii ingekuwa inatimiza wajibu wake kwa mlengo wa kulinda uchumi wa nchi yetu, maana yake ingefanya kazi ya kuzuia nchi yetu isiingie kwenye mikataba hiyo mibovu. Kwamba watu wanakwenda wanafanya utaratibu, wanachukua hela za EPA wanagawana, inakwenda kwa muda mrefu *unnoticed* halafu baadaye tunakuja kuambiwa unajua kuna watu walipiga hela mahali, halafu wanachukuliwa hatua hawa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo hiki hakinyooshowi kidole, hawaulizwi, hawasemi chochote, nadhani inawezekana sheria tuliyonayo inawafunga mikono kwa namna moja ama nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba Kamati yetu ingeleta mapendekezo, tupitie upya Sheria ya Usalama wa Taifa ili mikono yao iende mbali, wakumbuke jukumu lao la kuhakikisha wanalinda uchumi wa nchi yetu, katika kipindi hichi ambacho tunahama kutoka kwenye Diplomasia ile ya Siasa kwenda kwenye Diplomasia ya Uchumi muda mwingi wautumie huku, badala ya hivi sasa wanavyofanya kubaki tunasikiliza simu za watu, tunafanya mambo ambayo kimsingi nadhani hayalindi uchumi wetu na mwisho wake gharama yake inakuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani twende huko, sheria ile iletwe hapa, tuipitie tuone kama yapo mapungufu yanayowafanya tupelekwe huko tunakoenda, mwishowe tutabaki tunalaumiana kila siku, nchi yetu inaingia kwenye mikataba ya hovyoyote kila siku na wanaoumia na kuathirika wanakuwa ni wale waliopewa dhamana kwa maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaopaswa kushauri

tusiingie huko ni akina nani? Maeneo yetu ya bandari, *airport* na maeneo mengine, nilidhani eneo la kwanza nishauri umefika wakati tupitie upya Sheria ya Usalama wa Taifa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape muda wako umekwisha, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lema naomba ukae.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Naibu Naibu Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao; inasikitisha sana kushuhudia matukio yanayohatarisha maisha ya raia na mali zao na kusababisha hofu kubwa miongoni mwa wananchi. Mathalani, kumekuwa na kupotea kwa wananchi wengi katika maeneo mbalimbali kama vile kupotea kwa Ben Saanane na wengine. Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha inadhhibiti matukio haya.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, ulinzi na usalama wa Wabunge; kwa kweli inasikitisha sana kwa kuwa Wabunge hawana ulinzi wowote na hata maeneo wanayoishi hayana ulinzi wowote. Naomba Serikali ijifunze kutoka nchi nyingine namna Wabunge wanavyolindwa wao na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inasikitisha kuona Wabunge wanajilinda wenyewe na hii imehatarisha maisha ya Wabunge na hata kupelekea Wabunge hao kuvamiwa na kupigwa risasi mfano, Mheshimiwa Tundu Lissu, aliyepigwa risasi 38 hapo mwaka jana. Naiomba Serikali kuleta marekebicho ya Sheria ili kiingie kipengele cha kuweka walinzi

kwa ajili ya Wabunge, siyo hapa Bungeni tu bali hata maeneo wanayoishi Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kukamatwa Wabunge kwenye maeneo ya Bunge, kumekuwa na kamata kamata Wabunge kwenye maeneo ya Bunge. Huu ni udhalilishaji wa Wabunge, maana ya kinga za Bunge ni nini? Naiomba Serikali ilete marekebisho ya sheria kuheshimu maeneo ya Bunge ambapo Wabunge wana kinga pia askari wawe na heshima kwa Wabunge na hasa wawapo kwenye Majimbo yao, maana askari wanawadhilisha Wabunge. Mfano, mnamo tarehe 16 Novemba, 2017, Mbunge wa Viti Maalum alidhalilishwa na askari kule Kilolo Kata ya Kimala.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, mrundikano wa mahabusu na wafungwa; katika magereza mengi hapa nchini kuna mrundikano wa mahabusu ambao wakati mwingine hawana kesi yoyote, bali wanajaza magereza, mfano, Gereza la Njombe Mjini kuna mrundikano wa mahabusu, naomba kuishauri Serikali mahabusu ambao hawana kesi, kesi zao ziharakishwe kusikilizwa ili kuondokana na mrundikano wa wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa taarifa yake nzuri ya kipindi cha Februari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto hususan katika Kikosi cha Zimamoto kilichopo Mkoa wa Dar es Salaam kinawalazimisha wafanyabiashara waliopo karibuni Wilaya ya Ilala kununua mitungi ya gesi (*Fire extinguish*) kwa lazima na kuiweka ndani ya duka la kila mfanyabiashara. Mfanyabiashara asipotekeleza hutozwa faini, badala ya mmiliki wa nyumba kununua mitungi hiyo na kuiweka pembezoni mwa jengo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza je, ikiwa moto utatokea usiku na wakati huo mfanyabiashara ameshafunga duka, amelala nyumbani kwake, je mtungi huo uliopo ndani ya duka utamsaidiaje mfanyabiashara kuokoa mali zake? Je, hatuoni kuwa huu ni mradi maalum wa Kikosi cha Zimamoto na siyo kulinda mali za wafanyabiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu wafanyabiashara hao wanaelemewa na milolongo ya kodi nyingi na wakati mwingine kushindwa kuendesha biashara zake na kupelekea kufunga duka. Naomba Wizara husika isaidie kuondoa kero hii na kiuhalisia haina tija yoyote kwa mfanyabiashara ambaye anachangia pato la Taifa kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufinyu wa fedha hupelekea msongamano wa wafungwa magerezani na pia kuna uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania. Naomba Serikali itenge fedha za kutosha na kwa wakati ili kupeleka katika Wizara husika kuondoa tatizo hilo. Mwisho nakupongeza Mheshimiwa wa Kamati Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu kwa taarifa yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kuhusu Maafisa kupelekwa Ubalozini. Napendekeza kuwa kwa kuanzia Serikali ingepeleka Maafisa maeneo ya kimkakati hasa nchi za South-East Asia kama Korea, China na pia nchi au vituo ambavyo ni *multiple* kama Sweden au Ujerumani ambako Ubalozini unafanya kazi nchi zaidi ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kupendekeza umuhimu wa kufungua ubalozi mdogo kwa kuanzia Lubumbashi na Guangzhou. Jambo hili ni muhimu hasa ukizingatia biashara iliyopo katika ya nchi yetu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza na naunga mkono taarifa ya Kamati. Ningependa kuongelea juu ya msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani yamefikia mahali pa kuvunja haki za binadamu kwani inafikia mahali wafungwa na mahabusu kushonana kama vijiti vya kiberiti, kitu ambacho hukupelekea wafungwa kukosa haki ya msingi ya kulala na pia kuambukizana magonjwa. Msongamano huu pia umesababisha Serikali kutumia fedha nyingi kuwahudumia. Ningeshauri ugeuzwe kuwa nguvu kazi ya uzalishaji hivyo kuzalisha vyakula au huduma itakayoongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishauri Serikali inapopeleka mabalazi nje iangalie uwakilishi bora wenye tija wa kutangaza na kutafuta fursa za kiuchumi, kwani Mabalazi ndio wanaotarajiwa kuiiza nchi yetu kimataifa. Nishauri Serikali kufanya upimaji wa kazi zilizofanywa na balazi ili kutathimini iwapo kuna haja ya balazi huyo kuwepo huko kwenye uwakilishi wa Serikali katika nchi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kuangalia pya juu ya watoto wanaozaliwa magerezani, wasiishi maisha ya ufungwa ya mzazi. Serikali itafute njia ya kuwalea watoto hao na kuwapa haki za msingi za watoto ili wasijione nao kama wafungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kuwajali wafungwa wenye ulemavu na wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa kuwapa lishe bora pia kuwakinga na magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kuangalia upya mpango wa ulinzi wa Wabunge ambao wamekuwa wakikamatwa kwenye maeneo ya Bunge kinyume na kanuni za Bunge, hivyo suala hili limekuwa kero sana kwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kuwahisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati, nashauri Serikali itambue uhitaji wa Wizara hii kwani ni nyeti sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali kuboresha nyumba za askari magereza kwani zina hali mbaya sana, zinapunguza morali ya kazi kwa askari hao.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maoni ya Kamati yakizingatiwa na Serikali ikayafanyia kazi, kutokana na changamoto zilizopo kupitia zoezi zima la vitambulisho vya Taifa pamoja na Serikali kutumia pesa kwa ajili ya kutengeneza vitambulisho hivi (*NIDA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara kuiwezesha *NIDA* au kuharakisha kuipatia fedha *NIDA* ili wananchi ambao hawajapata vitambulisho mpaka sasa waondokane na usumbufu huu tukielekea kwenye *electronic system* kuhusu usajili wa wageni katika mfumo ili kujua kama wanaishi kihalali nchini. Katika zoezi hili Serikali isimamie kwa umakini usajili huu ili kuondoa malalamiko ya wageni kupata vitambulisho vya Taifa na *passport* kabla ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi hili la usajili wa vitambulisho hususan wananchi wa mikoani inaleta usumbufu kusafiri kufuata mikoa yenye huduma hii kama Dar es Salaam na kuwaongezea gharama wananchi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuweka ofisi kila wilaya ili huduma za vitambulisho ifanyiike kila wilaya nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu kubwa la Serikali kuangalia masuala yote yanayohusiana na siasa kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, askari wetu wanajeshi wamekuwa wakichukuliwa kwenda kutuliza ghasia katika nchi zenye vita na ghasia na askari wetu wamekuwa wakipelekwa kutuliza ghasia lakini wakipoteza maisha na kufa Serikali imekuwa ikichukua pesa kuzilipa familia kama rambirambi, lakini baada ya kumaliza msiba mnazitelekeza familia hizo na kuziacha zikiteseka. Je, Serikali ni kwa nini inashindwa kuendelea kuzisaidia familia zao ilihali walikufa vitani huku wakilinda mipaka yetu na kulinda mahusiano ya kidiplomasia? Serikali inalichukuliaje suala hilo ambalo



linasababisha askari kuogopa kwenda kulinda amani nje ya Tanzania kwa sababu mnawatelekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la usajili wa vitambulisho (*NIDA*); hivi sasa wapo katika baadhi ya mikoa na zoezi hili linasababisha foleni na msongamano katika ofisi za usajili. Malalamiko ya wananchi ni kutozwa Sh.2,000 katika zoezi hili; je, Serikali haioni kuwatoza wananchi Sh.2,000 na wananchi ni maskini hawawezi kulipia gharama hizi katika mchakato wa kupata vitambulisho? Serikali inawasaidiaje wananchi maskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika Balozi mbalimbali nchini; pamoja na juhudi za Serikali kupeleka Mabalози na watumishi katika nchi wakilishi, kuna changamoto, kwa mfano, katika balozi Nchini China (Beijing), kuna watumishi wachache na bado malipo yao yanachelewa, uchakavu wa majengo na asilimia kubwa tumepanga, mfano, Balozi Zimbabwe na watumishi kujibana katika ofisi. Je, Serikali haioni iko haja kuwapatia fedha ili wafanye kazi pamoja na kuweza kutafuta fursa za kiuchumi?

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa kina kabla ya kutoa adhabu kwa Wabunge; kumekuwa na adhabu mara kwa mara kwa Wabunge na hasa Wabunge wa Upinzani, nimekuwa nikijiuliza ni kwa nini? Nimegundua kuwa Wapinzani wanapoonaa mambo fulani yanakwenda isivyotegemewa au bila haki kutendeka ndio maana inawafanya kupata hasira na kuropoka au kutenda vitendo kinyume na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba kuishauri Serikali kuchunguza ni kwa nini mambo haya yanatokea. Serikali ikitenda haki na usawa na ikiwasikiliza hasa yale wanayoshauri kwa manufaa ya Taifa, watu hawataweza kutenda matendo kinyume na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa adhabu; naomba Wabunge waliopata adhabu mwaka jana walipata adhabu ya muda mrefu mno. Naomba adhabu zipunguzwe maana Wabunge wanakosa uwakilishi kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upendeleo; katika kupeleka watu kwenye maadili wanapelekwa wa upande mmoja, ni wale wa kutoka Upinzani tu. Mara nyingi nimesikia maneno ya kuudhi kutoka upande wa Chama Tawala hawachukuliwa hatua yoyote. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kwamba Uongozi wa Bunge uendele kutoa elimu na maelekezo juu ya taratibu za Bunge ambazo zitasaidia Wabunge kutambua wajibu wao. Pia nishauri Uongozi wa Bunge kuweka Semina zitakazowaelimisha Wabunge kujua ni yapi mambo ambayo hayatakiwi Mbunge kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vilevile uongozi wa Bunge kabla ya Mbunge kupewa adhabu aitwe aonywe na apate muda wa kujieleza ili haki ipate kutendeka.

Hata hivyo, naomba nishauri kuwa Uongozi ujaribu kufuatilia tabia za Waheshimiwa Wabunge ili kutambua tabia zilizojificha kwa Wabunge hao ili wapate kusaidiwa mapema kabla hawajatenda makosa ambayo yanaweza kuathiri utendaji wa kazi zao za Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nishauri Kamati ya Maadili inaposhughulikia masuala ya Wabunge iweke weledi mbele na iwachukulie wakosaji wote sawa bila kuweka upendeleo wa aina yoyote. Pia nashauri adhabu zinazotolewa ziangaliwe zisiwe zile ambazo zinadhaliisha au kuathiri utendaji wa Wabunge husika kwani wametumwa na wananchi kuwawakilisha hivyo adhabu yoyote ile isiathiri uwakilishi wao.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia taarifa hii ya Kamati ambayo imetupa picha ya namna sisi kama Wabunge kujua wajibu na haki zetu na mchakato wa kutunga kanuni za maadili ndani ya Bunge. Muda ni finyu sana ambao umekuwa unatengwa tunapotunga sheria hizi na kupelekea Wabunge wasio na taaluma kupitisha kanuni ambazo baadaye huzilalamikia kanuni kuwaumiza hivyo muda uongezwe, hautoshi.

Kupitia kanuni hizi na lengo la Kamati hii katika suala la kutoa adhabu kwa Wabunge, kwa malalamiko ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba Kamati hii iko haja ya kutoa muda kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge kwa undani kabla ya kutoa adhabu ambazo kimsingi ukisoma taarifa ya Kamati inalenga kwa asilimia kubwa kuwapa adhabu Wabunge wa Upinzani kuliko wa CCM.

Je, kupitia Kamati hii na malalamiko ya Wabunge, ni kwa nini kila siku adhabu zinatolewa kwa Wabunge haohao kila siku majina yanajirudia, hamuoni kuwa Kamati ya Maadili badala ya kuhakikisha Wabunge wanapata elimu ya maadili na msikimbilie kutoa adhabu ambayo inapelekea kuleta chuki na sio kufundisha kama lengo. Hivyo, Kamati ya Maadili ione namna ya kuongeza semina kwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upendeleo Bungeni, Kamati ione haja ya kuchunguza jambo hili ili likawe Bunge lililotukuka katika ujenzi wa Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa tutaanza kusikia wachangiaji upande wa Serikali, Mheshimiwa Angelina Mabula.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kwa kupata fursa hii na niwapongeze pia Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya. Ninazo hoja mbili tu ambazo nataka kuchangia kutoka kwenye hii Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Jambo la kwanza, linapatikana kwenye ukurasa wa 21 inalozungumzia suala la alama za mipaka. Suala hili kidogo limekuwa na tatizo na changamoto lakini nilitaarifu Bunge lako kwamba sasa Wizara imepata pesa tumepewa bilioni nne kwa ajili ya kuhakiki mipaka hiyo na kazi zinazokwenda kufanyika ni kukarabati zile *pillars* zote za zamani ambazo zimechakaa lakini pia na kuweka *pillars* mpya ambapo hapakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu pia zilikuwa na umbali mrefu sasa hivi tutakwenda kuweka umbali wa mita 100 kutoka *pillar* moja mpaka nyingine ili iweze kuonekana na hii inakwenda kufanyika kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda pamoja na mpaka wa Tanzania na Kenya kazi hizo zinaenda kufanyika.

Lakini pia kazi nyingine itakayofanyika ni kuwa na ile ramani ya msingi kwa maana ya *base map* ili kuweza kutambua vilivyoko pale ardhini ikiwa ni pamoja na kusafisha ule Mkuza ulioko pale, kazi hiyo inakwenda kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapakuwa pia na *protocol* ya mpaka pale itakwenda kufanyika mwaka huu kwa sababu pesa tulizokuwa tumeweka kwenye bajeti zote zimetolewa na tunaishukuru Serikali kwa kazi hiyo.

Jambo la pili, ni mgogoro wa mipaka ambao umekuwepo katika taasisi nyingi za Jeshi.

Napenda kushukuru sana Wizara ya Ulinzi ambayo iliunda kamati ambayo imepitia katika mipaka mingi inayohusiana kati ya Jeshi na wananchi na wamehakiki mipaka yao yote na maeneo ambayo walikuwa wakiyahitaji wanaendelea nayo na yale ambayo walikuwa hawayatumii na hawayahitaji basi yale watakuwa wameyarejesha baada ya kuwa wameshakamilisha taarifa yao. Lakini kubwa zaidi ni kuzikumbusha taasisi zote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa dakika tano.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja zilizoko mbele yetu hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki hii kutakuwa na matukio mawili muhimu ya sehemu ya mahusiano ya kimataifa tuna mechi mbili za mpira kati ya Timu za Tanzania na timu kutoka Seychelles na kutoka Djibouti. Sasa Mheshimiwa sijui kuna kitu nafikiri kiliongelewa hapa maana kwenye simu yangu nakuta kila mtu ananiuliza kwamba kuna tatizo na tumefanya upendeleo kwa timu ya kimataifa kufanya mazoezi kwenye uwanja wa Taifa, lakini timu ya hapa Tanzania haijapewa nafasi kufanya.

Ningeomba nitumie fursa hii kwa sababu ni mambo ya *foreign affairs* haya niweze kuitolea ufafanuzi kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote mnajua tu kwamba tumefanaya ukarabati mkubwa wa kiwanja chetu uwanja wetu wa Taifa mwaka huu majuzi tu, tumekamilisha baada kiwanja hicho kutuhudumia kwa zaidi ya miaka 10 na ukarabati tulioufanya vilevile nyasi tulizoweka pale zinategemea zitahudumia kwa zaidi ya miaka 10 na ili ziweze kufika miaka 10 kuna masharti yake, haturuhusiwi hicho kiwanja kukitumikisha kikabeba michezo zaidi ya mitatu kwa wiki moja, ukifanya hivyo unaingiza uswahili na hata ikiharibika mapema huwezi hata kwenda kudai mtu aliye ku-*gurantee* kwamba kita miaka 10.

Kwa hiyo, wiki hii tuna mechi mbili muhimu; kesho wanaingia *Young Africans* wanashindana na timu kutoka Seychelles na kesho kutwa wanaingia Simba na timu kutoka Djibouti. (*Makofi*)

Kanuni za kimataifa zinataka timu ngeni hiyo ya kimataifa lazima ifanye mazoezi kwenye hicho kiwanja

kitakachofanyiwa mechi na vilevile FIFA inatambua kwamba hiki kiwanja ni cha timu ya hapa nchini kwa hiyo uwanja wa Taifa ni uwanja wa Yanga, uwanja wa Simba unategemewa ujue uwanja wako sasa wale wengine hawajajua ndio maana wanaopewa *priority* kuweza kufanya mazoezi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tuna mechi mbili na kwa sababu tunaruhusu hawa wageni kufanya mazoezi pale ambao ni lazima kwa hiyo tutakuwa tumekiuka tayari tuna michezo minne ndani ya wiki moja. Na usisahau wiki hii Azam na Simba wamecheza uwanja huo huo, kwa hiyo mara tano, uswahili umeanza kuingia katika uwanja wetu wa Taifa.

Mimi nashukuru kwa haya maneno niliyoyapata nadhani kuna vijana wangu pale wanahitaji kwa kweli wadhibitawe, utaruhusuje mechi tano katika uwanja huo ambao utarudia mara tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kufafanua tu kwamba ni haki ya wageni kupewa nafasi na sisi tuweze kutumia viwanja vyetu na naniombe nitoe rai na wito kwa wapenda mpira hapa, timu ya Yanga ina umri wa miaka 83 timu ya Simba ina umri wa miaka 82 timu zetu sasa zifike muda nazo zijenge viwanja vyake. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa nadhani huo ujumbe umeshafika, Mheshimiwa Kandege dakika mbili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa na Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika mbili nyingi sana kwangu kwa sababu nategemea kutoa ufafanuzi kwenye

eneo moja tu nalo liko ukurasa wa 38 ni kuhusiana na ubovu wa barabara za mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo sisi kama Taifa tumekuwa tukiweka vipaumbele kwa barabara ambazo zinaunganisha Mikoa, lakini pia kuna umuhimu mkubwa sana kwa barabara za mipakani na hasa barabara yetu ya kwenda Uganda kule kwa kupitia chombo chetu cha *TARURA* tutahakikisha kama Serikali ukarabati unafanyika ili barabara hii iwe nzuri iweze kusaidia katika shughuli nzima za kulinda mipaka yetu, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Mkuchika.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hiyo na kwa ajili ya muda niende kwenye mambo makubwa tu yanayohitaji ufafanuzi, yale mengine yaliyo ya maoni niseme tu tumeshapokea maoni hayo tutayafanyia kazi kiutawala kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja hii ambayo ilikuja kama swali anayoisemea Mheshimiwa Msigwa kama Mheshimiwa Rais alichozindua ni *e-passport* ana ni *e-immigration*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lilirudiwa kukosewa hata siku ile Mwenyekiti wa Kamati husika aliposema na niliona Wabunge wakishangilia wakisema kwamba tungeanzia kuzindua *e-immigration* ndio tuzindue *e-passport*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *e-immigration* ni *set* na hivi vingine tunavyoendelea navyo ni *subset* za *e-immigration*, so *the whole system* ni *e-immigration* ndani yake kuna *e-passport*, kuna *e-visa*, kuna *e-permit*, kuna *e-gate* kwa maana hiyo Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ile aliyosema anashangaa kwa nini tumezindua *e-passport* badala ya *e-immigration* ni *confusion*, *is a total confusion* kwa sababu *e-*

*immigration* hamna sehemu utaenda kuishika kwamba hii ndio *e-immigration*. Lakini tunachosema...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba utusaidie kwa sababu jambo hili limesha pelekwa kwenye Kamati ili nyaraka zipelekwe huko, mimi ningeomba ujielekeze kwenye mambo mengine kwa sababu hili tayari tutaletewa ufafanuzi na kamati mahsusii.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, lakini kuna mambo ambayo yalikuwa ya Wizara kwa mfano anaposemea hii ilikuwa inauzwa *pound* nane hii ni dola 68. Dola 68 hii siyo *arrangement ya supplier*, hii ni bei ya *immigration* ambayo sisi kama waendesha mradi tuna amri ya kutoa *passport* bure kama tunavyotoa kitambulisho cha Taifa ama kuuza, kwa hiyo tumepiga hesabu tukaona hii tunatakiwa tuuze ili kuweza kutengeneza maduhuli lakini pia na ku-*cover* gharama za mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa umetolea maelekezo na mimi wakati wa kusimama nilikuwa natamani nimwambie Mheshimiwa Msigwa aweke hizo nyaraka leo leo lakini mmempa muda mrefu zaidi basi ngoja aende kwenye hiyo ya muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye hili la ulinzi wa Waheshimiwa Wabunge, hoja ya viongozi kupewa ulinzi ni hoja ya msingi na sisi kama Serikali hatuwezi tukapingana na hoja ya ulinzi kwa viongozi na hoja ya ulinzi kwa wananchi ni hoja ya msingi ambayo sisi kama viongozi hatuwezi tukapinga hoja ya ulinzi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini jambo moja tu ambalo naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kuna miundombinu ambayo lazima iwe imefanyika katika nchi ili uweze kufanya ulinzi wa Mbunge mmoja mmoja. Kwa mfano kwa hapa Dodoma sisi tayari tulisha kubaliana na Kamati na tulikubaliana na tulitoa taarifa kwamba maeneo wanapokaa Wabunge tutaimarisha doria punde Wabunge wako hapa, na maeneo ambako kuna Wabunge



wengi wanakaa kwa pamoja tutaweza kutengeneza utaratibu wa askari ambao watakuwa katika maeneo hayo ama kwa njia ya doria ama kwa kuwaweka katika *station* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utaratibu wa kuwa na ulinzi kwa Mbunge mathalani kwa kila jimbo ni jambo ambalo linahitaji miundombinu kwanza kabla hujaweka utaratibu huo. Lakini hata hapa kuna maeneo mengine ambako Wabunge wanakaa. Kwa taratibu za kiusalama lazima utengeneze miundombinu kwanza kwa sababu si kila eneo unaweza ukam-*station* askari, unaweza ukamuweka kwenye *risk* ya kushambuliwa hasa katika maeneo ambayo watu wangeweza kutaka hata kuchukua silaha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo wazo kama hilo kufika Serikalini ni jambo jema, ni wazo ambalo ni la kitaifa na sisi tungeomba Wabunge waelewe kwamba jambo hilo linahitaji miundombinu kwanza kabla hujaweza kupeleka ulinzi katika eneo hilo. Kwa mfano nchi zingine ambako wanafanya ulinzi wa aina hiyo, Mbunge akishachaguliwa kuwa Mbunge hakai eneo alikokuwa anakaa, anakaa wilayani kama mkuu wa wilaya anavyokaa na kwa namna hiyo unaweza ukasema hili ni eneo la viongozi unaweza kupeleka ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwetu sisi katika nchi yetu utaratibu huo haupo na hata sheria yake haipo kwa maana hiyo kama jambo hilo litakubalika kama Taifa kuna miundombinu mingi sana ambayo inatakiwa ifanyike na hiyo ndiyo ingeweza kuwa njia njema ya kulifanyia jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nizitakie kila la heri timu zinazocheza *weekend* hii hasa Simba kwasababu mara ya mwisho Simba kushiriki mashindano haya Zitto Kabwe alikuwa bado yuko CHADEMA. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mkuchika tutamalizia na Mheshimiwa Mwinyi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kueleza hoja moja tu, baadhi ya watu mmezungumza juu ya utendaji kazi wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kama ifuatavyo, ukijua kazi inayofanywa na Idara ya Usalama wa Taifa yale mliyoyazungumza humu ndani msingeyazungumza, ninayo sheria hapa ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1996 nataka nikusomeeni kwa mujibu iliyopitishwa na Bunge, nataka nikusomeeni kazi za Idara ya Usalama wa Taifa, ukizisikiliza hayo yote mliyoyasema hayahusiani na Idara, fulani kapotea *police case*, fulani kaumizwa *police case*, haihusiani na Idara ya Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifupi kazi ya Idara ya Usalama nchi yoyote ni kutafuta habari na kuishauri Serikali. Nitasoma nitakusomea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto na Wabunge hapo tafadhali mwacheni Waziri ajibu, mkianza kujibizana hapo hatutafika mahali, mwacheni Waziri azungumze.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Nasema imeandikwa kiingereza Mimi nitasema kwa Kiswahili kwa sababu ili Watanzania wanaosikia waliopo hapa wote tupate uelewa mmoja kifupi ninachotaka kusema hoja mlizozitoa kuhusu Idara hazihusiani na Idara, hoja mlizozitoa kuhusu Idara haishauri Serikali mambo ya uchumi, haifanyi nini, haifanyi nini hamna ushahidi, katika nchi zote duniani Idara ya Usalama inatafuta habari nakuishauri Serikali yake kimya kimya *(Makofi)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana hakuna nchi utasikia msemaji wa Idara ya Usalama wa Taifa kasema hili, kasema hili, hakuna kitu kama hicho, kwa hiyo unaposema Serikali hawakuishauri unao ushahidi?

Sasa Sheria inasema hivi; *“Subject to the control of the Minister the functions of the service shall be”* shughuli zimewekwa nne;

(a) *to obtain, correlate, and evaluate intelligence relevant to security* (kukusanya habari, kutafuta habari na kuzifanyia tathimini) wanapofanya hayo hawayafanyi kwenye mkutano wa hadhara.

(b) *To cooperate as far as practicable and necessary with such other organs of state* (kushirikiana na vyombo vingine vya Idara zinazoshughulikia na usalama wa nchi), mna ushahidi hawana ushirikiana nao.

La tatu, linasema; *to advise Ministers, where the Director-General is satisfied that it is necessary to do so* (kuwashauri Mawaziri, kuishauri Serikali).

La nne, inasema *to inform the President, and any other person or authority which the Minister may so direct, of any new area of potential espionage, sabotage, terrorism or subversion.* Haya yote haya mambo ya kuhujumu uchumi ya nini, nini yanafanywa kimya kimya hakuna nchi inaita mkutano wa hadhara na kusema jamani tumevamiwa, hakuna nchi inaita mkutano wa hadhara na kusema tumefanya hivi, tumefanya hivi ninaomba Waheshimiwa Wabunge...

Mdogo wangu Zitto nakuheshimu sana, nimepewa mimi nafasi ya kuongea, ulipewa nafasi ya kuongea, hivi kwa nini mna-*disturb* wenzenu wakisema.

Sasa nataka kusisitiza ifuatayo, ....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Zitto Kabwe mara ya mwisho unazungumzishwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Sasa kwa sababu ya dakika tano nataka nifunge pia kwa haya maneno yamo

ndani ya sheria inasema hivi; *"It shall not be a function of the service (haitakuwa shughuli ya Idara ya TISS) (a) to enforce measures for security;* mambo ya mabavu mabavu kushika, kumkamata huyu haitakuwa kazi yake. *(Makofi)*

(b) Inasema; *to institute...*, sikilizeni nikupeni darasa. *(Makofi)*

(b) Inasema haitakuwa shughuli ya Idara *to institute surveillance of any person or category of persons by reason only of his or their involvement in lawful protest,* haitakuwa kazi ya Idara ya Usalama wa Taifa kumchunga chungu mtu, kumfuata fuata imo ndani ya sheria. *(Makofi).*

Kwa hiyo, kifupi ninachotaka kusema ndugu zangu, tukitaka kusema mambo mazuri yanafanywa na Idara hii mashahidi ninyi mimi nataka kutoa mfano, palikuwa na kilio mahala palikuwa kuna msiba, watu waliofiwa wamenuna, wakataka kumpiga kiongozi wa chama, wakamwambia wewe ndiye umesababisha mtu wetu afe, alitoroshwa na watu wa Idara ya Usalama nini hamjui? *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, tatizo mkiambiwa yale mnayoyajua yanayowauma mnapiga kelele.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, shukrani. Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Mheshimiwa Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Nakushukuru. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie hoja na hususani nitajikita katika Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama. Kwanza niipongeze Kamati kwa kazi nzuri

wanayoifanya na niwashukuru kwa ushirikiano wanaotupa mimi pamoja na watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizotolewa ya kwanza ni kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini na kuna athiri ufanisi katika utendaji. Tunakiri mpaka sasa hivi sera hiyo haijapatikana lakini nataka niseme kwamba sera hiyo tayari rasimu yake ipo imekwama katika jambo moja dogo nalo ni maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nilipata nafasi ya kuzungumza na Waziri mhusika kule Zanzibar akaniambia kwamba tayari wanajipanga kwenda kujadili katika Baraza la Mapinduzi ili hatimaye waweze kutufikishia maoni yao na baada hapo itafuata utaratibu uliobaki ili tuwe tuna sera ya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Angelina Mabula kwa kulijibu lile suala la *beacons* za mipakani kama mlivyosikia kazi imeanza kufanywa na vilevile nimpongeze Mheshimiwa Kandege kwa kujibu hoja za barabara za mipakani jambo hilo litashughulikiwa na TAMISEMI na tuna imani kwamba barabara hizo zitapatika ili ulinzi uweze kufanyika vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni ya Shirika la SUMA JKT, ni kweli kuna madeni mengi kuna madeni ya matreka, kuna madeni ya huduma zinazotolewa na *SUMA Guard* ya ulinzi kuna madeni ya mbegu zinazozalishwa na SUMA na kuuzwa katika taasisi mbalimbali. Lakini hatua zimeanza kuchukuliwa za kukusanya madeni hayo tulikuwa tunawa andikia barua lakini sasa hivi tume-*engage* kampuni za ukusanyaji wa madeni ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa na fedha hizo zipatikane ili SUMA jjiendeshe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa wanajeshi na migogoro ya ardhi kwa ujumla, nataka hapa niseme Waheshimiwa Wabunge ipo dhana kwamba Jeshi lina maeneo makubwa

ambayo hayatumiki. Nataka nisemie hivi kwamba jeshi lina maeneo makubwa kweli lakini yalichukuliwa kwa sababu maalum. Yako maeneo ya Jeshi kambi za Jeshi ambazo kazi zake ni utawala na *logistic*, lakini kuna kambi za mapigano, kuna vifaa vya milipuko, kuna kambi za mapigano, kuna vifaa vya milipuko, kuna kufanya mazoezi ni lazima wawe na maeneo makubwa.

Kwa hiyo, ninachosema hapa ni kwamba watu wasidhani kwamba kuna mapori wakadhani hayahitajiki wakavamia hiyo sio sahihi kwa sababu pale wanafanya mazoezi. Kambi zote lazima zifanye mazoezi, kwa maana hiyo ni kwamba maeneo makubwa yanahitajika jeshini na wananchi waelewe hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa wale wananchi waliovamia tungewataka na pamoja na nyinyi Waheshimiwa Wabunge niwaombe kwamba isiwe kawaida ya Wabunge kutetea upande wa wananchi peke yake, kwanza tuangalie tuhakikishe kwamba wananchi wana haki. Yako maeneo mengi wananchi ndio wamevamia maeneo ya jeshi, na ninyi mnatambua, kila kwenye Kambi ya Jeshi kwa sababu kuna huduma kuna afya pale, kuna shule pale, kuna maji pale wananchi wanakuwa haraka kuja karibu na wengine huwa wanalima katika maeneo yale. Kwa hiyo, tunaomba kwa sasa tuhakikishe kwamba wale wananchi ambao hawana haki ya kuwa katika maeneo hayo waondolewe na ndugu zangu mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa wale wanaodai fidia, kweli kuna maeneo ambayo Jeshi limetwaa tutahakikisha kwamba wanalipwa na haki zao watazipata na kwa kadri ya uwezo wa kifedha tutaendelea kulishughulikia suala hili ili wananchi wale waweze kupata haki zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ili ahitimshe hoja yake.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia na Waheshimiwa Mawaziri kwenye hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge 10 wamechangia kwenye hoja hii, watano kwa maandishi na watano kwa kuongea na Mawaziri, nawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Rhoda Kunchela, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Zainabu Amiri, Mheshimiwa Mary Muro na Mheshimiwa Cosato Chumi. Mengi ambayo wameongea ni maoni ambayo tutayapeleka Wizarani kwa ajili ya kushughulikiwa na kwa mfano Mheshimiwa Rhoda amezungumzia mambo ya vitambulisho kwamba *NIDA* waweze kupewa uwezo waweze kutoa vitambulisho kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Waziri wa Mambo ya Ndani yupo hapa tutampa hiyo hoja na Mheshimiwa Lucia Mlowe amezungumzia mambo ya *crime* ambayo matukio ya kupotea watu ambayo nimeyazungumzia kwa kirefu sana na kuwataka polisi basi hao watu ambao wanapotea na kutekwa na watu wasiojulikana basi wajitahidi kuhakikisha kwamba hao watu wanaofanya vitendo hivyo wanajulikana na wanakamatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukamatwa Wabunge ndani ya Bunge limeshughulikiwa vizuri na sasa hivi nafikiri polisi wana hayo maagizo kwamba ni lazima waripoti kwa Katibu wa Bunge kabla ya kuendelea kutekeleza hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la ucheleweshaji wa kesi ambayo limezungumzwa kwa kirefu na kwenye taarifa yangu/kwenye hoja yangu nimeeleza mbinu mbalimbali ambazo kamati imeona Jeshi la Polisi inatakiwa zichukue ili kuharakisha upelelezi wa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zainabu amegusa mambo ya kuongezewa zimamoto nyenzo na kuweza kulipwa kupewa fedha kwa ajili ya maendeleo kama ambavyo tumezungumza kwenye hoja yangu. Mheshimiwa Mary Muro kazungumzia msongamano wa Mahabusu na Wafungwa ambao ameuzungumzia kwa uchungu lakini na kwenye taarifa yetu, kwenye hoja yetu tumeelezea na kuwataka Serikali kuhakikisha kwamba basi kesi ambazo ziko Mahakamani zinasikilizwa kwa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Cosato Chumi ameshauri ufunguzi wa Balozi mbalimbali kule Lubumbashi na Guangzhou, China ambapo kwa kweli kwenye Kamati tumelizungumzia suala hili kwa makini sana na kumshauri Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa aweze kulichukua suala hili, kwa sababu hizi sehemu ni sehemu za biashara. Lubumbashi Watanzania wengi sana wanakwenda kwa ajili ya kufanya biashara, pamoja na Guangzhou wanakwenda wengi sana ni lazima tuwe na Balozi ndogo kwenye hizo sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watano wamechangia kwa kuongea tukianza na Mheshimiwa Katani ambaye amezungumzia suala la ulinzi wa Wabunge ambaye ame-*support issue* hiyo akihusisha na kupigwa risasi kwa Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba kwenye ile hoja yangu kwenye taarifa hiyo nimeongea kwa kinaga ubaga kwamba kuna suala la mlinzi na kuna suala la ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesisitiza sana suala la ulinzi, Jeshi la Polisi ni lazima lihakikishe kwamba basi linatoa ulinzi kwa Waheshimiwa Wabunge kwenye makazi na kwenye maeneo ambayo wanaishi. Haina maana kwamba watoe mlinzi, kwa hiyo kuna mbinu mbalimbali ambazo wanazotakiwa kufanya kama kufanya doria na kadhalika, kama ambavyo ameelezea Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa suala la usajili wa gari nimelieleza kwa ufafanuzi mkubwa kama mamlaka inahusika itaridhia basi ingekuwa ni vizuri ili usajili wa magari ya Wabunge basi yaonekane kama ni MB *so, so, so* au Viti Maalum *so, so!* Kwa hiyo, suala hilo ni la muhimu isipokuwa hapo ni lazima Wabunge waangalie kwamba gari gani hiyo ambayo unataka kuiwekea inazunguka na bendera. Kwa hiyo ni lazima uangalie na nafikiri taratibu zingine zitafuatwa namna ya kushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma ametaja mambo ya amani na ulinzi ambayo kwa kweli ni Jeshi la Polisi linatakiwa liongezewe tu nyenzo na fedha ili liweze kukabiliana na uhalifu mbalimbali ambao unatokea hapa nchini.

Mheshimiwa Msigwa ametaja tukio la Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba waliomba vyombo vya kimataifa vije kuchunguza tukio hilo, lakini ninavyofahamu ni kwamba ni lazima pana *conditions* zake kabla ya kuleta vyombo vya kimataifa. Ukianzia kwanza na tukio lenyewe, hilo kosa lenyewe linakuwa *regarded* kama nini, ni *international crime*, ni *organize crime* au ni *domestic crime*. Sasa na hawa wapelelezi ambao unataka kuwaleta je, tuna mahusiano nao kwa kinchi. Kwa hiyo, ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe na sio kuwaleta wapelelezi kutoka nje kwa kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *immigration* mimi niliwakilisha kamati kwenye kupokea *passport* mpya hizi za *e-immigration* sasa na Mheshimiwa Rais pale alisema kabisa kwamba wamejaribu kuokoa kutoka kwenye wajanja walikuwa wameweka bilioni 400 pale lakini wametengeneza huo mradi wa hizi *passport* mpya kwa bilioni 50. Sasa hebu angalia hapo ni kiasi gani fedha ambazo zimeokolewa. Lakini nachosema hivyo ni kwamba sasa sidhani kama hizo taarifa ambazo anazo Mheshimiwa Msigwa zina ukweli kiasi gani kwa sababu mpaka Mheshimiwa Rais atangaze pale sidhani kama watu wanaweza wakampa taarifa ambazo ni za uongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linakuja kwenye kamati yako, kwa hivyo nyinyi ndio mtakuja kutuambia kama nyaraka zipo zinazoonyesha ufisadi ama hapana. Kwa hiyo, ningekuomba ujielekeze kwenye hoja nyingine ili hii nyingine itakapokuja kwako uweze kuitendea haki. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwambalaswa ameelezea usalama wa Wabunge ambao nimeshaufafanua kwa kirefu lakini amesitiza suala la ujenzi wa nyumba za Wabunge kwa sababu tuko Dodoma hapa Wabunge ni lazima watakuwepo kwa hiyo, ni muhimu sana Ofisi za Bunge zikafikiria namna ambazo zinaweza zikatengeneza Kijiji cha Wabunge ambacho kitakuwa na urahisi wa kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mheshimiwa Nape Nnauye limefafanuliwa vizuri na Mheshimiwa Waziri wa Nchi na sijui kama kuna umuhimu wa kuileta Bungeni hiyo Sheria ya Usalama wa Taifa kwa sababu kazi za Usalama wa Taifa zinajulikana na ni *intelligence informations* na kushauri taasisi mbalimbali. Lakini nimeshindwa kuelewa hapa ilivyohusishwa na EPA pamoja na Diplomasia ya Uchumi ambayo kila watu na mikataba wako wataalam kwenye hizo sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema, kutoa ufafanuzi huo naomba sasa kutoa hoja ili mapendekezo yote na maoni ambayo nimeyaeleza yaweze kukubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, lakini kabla sijawahoji nalazimika

kufafanua jambo moja. Waheshimiwa Wabunge katika taarifa ya Kamati yetu ambayo sasa tutaikubali hapa kama tukihojiwa na tukakubali ndio, ukurasa wa 41 mpaka ukurasa wa 42 unazungumzia ulinzi kama alivyofafanua Mheshimiwa Mwenyekiti na pia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ujumla.

Lakini pia kuhusu kutoa namba maalum za usajili wa magari ya Wabunge, Waheshimiwa Wabunge mtagundua Mwenyekiti alilzungumza kwa kirefu wakati akiwasilisha hoja hii lakini pia hapa wakati akitoa ufafanuzi na yeye ameonyesha namna ambavyo kunaweza kukawa na ugumu ni gari gani iweze kuwekewa hizo namba na namna ya kufanya huu ulinzi kwa namna alivyosema Mheshimiwa Waziri.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu haya yaliyoko kwenye ripoti hii tukishahojiana ni suala la Serikali kuanza utekelezaji. Kwa sababu hiyo hili suala la ulinzi upande wa Serikali kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri na hili la Magari mimi naagiza mkalifanyie kazi mlipeteleke kwenye Kamati ili litakapokuja hapa wakati wa kuazimia ili haya yafanyike upande wa Serikali uwe umejipanga namna ya kulifanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge azimio hili ambalo ingebidi tulipitisha kwenye kifungu cha 3.2.4 naiagiza Serikali ikalifanyie kazi irudi kwenye Kamati na taarifa ili sasa Bunge liweze kuazimia jambo linaloweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji, wanaokubaliana na hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa kwa sababu ni Kamati mbili nitazungumza kidogo tukimaliza. Nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kufanya majumuisho ya taarifa ya utekelezaji wa majukumu na shughuli za Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kipindi cha Januari 2017 mpaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi mengi yameongelewa na mimi nilibakiza na kipande kidogo tu katika kumaliza kuhitimisha hii taarifa yangu.

La kwanza, nataka Wabunge wenzangu humu ndani na wananchi waelewe kwamba kimsingi kazi ya Kamati yangu sio kutoa adhabu kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa raia yeyote bali ni kuhakikisha kuwa nidhamu, ustahimilivu, heshima, utulivu na uzingatiji wa kanuni za majadiliano ndani ya Bunge unazingatiwa kwa ukamilifu ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikatiba kwa manufaa ya wananchi tunaowawakilisha na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo haki na madaraka ya Bunge, Kiti cha Spika, shughuli za Bunge ni lazima vilindwe kwa mujibu wa sheria na kanuni dhidi ya vitendo vyovyote vinavyoweza kupotosha, kudhalilisha, kuingilia na kushusha hadhi ya mhimili wa Bunge. Lakini pia watu na raia na Waheshimiwa Wabunge mjue kwamba mhimili huu ni moja ya mhimili mitatu ya dola hapa nchini kama inavyoelekezwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimepokea kwa maandishi michango ya Waheshimiwa Wabunge, naomba niwataje Mheshimiwa Mary Muro, Mheshimiwa Rhoda

Kunchela na Mheshimiwa Lucia Mlowe. Lakini pia nimepokea mchango wa Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma wote wameongelea maboresho ya kanuni, lakini pia wameomba uwepo usawa katika maamuzi hasa tunaposhauri Bunge. Na mimi nawaambia kwa sababu Kamati hii inafanya kazi chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Spika nitafikisha yote niliyoyapokea kwa maandishi kama ambavyo mmetaka.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu na jamii kwa ujumla nasema asanteni sana kwa ushirikiano mlionipa mimi na wajumbe wote wa Kamati ya Haki na Madaraka ya Bunge. Ushirikiano huo ulitupa hamasa na nguvu ya utekelezaji hasa jinsi ya kutekeleza majukumu na shughuli za Kamati kwa ufanisi mkubwa. Nasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wa Kamati hii wamepata taabu kwa baadhi ya Wabunge wameacha kutusalimia, tukiwasalimu hawajibu na wengine wanaona kama sisi tunafurahi sana tunapofanya maamuzi. Naomba nikiri kwamba hatuko hapa kwa sababu ya kuwakomoa Wabunge; hapana, hatuko hapa kwa sababu ya kuwakomoa raia hapana, tuko hapa kulinda maslahi ya muhimili wa Bunge kama ambavyo ipo katika Katiba na kama hivi ilivyo katika Kanuni ya Bunge za mwaka za 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja kwa Bunge lako, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Toa hoja.

**MHE. ALMAS A. MAIGE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja sasa Bunge lako lipitishie taarifa yangu hii ya mwaka ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, asante sana.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Wajumbe wa hii Kamati hawamo humu ndani?

Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji. Sasa nitawahoji wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili bna Madaraka ya bunge kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kwanza niwashukuru sana kwa kazi nzuri iliyofanywa na Kamati hizi mbili kwa niaba yetu sisi sote kama bunge lakini pia Wabunge ambao wameshiriki kwenye kuiboresha taarifa hii tunawashukuru sana kama Bunge. *(Makofi)*

Sasa upande wa Serikali haya ndio maazimio ya Bunge kutoka kwenye hizi Kamati mbili na tunaamini kwamba mtaanza utekelezaji mara moja ili Waheshimiwa Wabunge kwenye hizi Kamati wanapoanza kufuatilia utekelezaji wa mambo haya wasione yako vilevile pamoja na kwamba Bunge limeshaazimia.

Kwa hiyo, niwatakie utekelezaji mwema wa maazimio haya ya Bunge na yale ambayo mmeyafanyia kazi naamini taarifa za Kamati zitakazokuja zitatupa taarifa hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea na ratiba yetu mpaka tutakapomaliza shughuli zetu leo.

Katibu!

**NDG. NENELWA M. WANKANGA- KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Katibu wa Bunge.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi wa Bunge sasa zimemalizika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa fadhila na rehema kwa kutujalia afya njema hadi leo hii tunapohitimisha Mkutano huu wa Kumi wa Bunge lako tukufu ambao umetuweka Mjini Dodoma kwa takribani wiki mbili. Kwa kuwa huu ni mkutano wa kwanza tangu mwaka huu wa 2018 uanze nimitakie heri Mheshimiwa Spika ambaye kwa sasa yuko India, nakutakia wewe, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na watumishi wote wa Bunge hili heri ya mwaka mpya wa 2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa wananchi wa Jimbo la Songea Mjini na kwa Bunge lako Tukufu na kwa familia ya Marehemu Leonidas Gama aliyetangulia mbele ya haki wakati akiendelea

kulitumikia Taifa. Vilevile natoa salam za pole kwa ndugu, jamaa na familia ya Marehemu Mzee wetu Kingunge Ngombale Mwiru aliyewahi kulitumikia Bunge hili na Serikali hii na ni miongoni mwa waasisi wa Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu wote mahali pema peponi, amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Disemba mwaka 2017 taifa letu lilikumbwa na msiba mzito baada ya kuondokewa na askari wetu 14 ambao tunaendelea kuwakumbuka kwa ushupavu na ushujaa wakati wakitekeleza majukumu yao ya ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa kuuawa na waasi katika shambulio la kushtukiza. Kwa majonzi makubwa kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Jeshi la Wananchi Tanzania, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha natumia fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Kangi Lugola, Mbunge mwenzetu na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kufiwa na mwenza wake.

Vilevile natoa salamu za pole kwa familia ya watumishi wa mahakama kwa kifo cha Mheshimiwa Jaji Mstaafu Mheshimiwa Robert Kisanga ambaye atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa kulitumikia Taifa letu katika nyadhifa mbalimbali. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu pahala pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata ulemavu katika matukio mbalimbali ikiwemo ajali za vyombo vya usafiri, pia wale wote waliokumbwa na janga la mafuriko yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa mali ikiwemo miundombinu na hata vifo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo Wilayani Chemba, Mkoani Dodoma, Mkoa mzima wa Dar es Salaam na Wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro.



Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunahitimisha shughuli zilizopangwa katika Mkutano huu wa Kumi wa Bunge lako tukufu, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko, Mbunge wa Jimbo la Bukombe kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Madini. Napenda pia kuwapongeza Wabunge wallochagulia, Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro wa Jimbo la Songea Mjini, Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Jimbo la Singida Kaskazini na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa kutoka Jimbo la Longido. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Aderladus Kilangi kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni matumaini yangu kwamba uzoefu na umahiri wake katika masuala ya sheria utasaidia sana katika kuishauri Serikali na Bunge letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa George Masaju kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Tunamshukuru sana Mheshimiwa George Masaju kwa kazi kubwa aliyofanya katika kipindi chake alipokuwa nasi katika Bunge hili kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu wa Kumi tunaouhitimisha leo, jumla ya maswali 125 ya msingi na mengine 346 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miswada, Serikali na Bunge lako tukufu lilipitisha kwa hatua zake zote Miswada miwili ya sheria ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 91. Miswada hiyo ni kama ifuatavyo; muswada wa kwanza ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa mwaka 2017 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 5 Bill, 2017)* na Muswada wa pili ni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa mwaka 2017 *(The Public Service Social Security Fund Bill, 2017)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mkutano huu, kamati za kudumu za Bunge zipatazo 16 ziliwasilisha taarifa zake Bungeni. Aidha, taarifa hizo zilisheni maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati hizo kwa kazi nzuri waliyofanya kuanzia maandalizi ya kazi za Kamati hadi kuwasilisha taarifa zao katika Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea hoja nyingi zilizoibuliwa wakati wa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge na Serikali inaamini kuwa hoja hizo zimeibuliwa kwa malengo mazuri ya kuhakikisha kuwa tunaboresha utendaji kazi na uwajibikaji katika sekta ya umma kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma bora kama ilivyokusudiwa. Serikali inaahidi kuzifanyia kazi hoja hizo hasa wakati huu wa maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huu, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, Mbunge wa Jimbo la Kishapu aliwasilisha hoja binafsi kuhusu uzalishaji na ununuzi wa zao la pamba. Natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Nchambi (Mbunge) kwa hoja yake hiyo ambayo imeleta maboresho katika mtiririko mzima wa uboreshaji wa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya mpango wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka 2017/2018. Tarehe 1 Februari, 2018 Serikali iliwasilisha Bungeni taarifa kuhusu tathmini ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba 2017. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kupitia kwa kina taarifa hiyo na kupata picha kamili ya tathmini ya mapitio ya viashiria mbalimbali vya kiuchumi na mwenendo wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 na mwelekeo wake hadi Juni 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa hiyo ina umuhimu mkubwa kwa wananchi na wadau wa

maendeleo, napenda kutumia fursa hii kueleza japo kwa uchache kuhusu mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika kipindi cha nusu mwaka na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa katika mpango wa bajeti ya mwaka 2017/2018 yanafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viashiria mbalimbali vya kiuchumi vinaonyesha kwamba hali ya uchumi ni nzuri, pato la Taifa katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 lilikua kwa wastani wa asilimia 6.8. Hali hii inaashiria kwamba tuna matarajio makubwa ya kufikia lengo la mwaka la ukuaji wa asilimia 7.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta zilizochangia sana kwa kiwango kikubwa katika ukuaji huo ni pamoja na sekta ya habari na mawasiliano, uchimbaji madini, biashara, ujenzi na uzalishaji viwandani. Mfumuko wa bei uliendelea kutengemaa ambapo ulikuwa na wastani wa asilimia 4.8 kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa za huduma za nje ya nchi ilikuwa takribani dola za Marekani bilioni 8.695 ikilinganishwa na wastani wa dola bilioni 8.828 kwa miaka mitatu iliyopita. Aidha, hadi kufikia mwezi Novemba, 2017 akiba ya fedha za kigeni imeongezeka na kufikia dola za Marekani bilioni 5.91 kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa kwa takribani miaka minne kuanzia mwaka 2013 hadi 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha nusu mwaka ni wa kurudhisha ambapo ukusanyaji wa mapato ulifikia shilingi trilioni 12.95 sawa na asilimia 82.8 ya lengo lililopangwa katika kipindi hicho. Matumizi ya fedha hizo yameelekezwa katika kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali za kuhudumia wananchi na miradi ya kipaumbele kama ilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo ni pamoja na kuanza kwa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard*

*gage*, kugharamia mpango wa elimu msingi bila malipo, kugharamia mpango wa ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi na utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji Vijijini. Miradi mingine ni usambazaji wa umeme Vijijini kupitia REA, ununuzi wa meli za abiria na mizigo katika maziwa, ukarabati na ujenzi wa baadhi ya viwanja vya ndege na kujenga na kuendeleza maeneo ya uwekezaji wa viwanda katika mikoa mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika kwa mafaniko haya, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi anazofanya za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu na maendeleo ya haraka. Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kuwa inatekeleza ahadi zake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yanafikiwa kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga msingi na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuwa na mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Vilevile kuwa na usimamizi madhubuti wa ukusanyaji wa mapato ambao utasaidia sana kupanua wigo na kudhibiti ukwepaji wa kodi kupitia urasimishaji wa shughuli mbalimbali za uchumi kwa kuwezesha ukuaji wa biashara katika sekta ndogo na sekta za kati ambazo ndio mihimili ya kuzalisha ajira na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo; katika kipindi cha mwaka 2017/2018 hali ya usalama wa chakula nchini imeimarika sana kutokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula hususan mahindi katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Katavi, Kigoma, Mbeya, Songwe na Rukwa.

Aidha, taarifa zinaonesha kwamba mwenendo wa unyeshaji wa mvua za vuli ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini. Ni matarajio yetu kuwa hali ya mavuno ya msimu huu yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa hali ya utengamano na usalama wa chakula itaendelea kuwa imara kwa wananchi wote na kwa wakati wote. Hatua hizo ni pamoja na kuwezesha wafanyabiashara wa mazao ya chakula kuendelea kusafirisha na kuuza mazao ya chakula ndani na nje ya nchi. Natoa wito kwa wakulima kuendelea kuzitumia vizuri mvua zinazoendelea kunyeshwa kwa kupanda mazao stahiki na yatakayoweza kuiva kwa haraka kwa matumizi ya chakula ili kuweza kutumia chakula walichonacho kwa uangalifu hadi msimu mwingine wa mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa pembejeo; hali ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima imeimarika. Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia tarehe 1 Februari 2018, upatikanaji wa mbolea nchini kwa ajili ya mahindi na tumbaku ulifikia tani 250,376 sawa na asilimia 51.6 ya wastani wa mahitaji ya tani 485,000 kwa mwaka. Katika kipindi hicho, mbolea za kupandia na kukuzia zipatazo tani 229,839 ziliingizwa nchini na kusambazwa mikoani. Upatikanaji wa dawa za maji na unga (*sulphur*) kwa ajili ya mazao ya pamba na korosho unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 1 Februari 2018 upatikanaji wa mbegu bora nchini ulifikia tani 51,700 sawa na asilimia 86.2 ya mitaji halisi ya tani 60,000 kwa mwaka. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 222,357 za mbegu bora zilisambazwa nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mazao ya kimkakati na kuimarisha ushirika; wakati nikiahirisha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu tarehe 15 Septemba, 2017, nilieleza jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano kupitia maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usimamizi utakaokwenda sambamba na uzalishaji na uuzaji wa mazao makuu ya biashara hapa nchini ambayo ni pamoja na pamba, chai, kahawa, tumbaku na korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha mnyororo mzima wa kuongeza thamani ya mazao hayo ili kuhakikisha uwepo wa mfumo madhubuti wa usambazaji mbegu bora, kudhibiti visumbufu vya mimea, upatikanaji wa mbolea kwa wakati, kuboresha mifumo ya masoko pamoja na kufanya tafiti za kina zitakazotatua changamoto za uzalishaji wa mazao hayo. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa mazao haya yanachangia kikamilifu katika uchumi wa nchi na kutumika kama malighafi kwenye viwanda ili kutimiza malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye ziara zangu katika maeneo mbalimbali nchini, sambamba na mikutano ya wadau wa mazao hayo ya kibiashara, nilitoa maelekezo mahususi ikiwemo na kuimarisha ushirika, masoko, maafisa kilimo na ugani kutokaa ofisini na kwenda vijijini na mamlaka mbalimbali kufuata taratibu sahihi katika utoaji wa vibali vya ununuzi wa mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa watendaji wa vyama vya ushirika, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi maalum kuhusu mikataba mibovu ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (*NCU*), Chama Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga (*SHIRECU*), Chama Kikuu cha Ushirika cha Kagera (*KCU*) na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kilimanjaro (*KNCU*). Vilevile kuchunguza/kushikiriwa kwa mali za ushirika bila kufuata utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeagiza mali za Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (*NCU*) na Chama Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga (*SHIRECU*) kurudishwa kwenye vyama husika na watuhumiwa kuendelea kuchukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mali za *NCU* ambazo zimechukuliwa bila utaratibu ni kama ifuatavyo; jengo la *Nyanza Corporative Union Ltd*, maarufu kwa jina la *Transport House* au *Kauma House*, lililopo katika kiwanja namba 242 Mtaa wa *Station Road*, kiwanda cha kusindika mafuta cha

*New Era Oil Mill* kilichopo katika eneo la Igogo, jengo la viwanja vya *Ashok Industries* vilivyopo eneo la viwanja Igogo, majengo ya kilichokuwa kiwanda cha *Mkonge Dengu Industry*, kiwanda kilichipo Isamilo namba 80 Kitalu D, jengo lililopo katika kiwanja kilichopo kiwanja kilichopo Isamilo namba 110 Kitalu D, ghala moja katika viwanja namba 104 Kitalu A kilichopo eneo la Igogo, jengo moja lililopo Mjini Geita katika kiwanja namba 8 Kitalu K, jengo moja lililopo Mjini Geita katika kiwanja namba 24 Kitalu K pamoja na kiwanja kilichopo Isamilo katika kiwanja namba 89 Kitalu D ni miongoni mwa mali zilizotoweka kwa *NCU*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *SHIRECU*, mali ni ghala la *SHIRECU* lililopo Dar es Salaam na nyumba ya ghorofa tatu iliyopo kiwanja namba 1001 Kitalu BB Ilala, Dar es Salaam. Nafurahi kuwajulisha kuwa mali hizo zote za *NCU* kufikia leo hii tisa zimeshapatikana na zinarudi kwenye Ushirika Mkuu na mali moja ipo kwenye hatua ya uchunguzi ili mali zote kumi ziweze kurudi kwa *NCU*. Na mali za *SHIRECU* nazo zote zimepatikana na sasa wapo kwenye hatua za mwisho za makabidhiano. Serikali itaendelea kuviamsha Vyama vya Ushirika vya msingi na vyama vikuu vilivyosinzia katika mikoa yote ili kujenga ushirika imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi na hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali zinalenga kuongeza imani, hamasa na uzalishaji wa mazao na kusimamia masoko yake kwa wakulima na hivyo kuinua kipato cha wakulima wenyewe sambamba na kuwapatia fursa ya kujiajiri wenyewe katika sekta ya kilimo. Napenda kusesitiza kuwa uendelezaji wa mazao haya ya kimkakati kwa usimamizi mzuri wa mifumo sahihi ni katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kufikia uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo; zoezi la utambuzi wa mifugo. Tarehe 14 Desemba, 2016, tulianza zoezi la upigaji chapa mifugo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajiri na Ufuatiliaji wa Mifugo Namba 12 ya mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011. Lengo kuu la utambuzi huo ni kudhibiti magonjwa, wizi na migogoro

ya mifugo na kuimarisha usalama wa afya na mazao ya mifugo, kudhibiti usafirishaji na uhamaji wa mifugo kiholela na kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake kitaifa na kimataifa. Pia utambuzi wa mifugo unasaidia sana kutambua na kuboresha kwa usafi (*breed*) za mifugo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali illenga kupiga chapa ng'ombe milioni 17,390, 090 kati ya ng'ombe milioni 28,435,825 waliopo nchini. hadi kufikia tarehe 1 Februari, 2018 ng'ombe milioni 15,726,728 sawa na asilimia 90.4 ya lengo la ng'ombe milioni 17,390, 090 wameshapigwa chapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla zoezi la upigaji chapa la mifugo linaendelea vizuri na linatarajiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2018. Napenda kusesitiza kwamba zoezi hili la utambuzi wa mifugo ni endelevu na kila ndama anayefikia umri wa miezi sita atambuliwe. Natoa wito kwa wafugaji wote nchini kutoa ushirikiano kwa watendaji wa Serikali wanaotekeleza zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji; katika kutekeleza kauli mbiu ya ujezani wa viwanda nchini, Serikali imeendelea kuhamasisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji sambamba na uendelezaji wa miundombinu wezeshi ili kuvutia wawekezaji katika miradi mbalimbali. Serikali inaendelea kusesitiza kuwa halmashauri zote ziendelee na mpango wa kutenga maeneo maalum ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hiyo, Serikali imeandaa andiko maalum (*blueprint*) linaloainisha sheria, kanuni na tozo mbalimbali zinazopunguza urahisi na kufanya biashara nchini. Juhudi nyingine zinazofanyika ni pamoja na taasisi za udhibiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambazo ni Tume ya Ushindani (*FCC*), Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), Shirika la Viwango (*TBS*) na Wakala wa Vipimo (*WMA*) kuendelea kushirikiana kwa karibu kwa utendaji wao na kufanya kazi saa 24 kwa siku zote saba.



Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya upatikanaji rahisi wa huduma za kifedha na mikopo ya gharama nafuu kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF). Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2017, jumla ya mikopo 1,948 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.344 ilitolewa na kutengeneza ajira 4,438. Katika ajira hizo, wanaume ni 2,130 na wanawake walikuwa 2,308.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaelekeza watendaji wote waliopo katika mamlaka za Serikali, hususan zile za udhibiti na ukusanyaji wa mapato kutotumia vitisho dhidi ya wafanyabiashara katika kutekeleza majukumu yao ya utozaji mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya nishati, mpango kabambe wa upatikanaji wa nishati; Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na nishati ya umeme ya kutosha na ya uhakika na inayopatikana wakati wote. Miongoni mwa hatua hizo ni ujenzi wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rufiji (*Stiegler's Gorge*) wenye megawati 2,100; Mradi wa *Kinyerezi I* megawati 180 na Mradi wa *Kinyerezi II Extention* megawati 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi hiyo ya uzalishaji wa umeme unakwenda sambamba na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme ya Makambako mpaka Songea wa kV 240 na kutoka Singida kwenda Arusha mpaka Namanga wa kilovolti 400 na Serikali ina matumaini makubwa kwamba mradi wa kusambaza umeme unaokadiriwa kuwa na urefu wa kilometa 900 wa Makambako – Songea wenye kV 220 utakapokamilika utasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo ya Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako, Peramiho, Nyasa na Ludewa katika Mikoa ya Ruvuma na Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika *REA* Awamu ya III, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme

Vijijini Awamu ya III (REA) ambapo umepangwa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji 7,873 ambavyo bado havijapata umeme. Kati ya vijiji hivyo, ambavyo havijapata umeme ni vijiji 7,697 vimepangwa kupatiwa umeme wa gridi na vijiji 176 pamoja na visiwa vitapatiwa umeme kwa nje ya gridi kuwa ndiyo njia muafaka wa kuvipatia umeme kwa sasa. Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 689 kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali ya muda mrefu ya kuhakikisha maeneo yenye changamoto kubwa yanapata umeme wa kutosha na wa uhakika ni pamoja na kutekeleza miradi ya usambazaji umeme ya Somangafungu - Kinyerezi wa kilovolti 400, Mtwara - Somangafungu kilovolti 400 na *North West Grid Extension* ya kilovolti 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa miradi hiyo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama vile ulipaji fidia, upembuzi yakinifu na tathmini za athari ya mazingira kutawezesha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Katavi na Kigoma kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na hivyo kuboresha huduma za umeme katika mikoa hiyo na maeneo mengine yote nchini; tayari wakandarasi wako kila Wilaya kuanza kuweka umeme vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini, biashara za madini ya Tanzanite na Almasi. Itakumbukwa kwamba tarehe 6 Septemba, 2017 Spika aliunda Kamati ya Bunge kwa ajili ya kuchunguza mwenendo wa mnyororo wa uchimbaji wa biashara ya madini ya Almasi na Tanzanite. Kamati hizo ziliwasilisha taarifa zake zizoambatana na mapendekezo. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuhusu hatua mbalimbali zilizofikiwa na Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo hayo kama ifuatavyo:-

(i) Serikali imekwishaanza majadilano na wanahisa wa Makampuni ya *Tanzanite One Tanzania Ltd.* ili kubaini uwekezaji wao katika kampuni hiyo kwa lengo la kurekebisha mkataba wa umiliki ili uwe kwenye uhalisia.

(ii) Serikali imehamishia watumishi katika Mgoji wa Mereani kwa lengo la kusimamia kwa ufanisi shughuli zote za uchimbaji, uzalishaji na uuzaji wa madini ya Tanzania.

(iii) Serikali imeboresha utaratibu wa uthamini wa almasi unaofanywa na wataalam chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania.

(iv) Wajumbe wa iliyokuwa Bodi ya Uendeshaji wa Mgoji wa *William Diamonds Limited* wameondolewa katika nafasi hizo na Serikali inakamilisha taratibu za uteuzi wa Wajumbe wapya wa bodi hiyo; na

(v) Serikali imeimarisha ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, usafirishaji, uthamini na uuzaji wa madini yote ya vito na almasi nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ukuta wa Mererani; tarehe 20 Septemba, 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo la ujenzi wa ukuta katika eneo lililozunguka Mgoji wa Tanzania pale Mererani ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti utorohaji wa madini hayo. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu pamoja na Watanzania wote kuwa ujenzi wa ukuta huo wenye mzunguko wa kilometa 24.5 upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2018. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa uwekezaji kupitia wachimbaji wadogo, Serikali imeendelea na mkakati wake wa kuimarisha uwekezaji katika rasilimali za madini kupitia wachimbaji wadogo. Aidha, tangu mwaka 2000 hadi kufikia Desemba, 2017 kuna jumla ya leseni hai za wachimbaji wadogo 33,920 kwa nchi nzima. Kati ya hizo, leseni 6,976 zimetolewa kuanzia mwaka 2016/2017 hadi hivi sasa. Serikali imetenga maeneo 46 yenye ukubwa wa jumla ya hekta 281,534, mpango wa Serikali ni kuwekeza katika utafutaji wa madini (*mineral exploration*) katika maeneo yaliyotengwa ili tayari zitawasaidia wachimbaji wadogo katika uwekezaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kusaidia wachimbaji wadogo, natoa wito kwa wachimbaji wote wadogo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchimbaji madini kwa ajili ya usalama wao, afya yao na utunzaji wa mazingira yetu. Vilevile wanapaswa kutekeleza wajibu wao wa kulipa tozo stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utatuzi wa migogoro katika maeneo ya machimbo, Serikali inaendelea na juhudi za kutatua migogoro kadhaa katika maeneo mbalimbali ya machimbo na miongoni mwa maeneo yenye mgogoro mkubwa ni mgogoro uliko pale Nyamongo kati ya wananchi na mwekezaji wa Kampuni ya *North Mara* ambao kwa sasa unaendelea kushughulikiwa na tuna uhakika tutaumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Madini, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa uundaji wa Tume ya Madini unaendelea. Aidha, Katibu Mtendaji wa Tume hiyo ameshateuliwa na kikao cha kwanza cha Makamishna wa Tume kilifanyika tarehe 6 Januari, 2018. Kikao hicho pamoja na mambo mengine, kilipitia mapendekezo ya uteuzi wa wafanyakazi katika nafasi mbalimbali ndani ya tume; hata hivyo, kazi za msingi za tume kama utoaji wa vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi vinatolewa kwa usimamizi wa Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu, mvua kubwa zilizonyesha kwa kipindi cha mwezi Novemba, 2017 hadi Januari, 2018 zimeleta athari kubwa kwenye mtandao wa barabara nchini. Kutokana na mvua hizo, hali ya barabara zipatazo 50 katika mikoa 14 ziliathirika ambapo ilikuwa vigumu kupitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mikoa ambayo barabara zake ziliathirika na hali ya uwepo wa mvua ni pamoja na Mkoa wa Arusha, Pwani, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Manyara, Mbeya, Mwanza, Rukwa, Simiyu, Ruvuma, Singida, Songwe na Tabora. Kwa sasa barabara

hizo zimefanyiwa matengenezo ya dharura na zinapitika japo si kwa kuridhisha, lakini tunaendelea na kuimarisha kupitika kwake. Aidha, barabara 37 zilizofanyiwa matengenezo zinapitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mpango wa Elimu Msingi bila malipo; Serikali imeendelea kutekeleza kwa mafanikio Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo kupitia Waraka wa Elimu Namba Tatu wa mwaka 2016. Waraka huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka 2014, sambamba na maelekezo ya Ibara ya 52(a) ya Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 inayosisitiza utoaji elimu msingi bila malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2017, Serikali imetuma moja kwa moja shuleni jumla ya shilingi bilioni 124.8 kwa ajili ya kutekeleza mpango huo. Fedha zilizopelekwa moja kwa moja shuleni kwa mwezi ni shilingi bilioni 20.8 na shilingi bilioni 3.6 hupelekwa Baraza la Mitihani kwa ajili ya fidia ya gharama za mitihani kwa wanafunzi wa shule za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa michango shuleni, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa Waraka wa Elimu Namba Tatu wa mwaka 2016 ambao pamoja na mambo mengine ulipiga marufuku michango ya aina yoyote isiyo ya lazima katika elimu msingi. Katika siku za hivi karibuni kumejitokeza malalamiko kuhusu baadhi ya shule kuchangisha michango mbalimbali kutoka kwa wazazi na walezi na kusababisha watoto kurudishwa nyumbani kwa sababu ya mzazi au mlezi kutochangia michango shuleni. Hali hiyo ni kinyume na maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kutoa ufafanuzi na pia kutoa wito kwa watendaji wa elimu kuanzia Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wadau wote wa elimu, kuzingatia maelekezo ya waraka uliotolewa na Serikali ambapo majukumu ya kila mdau katika kutekeleza Mpango wa Elimu Msingi bila Malipo yamefafanuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruhusa ya michango shuleni ipo kutoka mtu mmoja mmoja, vikundi au taasisi. Hata hivyo, michango yote sasa itafikishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili ashirikishe kamati za shule kwa shule za msingi na bodi za shule kwa shule za sekondari, walimu wasisumbuliwe na michango hiyo ili wajikite kwenye taaluma zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda mipaka na viwanja vya shule; kufuatia kuwepo kwa changamoto ya umiliki wa ardhi kutokana na baadhi ya shule kutokuwa na hatimiliki, Serikali inaendelea kukusanya taarifa kutoka shule mbalimbali za Serikali kwa lengo la kujua hali ya umiliki wa ardhi katika shule hizo. Hatua hii ya awali inatarajiwa kuhusisha shule za sekondari kongwe zipatazo 89. Zoezi hilo litakapokamilika litawezesha Serikali kuandaa hatimiliki kwa shule zenye umiliki wa Serikali na pia kufanya maamuzi kwa shule ambazo umiliki wake uko chini ya taasisi za dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia zoezi hili, maeneo ya mipaka ya shule ikiwemo viwanja vya michezo vitatambuliwa na kujumuishwa kwenye ramani za shule. Zoezi la ufuatiliaji wa umiliki wa ardhi kwa shule za msingi na shule za sekondari zilizobaki za Serikali itaendelea kufanyika ili kuondoa changamoto za migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maji, utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri; Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri zote nchini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza mwaka 2006 hadi 2020/2025. Lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwa hadi kufikia mwaka 2020 hali ya huduma ya upatikanaji wa maji ifikie asilimia 85 kwa wananchi waishio vijijini na asilimia 95 kwa wale wanaoishi mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2017 jumla ya shilingi bilioni 55.6 za bajeti ya miradi ya maji kwa mwaka 2017/2018 zilipelekwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya utekelezaji

wa miradi mbalimbali ya maji. Jumla ya miradi 1,466, sawa na asilimia 80.99 ya miradi yote 1,810 iliyopangwa kutekelezwa kupitia Mpango wa Programu ya Sekta ya Maji imekamilika. Miradi iliyobaki ni 376 na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa naibu Spika, aidha, kutokana na changamoto za kuharibika kwa miundombinu ya maji, jumla ya vituo vya kuchotea maji 83,575 kati ya 122,655 vilivyojengwa ndivyo vinavyofanya kazi na vinahudumia wananchi wa vijijini wapatao 20,893,750 sawa na asilimia 56 ya wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Juni, 2020 utekelezaji wa programu hii umelenga kujenga, kukarabati na kuongeza wigo wa miradi ya maji katika vijiji ambapo vijiji 4,105 vitanufaika na mpango huo. Hali kadhalika vituo vipatavyo 76,334 vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu 19,000,080 vinatarajiwa kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji; Serikali imeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaohusika na ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Mathalani wakati wa ziara yangu ya kikazi katika Mkoa wa Mara mwezi Januari, 2018, nilibaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa kwa watendaji wa sekta ya maji mkoani humo. Mapungufu hayo yalichangia sana kwa kiasi kikubwa kuchelewa kukamilika kwa miradi, kutoanza kabisa kwa miradi ya maji licha ya Serikali kutuma fedha kila inapotakiwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ubadhirifu huo, Serikali imedhamiria, imelazimika kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa kufanya uchunguzi na kuivunja Bodi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoani Mara. Kupitia Bunge lako tukufu, natoa maelekezo kwa Wakuu wote wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maji iliyopo katika

maeneo yao ili wajiridhishe kuwa huduma ya maji inapatikana kwenye maeneo ya miji na vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuhamia Dodoma; Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutekeleza azma yake ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Mjini Dodoma. Aidha, napenda pia kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ofisi yake walihamia rasmi Dodoma tarehe 15 Desemba, 2017 kama ilivyopangwa. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana na kumkaribisha sana Mheshimiwa Makamu wetu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwenye Makao Makuu ya nchi Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kufuatia utekelezaji wa awamu ya kwanza na ya pili ya watumishi wa umma kuhamia Dodoma, jumla ya watumishi 3,829 kutoka Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali tayari wamehamia Dodoma. Ujio wao huo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Dodoma aliyoyatoa tarehe 23 Julai, 2016. Nitoe wito kwa watumishi wote waliohamia Dodoma, hapo ndiyo wamefika Mkoani Dodoma na hatutarajii kuwakuta Dar es Salaam na maeneo mengine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kuifanya Dodoma kuwa ya kijani; kuhamia kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais Mjini Dodoma kumeongeza hamasa ya kuboresha mazingira ya mji huu, hususan baada ya kuzindua rasmi kampeni maalum ya upandaji miti Mjini Dodoma maarufu kama Kampeni ya Kujanisha Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kuifanya Dodoma ambayo ndiyo Makao Makuu ya nchi kuwa ya ukanda wa kijani (*green belt*) kupitia mpango huo. Mpango huo unahusisha kuendeleza, kutunza na kuhifadhi maeneo ya ukanda wa kijani ambayo ni pamoja na Msitu wa Mahomanyika wenye ukubwa wa hekta 2,000, Msitu wa



Chimwaga Nzuguni wenye ukubwa wa hekta 300 na Msitu wa Mbwenzelo wenye ukubwa wa hekta 3,500 pamoja na vilima vya Image pamoja na Nkali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza malengo hayo ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani, Serikali imeendelea kutoa elimu ya upandaji miti na uhifadhi wa misitu hususan miti adimu ya asili na makao ya wanyamapori mbalimbali katika Kata nane za Ipala, Nzuguni, Kikombo, Ng'ong'ona, Chahwa, Zuzu, Hombolo na Kikuyu Kaskazini. Aidha, kila kata imepewa lengo la kupanda miti isiyopungua 40,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa zoezi la upandaji miti jumla miche 34,000 yenye thamani ya shilingi milioni 34 imetolewa bure katika kata mbalimbali. Vilevile kupitia mradi wa *TASAF* jumla ya miche 138 imeoteshwa na inaendelea kusambazwa kwa kwa wananchi. Aidha, kwa sasa Manispaa ya Dodoma inaendelea na maandalizi ya kuotesha miche mingine ipatayo 200,000 kwa ajili ya msimu hujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru wadau mbalimbali akiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), Bonde la Wami Ruvu Umoja wa vijana wa Chama cha Mapinduzi ambao kwa kushirikiana na Manispaa ya Dodoma wamefanikisha upandaji wa miche 79000 katika maeneo ya *UDOM*, *Mzakwe*, *Iseni Park*, Nala na Mahomanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha zoezi la upandaji miti linakuwa endelevu pamoja na kuongeza usimamizi naziagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinaandaa miche ya kutosha na kuweka utaratibu wa kila kaya kupanda na kutunza miti isiyopungua mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za utendaji na maendeleo ya Halmashauri zote zioneshe mafanikio yaliyopatikana kutokana na zoezi la upandaji miti. Aidha, utendaji wa Wakurugenzi na Wakuu wote wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya utapimwa kutokana na uendelezaji wa

utunzaji wa mazingira katika maeneo yao vilevile, Uendelezaji wa makao na mpangilio wa Mji wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia agizo la Serikali la kuamishi Makao Makuu ya nchi Dodoma mahitaji ya viwanja hadi mwezi Febuari, 2018 yalifikia viwanja 24,602. Katika kukabiliana na changamoto na mahitaji ya viwanja Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma hivi sasa inatekeleza mkakati wake wa kuzalisha viwanja 30,000 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, tayari upimaji wa viwanja vipya 15,316 umekamilika na kazi inaendelea. Viwanja hivi vitaanza kugawiwa kuanzia tarehe 30 Machi, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi kilichobaki cha viwanja 14,684 kitakamilika ifikapo Juni, 2018. Wananchi watauziwa viwanja hivyo kwa bei elekezi itakayotolewa na Halmashauri ya Manispaa Dodoma. Natoa wito kwa wananchi na watumishi wa umma watakao hitaji viwanja kufuata taratibu za maombi ya viwanja pindi vitakapo tangazwa rasmi. Eneo lililokuwa CDA na sasa Manispaa ya Dodoma huduma zote za kibenki ziko pale, mabenki yako pale kwa hiyo utaweza kupata fedha na kulipia viwanja na kwenda kupeleka risiti hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kubadilisha hati zilizo tolewa na ilikuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu CDA na kupata hati miliki za miaka 99 linaendelea. Wenye hati za CDA mnasisitizwa kuendelea na taratibu ya kuzibadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutuongoza vyema ndani ya Bunge lako Tukufu katika Bunge hili ambalo leo tunahitimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawashukuru Wenyeviti, Wabunge ambao kwa umahiri mkubwa wamekuwa wakiendesha vikao vya Bunge hili tukufu. Kadhalika niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu

kwa michango yenu mbalimbali muhimu katika kuboresha maisha ya wananchi wetu kwa ujumla wake.

Nimshukuru pia Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa huduma nzuri na msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niwashukuru watendaji wa Serikali na taasisi mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa na hivyo kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia siwezi kuwasahau wana habari ambao wamekuwa wakihararisha umma kwa uchambuzi wa hoja na kueleza mwenendo mzima wa Bunge hili na kufikisha habari hizo kwa wananchi nawasihhi muendeleo na kazi yenu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwa washiriki wa bunge hili. Pia niwashukuru madereva wote walio tuhudumia wametuleta hapa Bungeni wamekuwa wakitusafirisha hapa mjini wakati wote na sasa wana turudisha nyumbani. Kwa hiyo, niwatakie heri kwa safari ya kurejea nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nitoe hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne tarehe 3 Aprili, 2018 saa tatu asubuhi katika Ukumbi huu huu hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namba kutoa hoja.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.),  
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,  
WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA KUMI WA BUNGE LA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 9  
FEBRUARI, 2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

***Shukrani***

1. **Mheshimiwa Naibu Spika**, awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa fadhila na rehema kwa kutujaalia afya njema hadi leo hii tunapohitimisha Mkutano wa Kumi wa Bunge lako Tukufu ambao umetuweka mjini Dodoma kwa takriban wiki mbili. Kwa kuwa huu ni mkutano wa kwanza tangu mwaka huu uanze, ninakutakia wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote wa Bunge Heri ya Mwaka Mpya 2018.

***Salamu za Pole***

2. **Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa masikitiko makubwa naungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini, kwa Bunge lako Tukufu na kwa familia ya marehemu Leonidas Gama, aliyetangulia mbele za haki wakati akiendelea kulitumikia Taifa. Vilevile, natoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na familia ya marehemu Kingunge Ngombale-Mwiru, aliyewahi kulitumikia Bunge hili, Serikali na ni miongoni mwa waasisi wa Chama cha Mapinduzi. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi.

**Amina!**

3. **Mheshimiwa Naibu Spika**, mwezi Desemba, 2017 Taifa letu lilikumbwa na msiba mzito baada ya kuondokewa na askari wetu 14, ambao tutaendelea kuwakumbuka kwa ushupavu na ushujaa wao wakati wakitekeleza majukumu yao ya Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa, huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa kuuawa na waasi katika shambulio la kushtukiza. Kwa majonzi

makubwa kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa msiba huo mkubwa.

**4. Mheshimiwa Naibu Spika**, aidha, natumia fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mhe. Kangi Lugola (Mb.), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kufiwa na mwenza wake. Vilevile, natoa salamu za pole kwa familia na watumishi wa mahakama kwa kifo cha Jaji Mstaafu, Mhe. Robert Kisanga ambaye atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa wa kulumikia Taifa letu katika nyadhifa mbalimbali. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahala pema peponi.  
**Amina!**

**5. Mheshimiwa Naibu Spika**, nitumie nafasi hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata ulemavu katika matukio mbalimbali ikiwemo ajali za vyombo vya usafiri. Pia, wale wote waliokumbwa na janga la mafuriko yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa mali ikiwemo miundombinu na hata vifo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yakiwemo Chemba (Dodoma), Dar es Salaam na Kilosa (Morogoro).

#### *Pongezi*

**6. Mheshimiwa Naibu Spika**, wakati tunahitimisha shughuli zilizopangwa katika mkutano huu wa Kumi wa Bunge lako tukufu, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mhe. Dotto Mashaka Biteko (Mbunge wa Jimbo la Bukombe) kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Madini. Napenda pia kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa, Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Jimbo la Songea Mjini), Mhe. Justin Joseph Monko (Jimbo la Singida Kaskazini) na Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kisurwa (Jimbo la Longido).

**7. Mheshimiwa Naibu Spika**, vilevile, napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Adelardus Kilangi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ni matumaini yangu kwamba uzoefu na umahiri wake katika

masuala ya sheria, utasaidia sana katika kuishauri Serikali na Bunge. Aidha, nampongeza Mheshimiwa George Masaju kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Tunamshukuru Mheshimiwa George Masaju kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi chake alipokuwa nasi kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## SHUGHULI ZA BUNGE

### (a) *Maswali na Majibu*

8. **Mheshimiwa Naibu Spika**, katika mkutano huu wa Kumi tunaouhitimisha leo, jumla ya maswali **125** ya msingi na mengine **346** ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kupatiwa majibu na Serikali.

### (b) *Miswada ya Serikali*

9. **Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa upande wa Miswada ya Serikali, Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa hatua zake zote miswada miwili ya Sheria ambayo ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 91. Miswada hiyo ni kama ifuatayo: -

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017*].

(ii) Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 [*The Public Service Social Security Fund Bill, 2017*].

### (c) *Kamati za Kudumu za Bunge*

10. **Mheshimiwa Naibu Spika**, wakati wa mkutano huu, Kamati za Kudumu za Bunge zipatazo 16 ziliwasilisha taarifa zake Bungeni. Aidha, taarifa hizo zilisheheni maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali kwa Serikali. Nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na wajumbe

wote wa kamati hizo kwa kazi nzuri waliyoifanya kuanzia maandalizi ya kazi za kamati hadi kuwasilisha taarifa zao katika Bunge lako tukufu.

**11. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imepokea hoja nyingi zilizoibuliwa wakati wa vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge. Serikali inaamini kuwa hoja hizo zimeibuliwa kwa malengo mazuri ya kuhakikisha tunaboresha utendaji kazi na uwajibikaji katika sekta ya umma kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma bora kama ilivyokusudiwa. Serikali inahidi kuzifanyia kazi hoja hizo hasa wakati huu wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019.

**(d) Hoja Binafsi**

**12. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika Mkutano huu, Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, aliwasilisha hoja binafsi kuhusu uzalishaji na ununuzi wa zao la pamba. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa hoja yake hiyo ambayo italeta maboresho katia utendaji wetu.

**MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2017/2018**

**13. Mheshimiwa Naibu Spika**, tarehe 01 Februari, 2018 Serikali iliwasilisha Bungeni taarifa kuhusu Tathmini ya Hali ya Uchumi na Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka kuanzia mwezi Julai hadi Desemba, 2017. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kupitia kwa kina taarifa hiyo na kupata picha kamili ya tathmini ya mapitio ya viashiria mbalimbali vya kiuchumi na mwenendo wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 na mwelekeo wake hadi Juni, 2018.

**14. Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa kuwa taarifa hiyo ina umuhimu mkubwa kwa wananchi na wadau wa maendeleo, napenda kutumia fursa hii kueleza japo kwa uchache kuhusu mafanikio kadhaa yaliyopatikana katika kipindi cha nusu

mwaka na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/2018 yanafikiwa.

**15. Mheshimiwa Naibu Spika**, viashiria mbalimbali vya kiuchumi vinaonesha kwamba hali ya uchumi ni nzuri. Pato la Taifa katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017 lilikua kwa wastani wa asilimia **6.8**. Hali hii inaashiria kwamba tuna matarajio makubwa ya kufikia lengo la mwaka la ukuaji wa asilimia **7.0**.

Sekta zilizochangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji huo ni habari na mawasiliano, uchimbaji madini, biashara, ujenzi na uzalishaji viwandani. Mfumuko wa bei uliendelea kutengemaa ambapo ulikuwa wa wastani wa asilimia **4.8** kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, 2017.

**16. Mheshimiwa Naibu Spika**, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ilikuwa takriban dola za Marekani bilioni **8.695** ikilinganishwa na wastani wa dola bilioni **8.828** kwa miaka mitatu iliyopita. Aidha, hadi kufikia Novemba 2017, akiba ya fedha za kigeni imeongezeka na kufikia dola za Marekani bilioni **5.91** kiwango ambacho hakijawahi kufikiwa kwa takriban miaka minne kuanzia mwaka 2013 hadi 2016.

**17. Mheshimiwa Naibu Spika**, utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka ni wa kuridhisha ambapo ukusanyaji wa mapato ulifikia shilingi trilioni **12.95** sawa na asilimia **82.8** ya lengo lililopangwa katika kipindi hicho. Matumizi ya fedha hizo yameelekezwa katika kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali za kuhudumia wananchi na miradi ya kipaumbele kama ilivyopitishwa na Bunge lako tukufu.

Miradi hiyo ni pamoja na kuanza kwa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*, kugharamia mpango wa elimumsingi bila malipo, kugharamia mpango wa ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, na utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji vijijini na mijini. Miradi mingine ni usambazaji wa umeme vijijini kupitia REA, ununuzi wa meli



za abiria na mizigo katika maziwa, ukarabati na ujenzi wa baadhi ya viwanja vya ndege na kujenga na kuendeleza maeneo ya uwekezaji wa viwanda katika mikoa mbalimbali nchini.

**18. Mheshimiwa Naibu Spika**, hakika kwa mafanikio haya tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi anazofanya za kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu na maendeleo ya haraka. Serikali ya Awamu ya Tano itahakikisha kuwa inatekeleza ahadi zake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa kwa mwaka 2017/2018 yanafikiwa kwa kiwango kikubwa.

Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha na kujenga misingi na mifumo imara ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa lengo la kuwa na mapato endelevu kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Vilevile, kuwa na usimamizi madhubuti wa ukusanyaji wa mapato ambao utasaidia kupanua wigo na kudhibiti ukwepaji wa kodi kupitia urasimishaji wa shughuli za uchumi kwa kuwezesha ukuaji wa biashara katika sekta ndogo na za kati ambazo ndiyo mihimili wa kuzalisha ajira na kukuza uchumi.

## **KILIMO**

### **(a) Hali ya Upatikanaji wa Chakula**

**19. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, hali ya usalama wa chakula nchini imeimarika kutokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula hususan mahindi katika mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Katavi, Kigoma, Mbeya, Songwe na Rukwa. Aidha, taarifa zinaonesha kwamba mwenendo wa unyeshaji wa mvua za vuli ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini. Ni matarajio yetu kuwa hali ya mavuno msimu huu itakuwa nzuri.

**20. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa hali ya utengamano na

usalama wa chakula inaendelea kuwa imara kwa wananchi wote na kwa wakati wote. Hatua hizo ni pamoja na kuwezesha wafanyabiashara wa mazao ya chakula kuendelea kusafirisha na kuuza mazao ya chakula nje na ndani ya nchi. Natoa wito kwa wakulima wazitumie vizuri mvua zinazoendelea kunyesha kwa kupanda mazao stahiki na kutumia chakula walichonacho kwa uangalifu hadi msimu mwingine wa mavuno.

**(b) Hali ya Upatikanaji wa Pembejeo**

**21. Mheshimiwa Naibu Spika**, hali ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima imeimarika. Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia tarehe 1 Februari, 2018 upatikanaji wa mbolea nchini kwa ajili ya mahindi na tumbaku ulifikia tani **250,376** sawa na asilimia **51.6** ya wastani wa mahitaji ya tani **485,000** kwa mwaka.

Katika kipindi hicho hicho, mbolea za kupandia na kukuzia zenye zipatazo tani **229,839** ziliingizwa nchini na kusambazwa mikoani. Upatikanaji wa dawa za maji na unga (Salfa) kwa ajili ya mazao ya pamba na korosho unaendelea.

**22. Mheshimiwa Naibu Spika**, hadi kufikia tarehe 1 Februari, 2018 upatikanaji wa mbegu bora nchini ulifikia tani **51,700**, sawa na asilimia **86.2** ya mahitaji halisi ya tani **60,000** kwa mwaka. Katika kipindi hicho jumla ya tani **22,357** za mbegu bora zilisambazwa nchini.

**(c) Usimamizi wa Mazao ya Kimkakati na Kuimarisha Ushirika**

**23. Mheshimiwa Naibu Spika**, wakati nikiahirisha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu tarehe 15 Septemba 2017, nilieleza jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano kupitia maelekezo mahsusi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usimamizi utakaokwenda sambamba na uzalishaji na uuzaji wa mazao makuu ya biashara hapa nchini ambayo ni pamoja na pamba, chai, kahawa tumbaku na korosho.

**24. Mheshimiwa Naibu Spika,** Serikali imeendelea kuboresha mnyororo mzima wa kuongeza thamani ya mazao hayo, ili kuhakikisha uwepo wa mfumo madhubuti wa usambazaji mbegu bora, kudhibiti visumbufu vya mimea, upatikanaji wa mbolea kwa wakati, kuboresha mifumo ya masoko pamoja na kufanya tafiti za kina zitakazotatua changamoto za uzalishaji wa mazao hayo.

Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa mazao hayo yanachangia kikamilifu katika uchumi wa nchi na kutumika kama mali ghafi kwenye viwanda. Ili kutimiza malengo hayo, nilipokuwa kwenye ziara zangu katika maeneo mbalimbali nchini sambamba na mikutano ya wadau wa mazao hayo ya biashara, nilitoa maelekezo mahsusi ikiwemo kuimarisha ushirika, masoko, maafisa kilimo na ugani kutokaa ofisini na kwenda vijijini na mamlaka mbalimbali kufuata taratibu sahihi katika utoaji wa vibali vya ununuzi wa mazao.

**25. Mheshimiwa Naibu Spika,** katika kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa watendaji wa vyama vya ushirika, Serikali inaendelea kufanya uchunguzi maalum kuhusu mikataba mibovu ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (NCU), Chama Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga (SHIRECU), Chama Kikuu cha Ushirika cha Kagera (KCU) na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kilimanjaro (KNCU). Vilevile, kuchunguza kushikiliwa kwa mali za ushirika bila kufuata utaratibu.

**26. Mheshimiwa Naibu Spika,** Serikali imeagiza mali za Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (NCU) na Chama Kikuu cha Ushirika cha Shinyanga (SHIRECU) zirudishwe kwenye vyama husika na watuhumiwa wachukuliwe hatua za kisheria. Mali za NCU ni pamoja na;

1. Jengo la Nyanza Cooperative Union (1984) Ltd. maarufu kwa jina la "Transport House" au KAUMA House, lililopo katika kiwanja namba 242, Kitalu T, Mtaa wa *Station Road*;

2. Kiwanda cha kusindika mafuta cha New Era Oil Mill, kilichopo katika eneo la Igogo;

3. Jengo na viwanja vya Ashock Industries vilivyopo eneo la viwanda Igogo.
4. Majengo ya kilichokuwa Kiwanda cha Mkonge na Dengu kilichopo eneo la Igogo, kiwanja namba 41 na 79;
5. Jengo lililopo katika kiwanja kilichopo Isamilo Namba 80, Kitalu "D";
6. Jengo lililopo katika Kiwanja kilichopo Isamilo Namba 110, Kitalu "D";
7. Ghala moja katika kiwanja Namba 104, Kitalu "A" kilichopo eneo la Igogo;
8. Jengo moja lililopo mjini Geita katika kiwanja Namba 8 Kitalu "K";
9. Jengo moja lililopo mjini Geita, katika kiwanja Namba 24, Kitalu "K"
10. Jengo lililopo Isamilo katika kiwanja namba 89 Kitalu "D".

**27. Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa upande wa **SHIRECU**, mali hizo ni ghala la **SHIRECU** lililopo Kurasini, Dar es Salaam na nyumba ya ghorofa tatu (3) iliyopo Kiwanja Namba 1001 "BB" Ilala, Dar es Salaam. Serikali itaendelea kuviamsha vyama vya ushirika vya msingi na vyama vikuu vilivyo sinzia katika mikoa yote ili kujenga ushirika imara.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba mali tisa za **NCU** zimepatikana na zimerudi kwenye ushirika huo, wakati mali moja bado iko kwenye hatua ya uchunguzi. Kwa upande wa **SHIRECU**, mali zote zimepatikana na ziko kwenye hatua ya makabidhiano.

**28. Mheshimiwa Naibu Spika**, juhudi na hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali, zinalenga kuongeza imani, hamasa na uzalishaji wa mazao na kusimamia masoko yake,

na hivyo, kuinua kipato cha wakulima sambamba na kuwapatia fursa ya kujijiri wenyewe katika sekta ya kilimo. Napenda kuisitiza kuwa uendelezaji wa mazao hayo ya kimkakati kwa usimamizi mzuri wa mifumo sahihi ni katika kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kufikia uchumi wa viwanda.

## MIFUGO

### *Zoezi la Utambuzi wa Mifugo*

29. **Mheshimiwa Naibu Spika**, tarehe 14 Desemba, 2016 tulianza zoezi la upigaji chapa mifugo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2011. Lengo kuu la utambuzi huo ni kudhibiti magonjwa ya mifugo na wizi wa mifugo, kuimarisha usalama wa afya na mazao ya mifugo, kudhibiti usafirishaji na uhamaji wa mifugo kiholela na kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake kitaifa na kimataifa. Pia, utambuzi wa mifugo unasaidia kutambua na kuboresha kosaafu (breed) za mifugo.

30. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali lililenga kupiga chapa ng'ombe **17,390,090** kati ya ng'ombe **28,435,825** waliopo nchini. Hadi kufikia tarehe 1 Februari 2018, ng'ombe **15,726,728** sawa na asilimia **90.4** ya lengo la ng'ombe **17,390,090** walikuwa wameshapigwa chapa.

31. **Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa ujumla, zoezi la upigaji chapa mifugo linaendelea vizuri na linatarajiwa kukamilika tarehe 30 Machi, 2018. Napenda kuisitiza kwamba zoezi hili la utambuzi wa mifugo ni endelevu na kila ndama anayefikia umri wa miezi sita lazima atambuliwe. Ntoa wito kwa wafugaji wote nchini kutoa ushirikiano kwa watendaji wa Serikali wanaotekeleza zoezi hilo.

## VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

32. **Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kutekeleza kaulimbiu ya ujenzi wa viwanda nchini, Serikali imeendelea

kuhamasisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji sambamba na uendelezaji wa miundombinu wezeshi ili kuvutia wawekezaji katika miradi mbalimbali. Serikali inaendelea kusisitiza kuwa Halmashauri zote ziendeleo na mpango wa kutenga maeneo maalumu ya uwekezaji.

**33. Mheshimiwa Naibu Spika**, sambamba na hatua hiyo, Serikali imeandaa andiko maalum *“Blue Print”* linaloainisha Sheria, Kanuni na tozo mbalimbali zinazopunguza urahisi wa kufanya biashara nchini. Juhudi nyingine zilizofanyika ni pamoja na taasisi za udhibiti zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuendelea kushirikiana kwa karibu katika utendaji wao na kufanya kazi saa 24 kwa siku 7. Taasisi hizo ni Tume ya Ushindani (FCC), Kituo cha Uwekezaji (TIC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Vipimo Nchini (WMA).

**34. Mheshimiwa Naibu Spika**, vilevile, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya upatikanaji rahisi wa huduma za kifedha na mikopo ya gharama nafuu kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF). Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2017, jumla ya mikopo **1,948** yenye thamani ya Shilingi Bilioni **3.344** ilitolewa na kutengeneza ajira **4,438**. Katika ajira hizo, wanaume ni **2,130** na wanawake ni **2,308**.

**35. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali inaelekeza watendaji wote waliopo katika Mamlaka za Serikali hususan zile za udhibiti na ukusanyaji wa mapato kutotumia vitisho dhidi ya wafanyabiashara wakati wakitekeleza majukumu yao.

## **NISHATI**

### ***Mpango Kamambe wa Upatikanaji wa Nishati***

**36. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na nishati ya umeme ya kutosha na inayopatikana kwa uhakika. Miongoni mwa hatua hizo ni

ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Rufiji (**Stiegler's Gorge MW 2,100**), Mradi wa Kinyerezi I (**MW 180**) na Mradi wa Kinyerezi II *Extension (MW 240)*.

**37. Mheshimiwa Naibu Spika**, utekelezaji wa miradi hiyo ya uzalishaji wa umeme unakwenda sambamba na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme ya Makambako-Songea (**kV 220**) na Singida-Arusha-Namanga (**kV 400**). Serikali ina matumaini makubwa kwamba mradi wa kusambaza umeme unaokadiriwa kuwa na urefu wa kilometa **900** wa Makambako-Songea (**kV 220**) utakapo kamilika utasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo ya Wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Makambako, Peramiho na Ludewa katika Mikoa ya Ruvuma na Njombe.

### ***REA Awamu ya Tatu***

**38. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA) ambao umepangwa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji **7,873** ambavyo bado havijapata umeme. Kati ya vijiji hivyo ambavyo havijapata umeme, vijiji **7,697** vimepangwa kupatiwa umeme wa gridi na vijiji **176** pamoja na visiwa vitapatiwa umeme wa nje ya gridi kwa kuwa ndiyo njia muafaka ya kuvipatia umeme kwa sasa. Serikali imetenga jumla ya Shilingi **bilioni 689** kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini.

**39. Mheshimiwa Naibu Spika**, Mipango ya Serikali ya muda mrefu ya kuhakikisha maeneo yenye changamoto kubwa yanapata umeme wa kutosha na wa uhakika ni pamoja na kutekeleza miradi ya usambazaji umeme ya Somanga-Fungu-Kinyerezi (**kV 400**), Mtwara-Somanga-Fungu (**kV 400**) na North West Grid Extension (**kV 400**).

**40. Mheshimiwa Naibu Spika**, kukamilika kwa miradi hiyo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama vile ulipaji fidia, upembuzi yakinifu na tathmini ya athari ya mazingira, kutawezesha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Rukwa, Katavi na Kigoma kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na

hivyo, kuboresha huduma ya umeme katika mikoa hiyo na maeneo mengine nchini. Tayari wakandarasi wapo kila Wilaya kuanza kuweka umeme vijijini.

## MADINI

### (a) *Biashara za Madini ya Tanzanite na Almasi*

41. **Mheshimiwa Naibu Spika**, itakumbukwa kwamba tarehe 06 Septemba, 2017, uliunda Kamati za Bunge kwa ajili ya kuchunguza mwenendo wa mnyororo wa uchimbaji na biashara ya madini ya Almasi na Tanzanite. Kamati hizo ziliwasilisha taarifa zake zilizoambatana na mapendekezo. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuhusu hatua mbalimbali zilizofikiwa na Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo hayo kama ifuatavyo: -

**Moja:** Serikali imekwishaanza majadiliano na wanahisa wa makampuni ya *Tanzanite One (T) Limited* ili kubaini uwekezaji wao katika kampuni hiyo kwa lengo la kurekebisha mkataba wa umiliki ili uwe kwenye uhalisia;

**Mbili:** Serikali imehamishia watumishi wake katika mgodi wa Mererani kwa lengo la kusimamia kwa ufanisi shughuli zote za uchimbaji, uzalishaji na uuzaji wa madini ya *Tanzanite*;

**Tatu:** Serikali imeboresha utaratibu wa uthamini wa almasi unaofanywa na wataalamu chini ya usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania;

**Nne:** Wajumbe wote wa iliyokuwa Bodi ya Uendeshaji wa Mgodi wa *Williamson Diamonds Limited* wameondolewa katika nafasi hizo na Serikali inakamilisha taratibu za uteuzi wa wajumbe wapya wa Bodi hiyo; na

**Tano:** Vilevile, Serikali imeimarisha ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, usafirishaji, uthamini na uuzaji wa madini yote ya vito na almasi nchini.



**(b) Ujenzi wa Ukuta Mererani**

42. **Mheshimiwa Naibu Spika**, tarehe 20 Septemba, 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa agizo la ujenzi wa ukuta katika eneo linalozunguka mgodi wa Tanzanite Mererani ili kuimarisha ulinzi na kudhibiti utoroshaji wa madini hayo. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu pamoja na Watanzania wote kuwa ujenzi wa ukuta huo wenye mzunguko wa kilomita **24.5** upo katika hatua za mwisho na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2018.

**(c) Mwenendo wa uwekezaji kupitia wachimbaji wadogo**

43. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imeendelea na mkakati wake wa kuimarisha uwekezaji katika rasilimali za madini, kupitia wachimbaji wadogo. Aidha, tangu mwaka 2000 hadi kufikia Desemba, 2017 kuna jumla ya leseni hai za uchimbaji mdogo **33,920** kwa nchi nzima. Kati ya hizo, leseni **6,976** zimetolewa kuanzia mwaka 2016/17 hadi hivi sasa. Serikali imetenga maeneo **46** yenye ukubwa wa jumla ya hekta **281,534**. Mpango wa Serikali ni kuwekeza katika utafutaji wa madini (*mineral exploration*) katika maeneo yaliyotengwa ili taarifa zivasaidie wachimbaji wadogo katika uwekezaji wao.

44. **Mheshimiwa Naibu Spika**, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kusaidia wachimbaji wadogo, natoa wito kwa wachimbaji wote wadogo kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uchimbaji madini kwa ajili ya usalama, afya na utunzaji mazingira. Vilevile, wanapaswa kutekeleza wajibu wao wa kulipa tozo stahiki.

**(d) Utatuzi wa migogoro katika maeneo ya machimbo**

45. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali inaendelea na juhudi za kutatua migogoro katika maeneo mbalimbali ya machimbo. Miongoni mwa maeneo hayo ni Nyamongo ambako kuna mgogoro kati ya mwekezaji Kampuni ya North Mara na wananchi.

**(e) Tume ya Madini**

46. **Mheshimiwa Naibu Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa uundaji wa Tume ya Madini unaendelea. Aidha, Katibu Mtendaji wa Tume hiyo ameshateuliwa na kikao cha kwanza cha Makamishna wa Tume kilifanyika tarehe 6 Januari, 2018. Kikao hicho pamoja na mambo mengine kilipitia mapendekezo ya uteuzi wa wafanyakazi katika nafasi mbalimbali ndani ya Tume. Hata hivyo, kazi za msingi za Tume kama utoaji wa vibali vya kusafirisha madini nje ya nchi (*export permit*) vinatolewa kwa usimamizi wa Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume hiyo.

**MIUNDOMBINU**

47. **Mheshimiwa Naibu Spika**, mvua kubwa zilizonyesha kwa kipindi cha mwezi Novemba 2017 hadi Januari 2018, zimeleta athari kubwa kwenye mtandao wa barabara nchini. Kutokana na mvua hizo, hali ya barabara zipatazo **50** katika mikoa **14** ziliathirika ambapo ilikuwa vigumu kupitika kwa urahisi.

48. **Mheshimiwa Naibu Spika**, baadhi ya Mikoa ambayo barabara zake ziliathirika na hali ya uwepo wa mvua nyingi ni pamoja na Arusha, Pwani, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Manyara, Mbeya, Mwanza, Rukwa, Simiyu, Ruvuma, Singida, Songwe na Tabora. Kwa sasa barabara hizo zimefanyiwa matengenezo ya dharura na zinapitika japo si kwa kuridhisha. Aidha, barabara **37** zilizofanyiwa matengenezo zinapitika kwa urahisi.

**ELIMU**

**(a) Mpango Elimumsingi Bila Malipo**

49. **Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza kwa mafanikio Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo kupitia Waraka wa Elimu No. 3 wa mwaka 2016. Waraka huu ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 sambamba na maelekezo ya Ibara

ya 52(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020 inayosisitiza utoaji wa Elimumsingi Bila Malipo.

**50. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2017, Serikali imetuma moja kwa moja shuleni jumla ya shilingi bilioni **124.8** kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo. Fedha zinazopelekwa moja kwa moja shuleni kwa mwezi ni shilingi bilioni **20.8** na shilingi bilioni **3.06** hupelekwa Baraza la Mitihani kwa ajili ya fidia ya gharama za mitihani kwa wanafunzi wa shule za Serikali.

**(b) Udhhibiti wa Michango Shuleni**

**51. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitoa Waraka wa Elimu Namba 3 wa mwaka 2016 ambao pamoja na mambo mengine, ulipiga marufuku michango ya aina yoyote isiyo ya lazima katika Elimumsingi.

**52. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika siku za hivi karibuni kumejitokeza malalamiko kuhusu baadhi ya shule kuchangisha michango mbalimbali kutoka kwa wazazi na walezi na kusababisha watoto kurudishwa nyumbani kwa sababu ya mzazi au mlezi kutochangia michango shuleni. Hali hiyo ni kinyume na maelekezo ya Serikali.

Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa watendaji wa elimu kuanzia Wakurungezi wa Halmashauri pamoja na wadau wote wa elimu kuzingatia maelekezo ya Waraka uliotolewa na Serikali ambapo majukumu ya kila mdau katika kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo yamefafanuliwa.

**53. Mheshimiwa Naibu Spika**, ruhusa ya michango shuleni ipo, kutoka mtu mmoja mmoja, vikundi au taasisi. Hata hivyo, michango yote sasa itafikishwa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili ashirikishe Kamati ya Shule kwa shule za msingi na Bodi za Shule kwa shule za sekondari. Walimu wasisumbuliwe na michango ili wajikite na taaluma.

**(a) Kulinda Mipaka na Viwanja vya Shule**

**54. Mheshimiwa Naibu Spika**, kufuatia kuwepo kwa changamoto ya umiliki wa ardhi kutokana na baadhi ya shule kutokuwa na hati miliki, Serikali inaendelea kukusanya taarifa kutoka shule mbalimbali za Sekondari kwa lengo la kujua hali ya umiliki wa ardhi katika shule hizo. Hatua hii ya awali inatarajiwa kuhusisha shule za Sekondari Kongwe zipatazo **89**.

Zoezi hilo litakapokamilika litawezesha Serikali kuandaa hati miliki kwa shule zenye umiliki wa Serikali na pia kufanya maamuzi kwa shule ambazo umiliki wake uko chini ya taasisi za dini. Aidha, kupitia zoezi hili maeneo ya mipaka ya shule ikiwemo viwanja vya michezo vitatambuliwa na kujumuishwa kwenye ramani za shule. Zoezi la ufuatiliaji wa umiliki wa ardhi kwa shule za msingi na shule za Sekondari zilizobaki za Serikali litaendelea kufanyika ili kuondoa changamoto za migogoro ya ardhi.

**MAJI**

**(a) Utekelezaji wa Miradi ya Maji Katika Halmashauri**

**55. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeendelea kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri zote nchini kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliyoanza mwaka 2006 hadi 2025. Lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwa hadi kufikia mwaka 2020, hali ya huduma ya upatikanaji wa maji inafika **asilimia 85** kwa wananchi waishio vijijini na **asilimia 95** kwa wale waishio mijini.

**56. Mheshimiwa Naibu Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2017, jumla ya **shilingi bilioni 55.6** za bajeti ya miradi ya maji kwa mwaka 2017/2018 zilipelekwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji. Jumla ya miradi **1,466** sawa na asilimia **80.99** ya miradi yote **1,810** iliyopangwa kutekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imekamilika. Miradi

Iliyobaki ambayo ni **376** na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, kutokana na changamoto za kuharibika kwa miundombinu ya maji, jumla ya vituo vya kuchotea maji **83,575** kati ya **122,655** vilivyojengwa ndivyo vinavyofanya kazi na vinahudumia wananchi wa vijijini wapatao **20,893,750** sawa na **asilimia 56** ya wananchi hao.

**57. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Juni, 2020 utekelezaji wa programu hii umelenga kujenga, kukarabati na kuongeza wigo wa miradi ya maji katika **vijiji** ambapo **vijiji 4,105** vitanufaika na mpango huo. Hali kadhalika, vituo vipatavyo **76,334** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia **watu 19,080,000** vinatarajiwa kujengwa.

*(a) Ubadhirifu wa Fedha za Miradi ya Maji*

**58. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imeendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wanaohusika na ubadhirifu wa fedha za miradi ya maji katika Halmashauri na Sekretarieti za Mkoa. Mathalan, wakati wa ziara yangu ya kikazi katika mkoa wa Mara mwezi Januari, 2018 nilibaini kuwepo kwa mapungufu kadhaa kwa watendaji wa sekta ya maji mkoani humo. Mapungufu hayo yalichangia kwa kiasi kikubwa kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maji licha ya Serikali kutuma fedha kila ilipotakiwa kufanya hivyo.

**59. Mheshimiwa Naibu Spika**, kutokana na ubadhirifu huo Serikali imelazimika kuagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa, ifanye uchunguzi na kuivunja Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma. Ntoa maelekezo kwa Wakuu wote wa Mkoa na Wilaya wafuatilie utekelezaji wa miradi ya maji iliyopo katika maeneo yao ili wajiridhishe kuwa huduma ya maji safi inapatikana mijini na vijijini.

## **KUHAMIA DODOMA**

**60. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutekeleza azma yake ya kuhamishia shughuli

za Serikali Kuu mjini Dodoma. Aidha, napenda pia kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ofisi yake walihamia rasmi Dodoma tarehe 15 Desemba, 2017 kama ilivyopangwa. Nitumie nafasi hii kumpongeza na kumkaribisha sana Mheshimiwa Makamu wa Rais kwenye Makao Makuu ya nchi mjini Dodoma.

**61. Mheshimiwa Naibu Spika**, aidha, kufuatia utekelezaji wa Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Watumishi wa Umma kuhamia Dodoma, jumla ya Watumishi **3,829** kutoka wizara na taasisi mbalimbali za Serikali tayari wamehamia Dodoma. Ujio wao huo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu Dodoma, aliyoyatoa tarehe 23 Julai 2016. Wito wangu kwao ni kwamba watambue wameshafika Dodoma na hatutarajii kuwakuta tena Dar es Salaam.

*(a) Mpango wa Kuifanya Dodoma Kuwa ya Kijani*

**62. Mheshimiwa Naibu Spika**, kuhamia kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais mjini Dodoma kumeongeza hamasa ya kuboresha mazingira ya mji huu, hususan baada ya kuzindua rasmi kampeni maalumu ya upandaji miti mjini Dodoma maarufu kama "**Kampeni ya Kijanisha Dodoma**".

**63. Mheshimiwa Naibu Spika**, Serikali imedhamiria kuifanya Dodoma ambayo ndiyo Makao Makuu ya nchi, kuwa na Ukanda wa Kijani (Green Belt) kupitia mpango huo. Mpango huo unahusisha kuendeleza, kutunza na kuhifadhi maeneo ya ukanda wa kijani ambayo ni pamoja na msitu wa Mahomanyika wenye ukubwa wa hekta **2,000**, msitu wa Chimwaga Nzuguni wenye ukubwa wa hekta **300** na msitu wa Mbwendelo wenye ukubwa wa hekta **3,500** pamoja na vilima vya Image na Nyankali.

**64. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kutimiza malengo hayo ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani, Serikali imeendelea kutoa elimu ya upandaji miti na uhifadhi wa misitu hususan

miti adimu ya asili na makao ya wanyamapori mbalimbali katika kata **nane** za Ipala, Nzuguni, Kikombo, Ng'ong'ona, Chahwa, Zuzu, Hombolo na Kikuyu Kaskazini. Aidha, kila kata imepewa lengo la kupanda miti isiyopungua **40,000**.

**65. Mheshimiwa Naibu Spika**, kwa upande wa zoezi la upandaji miti, jumla ya miche **34,000** yenye thamani ya Shilingi **34,000,000** imetolewa bure katika kata mbalimbali. Vilevile, kupitia mradi wa TASAF jumla ya miche **138,000** imeoteshwa na inaendelea kusambazwa kwa wananchi. Aidha, kwa sasa Manispaa ya Dodoma inaendelea na Maandalizi ya kuotesha miche mingine ipatayo **200,000** kwa ajili ya msimu ujao.

**66. Mheshimiwa Naibu Spika**, napenda niwashukuru wadau mbalimbali kikiwemo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Bonde la Wami Ruvu, Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) ambao kwa kushirikiana na Manispaa ya Dodoma wamefanikisha upandaji wa miche **79,000** katika maeneo ya UDOM, Mzakwe, Iseni *Park*, Nala na Mahomanyika.

**67. Mheshimiwa Naibu Spika**, katika kuhakikisha zoezi la upandaji miti linakuwa endelevu pamoja na kuongeza usimamizi, naziagiza Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinaandaa miche ya kutosha na kuweka utaratibu wa kila kaya kupanda na kutunza miti isiyopungua mitano. Taarifa za utendaji na maendeleo za Halmashauri zote zioneshe mafanikio yaliyopatikana kutokana na zoezi la upandaji miti. Aidha, utendaji wa Wakurugenzi na Wakuu wote wa Mikoja na Wilaya utapimwa kutokana na uendelezaji na utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

**(b) Uendelezaji wa Makazi na Mpangilio wa Mji wa Dodoma**

**68. Mheshimiwa Naibu Spika**, kufuatia agizo la Serikali la kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma, mahitaji ya viwanja hadi mwezi Februari 2018 yalikuwa viwanja **24,602**. Katika kukabiliana na changamoto ya mahitaji ya viwanja, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma hivi sasa inatekeleza

mkakati wake wa kuzalisha viwanja **30,000** kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, tayari upimaji wa viwanja vipya **15,316** umekamilika na kazi inaendelea. Viwanja hivi vitaanza kugawiwa kuanzia tarehe 30 Machi 2018. Kiasi kilichobaki cha viwanja **14,684** kitakamilika ifikapo Juni, 2018. Wananchi watauziwa viwanja hivyo kwa bei elekezi itakayotolewa na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.

**69. Mheshimiwa Naibu Spika**, natoa wito kwa wananchi na watumishi wa umma watakaohitaji viwanja wafuate taratibu za maombi ya viwanja pindi vitakapotangazwa rasmi. Zoezi la kubadilisha hati zilizotolewa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) na kupata **HATI MILIKI** za miaka 99 linaendelea. Wenye hati za CDA mnasisitizwa kuendelea na taratibu za kuzibadilisha.

#### **HITIMISHO**

**70. Mheshimiwa Naibu Spika**, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu napenda nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutuongoza vema ndani ya Bunge lako tukufu. Vilevile, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge ambao kwa umahiri mkubwa wamekuwa wakiendesha vikao vya Bunge hili tukufu. Kadhalika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu mbalimbali muhimu katika kuboresha maisha ya wananchi wetu kwa ujumla. Nimshukuru Katibu wa Bunge na wasaidizi wake kwa huduma nzuri na msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa hapa Bungeni.

**71. Mheshimiwa Naibu Spika**, mwisho, niwashukuru watendaji wa Serikali na taasisi mbalimbali kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa na hivyo, kufanikisha shughuli zilizopangwa za Bunge lako tukufu bila kuwasahau wanahabari kwa uchambuzi wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge na kufikisha habari hizo kwa wananchi. Vilevile, niwashukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma ambazo wamekuwa wakizitoa kwa washiriki wa Bunge hili. Pia, niwashukuru madereva wote waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa. Nawatakia kheri kwa safari ya kurejea nyumbani.



**72. Mheshimiwa Naibu Spika**, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe hoja kwamba Bunge lako tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumanne tarehe **3 Aprili 2018** saa tatu asubuhi katika ukumbi huu, hapa mjini Dodoma.

**73. Mheshimiwa Naibu Spika**, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono sasa tukae ili niweze kuwahoji.

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawa hoji, wanao hafiki hoja ya kuhairisha Bunge ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hivyo hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imepita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa kutupa maelezo marefu ya utekelezaji wa mambo mbalimbali kwa upande wa Serikali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hiyo ndiyo taarifa rasmi ya hicho kipindi kilichopita lakini kabla hatuja endelea nayo mambo mawili hapa halafu tutamalizia ratiba yetu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akihitimisha hoja Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama nilimwambia kwamba asitoe maelezo kuhusu mradi wa *passport* kwa sababu Mheshimiwa Msigwa ataenda kwake. Jambo hili limeelekezwa kwenda kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madara ya Bunge na siyo Kamati ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na sababu ya msingi ya kupeleka kwenye Kamati hii ni kwa sababu Bunge linataka kujiridhisha na

taarifa alizosema Mheshimiwa Msigwa ili liweze kuchukua hatua sitahiki. Kwa hiyo, inaenda kwenye Kamati ya Maadili ili tusiipungukie Kanuni ya 63 inayokataza kusema uwongo Bungeni ili ni kama ni kweli Bunge liweze kuchukua hatua kwa huo ufisadi unaozungumzwa kuhusu mradi wa uhamiaji kielektroniki.

Waheshimiwa Wabunge. jambo lingine la mwisho nilishotoa maelekezo kwa mwongozo wa Mheshimiwa Khatib aliokuwa ameomba kuhusu maswali yanayopelekwa Ofisi ya Katibu, sasa hili sikusudii kurudia nilichozungumza, lakini Ofisi imeniletea taarifa hapa.

Kwa hiyo, nataka kuwa taarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba mkienda Ofisi ya Bunge inayohusika na maswali mtakutana huko na taarifa ambayo hata mimi nimeletewa hapa ambayo inazungumza kwamba kila Mbunge kashapeleka maswali mangapi na ya kwake yameshajibiwa mangapi. Sasa nitatoa mifano miwili ili tuelewane vizuri Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Khatib yeye maswali aliyokwisha kupeleka mpaka sasa ni maswali 14 na ameshajibiwa maswali tisa ndani ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge Mbunge ambaye ameshajibiwa maswali kwa wingi kabisa ni yule ambaye amejibiwa maswali 13 na hao wako Wabunge kama wawili tu hivi. Kwa hiyo, maswali tisa ni mengi kabisa kwa sababu wako ambao wamejibiwa swali moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuangalie huo uwiano hii karatasi mtaikuta hiyo Ofisi ya Bunge ili uweze kujibiwa maswali yako yale ambayo unaona ni mengi na hayaja fanyiwa kazi. Kwa hiyo, wanayo idadi ya maswali uliyopeleka na idadi ya maswali ambayo yameshajibiwa humu Bungeni. Kwa hiyo, hii taarifa iko wazi Waheshimiwa Wabunge na iko tayari kwa ajili yenu ili mkatazame hayo.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwan Wabunge, naomba sasa tusimame ili tuweze kuimba wimbo wa Taifa.

*(Hapa Wimbo wa Taifa Ulimbwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumanne, tarehe 3 Aprili, 2018, saa tatu asubuhi.

*(Saa 8:33 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 3 Aprili, saa Tatu Asubuhi)*